Nipashe
Jumatano Mei 15, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0579918
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



**Bil. 200/- zamwagwa kumaliza kero mafuriko Mto Msimbazi**

UKURASA 3







UKURASA 13

## SAKATA LA KOROSHO

# Kabudi, Gavana wakaliwa kooni

**KAMBI** ya Upinzani yataka wajiuzulu kwa kuisababishia serikali hasara ya mabilioni, kisa?...

*Endelea Ukurasa. 2*



Prof. Luoga

Prof. Kabudi



## Dk. Bashiru awatemea cheche tena wanasiasa

UKURASA 3

MASUMIN PRINTWAYS & STATIONERS LTD
WYSEN
FiveStar
mondi business paper
CASIO
hp
Canon
nashuatec
DELL
EPSON
APC
Microsoft
KYOCERA
Datacard
CITIZEN
kangaro
NATARAJ
DYMO
Pritt
logitech
ZEBRA
Fellowes
UNOMAT
SanDisk
uni-ball
FALCON SAFE
Masumin Tower, Jamhuri / Mrima Street, P.O. Box 20073, Dar es Salaam, Tanzania
TOLL FREE: 0800-11-00-24
BEST OF TANZANIA
www.masumin.co.tz
Masumin printways

# CAG Assad aweka msimamo mzito

UKURASA 2

**MICHEZO** AZAM FC WAPATA KAULI SARE SIMBA UK. 31

**MAONI** UKURASA 5 **II** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Kabudi, Gavana wakaliwa kooni

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

KAMBI Rasmi ya Upinzani Bungeni, imewataka viongozi wote walioshiriki kutia saini makubaliano na Kampuni ya Indo Power ya Kenya kwa ajili ya ununuzi wa korosho kujiuzulu kutokana na kuisababishia serikali hasara kubwa kwa uamuzi huo.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana hotuba kuhusu makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka ujao wa fedha, Cecil Mwambe, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi hiyo, Anthony Komu, alisema uamuzi huo umeisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani milioni 500 (Sh. trilioni 1.1).

Waziri kivuli huyo alilieleza Bunge kuwa Juni, mwaka jana, serikali ilizindua awamu ya pili ya mpango wa kuendeleza sekta ya kilimo ambao unatekelezwa kwa miaka 10 ambao malengo yake ni pamoja na kuongeza tija katika uzalishaji na kufanya kilimo kiwe cha kibiashara.

Hata hivyo, wakati serikali ikifanya hivyo, Mwambe aliliambia Bunge kuwa mapema mwaka huu, serikali kupitia Bodi ya Nafaka Mchanganyiko (CPB), iliingia makubaliano na kampuni hiyo ya Kenya kwa ajili ya ununuzi wa korosho tani 100,000 kwa bei ya Dola za Marekani milioni 180.2 (Sh. bilioni 418).

Alisema hatua hiyo ilichukuliwa baada ya mipango, mikakati na maelekezo ya serikali kuhusu korosho kushindwa kutekelezeka na kusababisha hasara kubwa kwa wakulima wa zao hilo wanalolitegemea kama zao la biashara.

"Hata hivyo, miezi minne baadaye serikali imevunja mkataba na kampuni hiyo kwa kile kilichoelezwa kuwa kampuni hiyo kushindwa kutekeleza mkataba huo," alisema.

Mwambe alisema mkataba huo ambao serikali iliingia, ulitiwa saini mbele ya Waziri wa Katiba na Sheria (kipindi hicho Prof. Palamagamba Kabudi), Naibu Waziri wa Kilimo, Dk. Innocent Bashungwa, na Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda.

Tukio la kutiwa saini kwa mkataba huo jijini Arusha Januari 30, pia lilishuhudiwa na Gavana wa Benki Kuu (BoT), Prof. Florens Luoga, Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Balozi wa Kenya nchini, Dan Kazungu na makatibu wakuu wa wizara zinazohusika.

"Lakini tunaamini pia vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vina jukumu katika mikataba hii ambayo taifa linaingia. Taarifa za kwamba kampuni hii imeshindwa kutekeleza vifungu vya kimkataba inatia ukakasi kwa kuwa lilikuwa wajibu wa seri

INAENDELEA UK 8

twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

**TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY**

**TAARIFA KWA WANAHISA**

Taarifa inatolewa kwa wanahisa wote wa Tanzania Portland Cement Public Limited Company kwamba Mkutano Mkuu wa Mwaka wa Wanahisa utafanyika:
**Ramada Beach Resort, Grand Ocean Hall, Ground Floor**
**Jangwani Beach, Plot 170-171,**
**Mbezi Beach, Dar es Salaam,**
**siku ya Ijumaa, tarehe 7 June 2019, saa nne asubuhi.**

**DONDOO**
1. Ufunguzi wa Mkutano: Katibu asome taarifa iliyotolewa kuuita Mkutano Mkuu na kuhakiki kama akidi ya Mkutano imetimia.
2. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 26 uliofanyika tarehe 30 Mei 2018.
3. Kupokea, kujadili na kama zitaafikiwa kupitisha taarifa ya wakurugenzi, taarifa ya wakaguzi na taarifa ya fedha kwa mwaka ulioisha tarehe 31 Desemba 2018.
4. Kupokea, kujadili na kama itaafikiwa kuthibitisha gawio la mwaka 2018.
5. Kuthibitisha uteuzi wa wakaguzi wa mahesabu kwa mwaka unaoisha tarehe 31 Desemba 2019.
6. Kuthibitisha kuchaguliwa upya kwa wakurugenzi Bi Ruth Zaipuna na Bw Oswald Urassa watakaowakilisha wanahisa wenye hisa chache kwenye Bodi ya Wakurugenzi hadi mkutano mkuu wa mwaka 2022.
7. Azimio Maalum: Kujadili na kama itaafikiwa, kupitisha azimio lifuatalo kama azimio maalum, kama lilivyopendekezwa na wakurugenzi:
"Kwamba jina la kampuni libadilishwe kutoka "Tanzania Portland Cement Company Limited" na liwe "Tanzania Portland Cement Public Limited Company" kuanzia tarehe tajwa kwenye Cheti cha Mabadiliko ya Jina ambacho kilitolewa na ofisi ya Msajili wa Makampuni".
8. Kujadili mambo mengine ya kampuni ambayo taarifa zake zimepokelewa.

Kwa Niaba ya Bodi
Tarehe: 15 Mei, 2019

Brian Kangetta
Katibu wa Kampuni

215228202

1. Mwanahisa yeyote aliye na haki ya kuhudhuria na kupiga kura kwenye mkutano, anaruhusiwa kuteua mwakilishi au wawakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake. Fomu ya kuteua mwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya kampuni (https://www.twigacement.com). Mwakilishi atakayeteuliwa siyo lazima awe mwanahisa wa kampuni. Fomu ya kuteua mwakilishi ambayo imejazwa na mwanahisa inatakiwa iwasilishwe kwenye ofisi za kampuni, Wazo Hill, Dar es Salaam angalau masaa 24 kabla ya muda wa kuanza mkutano, la sivyo fomu itakuwa haijakidhi vigezo.
2. Kwa ajili ya utambulisho, mwanahisa anatakiwa kuja na cheti cha umiliki wa hisa pamoja na kitambulisho chake (pasi ya kusafiria, leseni ya udereva, au kitambulisho cha taifa, cha kazi, au cha mpiga kura).
3. Mahesabu kamili ya kampuni, ambayo yamepitishwa na wakaguzi, yanapatikana kwenye ofisi za kampuni, Wazo Hill, Dar es Salaam, au pia kupitia tovuti ya kampuni (https://www.twigacement.com).




Makamu Rais wa Kampuni ya mafuta ya Total Kanda ya Afrika, Kaskazini, Kati na Afrika Mashariki, Jean Philippe Torres (kushoto), akibadilishana mawazo na Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa Total Tanzania, Tarik Moufaddal, wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali, Total kufanya utafiti wa mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kwa kushirikiana na Kampuni ya mafuta ya Total inatarajia kufanya utafiti wa mafuta nchini na kiwango kitakachogundulika kuwezesha kuubadili uchumi wa nchi.

Waziri wa Nishati, Titus Kalemani, alisema hayo wakati wa hafla ya kuwapongeza wafanyakazi na wadau wa Total Tanzania, katika Maadhimisho Total ya miaka 50 nchini.

Waziri Kalemani alisema utafiti umethibitisha, kila mahali ilipogunduliwa gesi asili, chini yake kuna mafuta, hivyo serikali imeanza mazungumzo na kampuni ya Total Tanzania, ili kufanya utafiti wa mafuta na kuwataka Watanzania kuipatia ushirikiano kampuni hiyo.

Aliipongeza kampuni hiyo kwa kazi zake kubwa sita inazozifanya nchini Tanzania, ikiongozwa na kuuza mafuta, vilanishi vyenye ubora, kujenga bomba la mafuta la Uganda, kusambaza nishati mbadala ya nishati jua, kutoa ajira za kudumu na za muda kwa Watanzania na kuchangia huduma kwa jamii.

Kwa upande wake Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji wa Total Tanzania, Tarik Moufaddal, alisema katika kipindi cha miaka 50, kampuni hiyo imefanya makubwa na kuongoza kwa wingi wa vituo vya mafuta, kuuza mafuta yanayoongoza kwa ubora na vilanishi vyenye ubora na kutoa huduma za jamii.

Sherehe za Maadhimisho hayo, zilizinduliwa wiki iliyopita na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, ambaye pia aliwakabidhi zawadi mbalimbali wafanyakazi wa muda mrefu wa kampuni hiyo na wadau wake.

# CAG aweka msimamo mzito

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MDHIBITI na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), Profesa Mussa Assad, amesema maofisa wa ofisi yake wanatakiwa kufanya kazi kwa kujiamini na kutoogopa chochote wanapotekeleza majukumu yao.

Profesa Assad aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati akifungua Baraza la Wafanyakazi wa ofisi yake na kusisitiza kuwa wanapaswa kuhakikisha wanajibu hoja kwa wakati ili kuonyesha msimamo kwenye kazi zao.

Alisema hakuna sababu ya watumishi wa ofisi hiyo kuwa na woga katika utendaji wao, hivyo wanapaswa kuwa mfano ili kufanya kazi kwa ufanisi.

Kwa mujibu wa CAG, kuna baadhi ya mifumo ambayo inahitajika katika ukaguzi ambayo alisema wakiipata watafanya kazi vizuri.

Mbali na hilo, Prof. Assad alipongeza viongozi waliochaguliwa kwa ajili ya kuongoza baraza hilo na kuwataka kufanya kazi na wasibweteke.

Alisema viongozi wa baraza hilo wanapaswa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha wanasukuma gurudumu hilo kwa maslahi ya wafanyakazi.

"Nawaomba mchape kazi na msibweteke," alisema Professa Asad.

Naye mgeni rasmi katika mkutano huo, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (Utumishi), Dk. Francis Michael, alisema utovu wa nidhamu na rushwa katika mabaraza havitakiwi kabisa.

Alisema kinachotakiwa ni kufanya kazi kwa bidii ili waweze kusaidia wafanyakazi kwa ujumla.

Alisema bajeti zinatakiwa zijadiliwe na Baraza kabla ya kupelekwa bungeni ili kuhakikisha wanazitendea haki.

HABARI KITAIFA

# Mto Msimbazi kujengwa kwa bil. 200/-

**Na Mary Geofrey**

CHANGAMOTO ya mafuriko katika bonde la Mto Msimbazi, inatarajiwa kufika kikomo baada ya serikali kuahidi kuanza kufanya upembuzi yakinifu mwezi ujao kwa kuanza ujenzi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, wakati alipofanya ziara ya kukagua athari za mvua katika eneo la Jangwani, alisema tayari Sh. bilioni 200 zimeshatolewa kama mkopo na Benki ya Dunia (WB) kwa ajili ya kazi hiyo.

Alisema maeneo yote ya bonde hilo yataboreshwa kwa kujengwa majengo ya miundombinu ya kisasa ili kuondokana na changamoto ya mafuriko yanayoleta athari kwa wananchi na wakazi wa maeneo hayo.

"Kuanzia mwezi ujao tutaanza kufanya upembuzi yakinifu kwaajili ya ujenzi wa bonde la mto Msimbazi wenye urefu wa kilometa 19 na tayari fedha zipo kwa ajili ya kazi hiyo," alisema Makonda.

Alisema pia serikali imeanza kufanya ukarabati wa miundombinu iliyoathiriwa na mvua zinazoendelea kunyesha ikiwamo madaraja, barabara, mito na mifereji.

Aidha, Makonda aliwapa pole wananchi waliokumbwa na athari za mafuriko wakiwamo ambao mali zao zimeharibiwa na wengine kulazimika kuyahama makazi yao.

Makonda pia aliwataka wananchi wanaoishi maeneo hatarishi kuhama huku akiwataka wakazi wa jiji hilo kufanya usafi katika mazingira yao ili kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Kwa upande wa wananchi wanaoishi Jangwani, walilieleza Nipashe kuwa, serikali imekuwa ikitoa ahadi hewa ya kuboresha bonde hilo.

Mmoja wa wananchi hao, Jumanne Mrisho alisema, hawapo tayari kuhama kwa sababu serikali imekuwa ikiwafukuza na kuwabomolea nyumba zao bila kufanya muendelezo wowote katika eneo hilo.

"Sisi tumekaa Jangwani kwa muda mrefu, lakini hakuna siku ambayo serikali imelienleza eneo hili. Kama wameahidi watajenga waje ila hatutaondoka mpaka tuwaone wakifanya kazi," alisema Mrisho.

Mwaka jana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, alikaririwa na vyombo vya habari akisema ndoto yake ni kuona eneo la Mto Msimbazi linaboreshwa na kuwekwa vivutio mbalimbali, maeneo ya kupumzika, maduka na hoteli kupitia fedha zitakazotolewa na Benki ya Dunia.

Agosti mwaka jana, Mhandisi Mshauri Mussa Nati, aliwasilisha andiko la utekelezaji wa mradi uboreshaji wa bonde hilo katika mkutano wa udhibiti wa maafa hatarishi uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema utafiti uliofanyika unaonyesha kuwa baadhi ya makazi ya watu yataondolewa ili kupisha ujenzi wa mradi huo ambao utawezesha maji kwenda katika mkondo wake hadi baharini.

Nati alisema mradi huo ulianza kwa kutambua eneo lenye tatizo, namna ya kupunguza kwa kuishirikisha jamii na wataalamu, kufundisha jamii na kuandaa wataalamu wa baadaye pamoja na mitaala kwa ajili ya kutumika kwenye vyuo mbalimbali nchini.

Mwaka 2015, Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (Nemc), liliendesha bomoabomoa kwa wakazi wa eneo la Bonde la Msimbazi, Kinondoni, ikiwa ni pamoja na maeneo mengine ya usawa wa mto Msimbazi na nyumba zaidi ya 150 zilibomolewa.

# Dk. Bashiru awatemea cheche wanasiasa

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amekemea wanasiasa wanaoingilia na kuwadhalilisha watoa huduma za afya wakiwamo madaktari na wauguzi.

Dk. Bashiru alieleza kusikitishwa na vitendo hivyo baada ya Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) na Taasisi isiyo ya kiserikali ya Sikika, kufanya mazungumzo naye ofisi kwake jijini Dodoma jana.

Walifanya mkutano huo kwa ajili ya kujadili uhusiano na mawasiliano kati ya wanasiasa na watoa huduma za afya.

Katika mazungumzo hayo, pia walijadili kuhusu bajeti ya afya na changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya afya Tanzania.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo iliyotiwa saini na Rais wa MAT, Dk. Elisha Osati na Mkurugenzi Mtendaji wa Sikika, Irenei Kiria, Dk. Bashiru alisema hakuna mtu anayewatuma wanasiasa kufanya hivyo na kuwataka wadau wote kushirikiana na kuwalinda wataalamu wa afya na kuwakinga dhidi ya udhalilishaji.

"CCM iko tayari kushirikiana na wataalam wa afya kutengeneza mazingira bora ya ushirikiano kati yenu na wanasiasa ili kuwahudumia wananchi ipasavyo," alisema.

Katika kuondokana na mgongano huo, Dk. Bashiru aliwataka wadau wa afya kutengeneza mkakati wa kutoa elimu ya namna bora ya mawasiliano kati ya wanasiasa na wataalam wa afya.

INAENDELEA UK 26

IPPmedia



IPP Media tunatoa shukurani za dhati kwa Vyombo vyote vya Habari vilivyoshirikiana nasi katika kuchapisha na kurusha mubashara **MSIBA MZITO wa MPENDWA WETU MWENYEKITI MTENDAJI WA IPP - DKT. REGINALD MENGI.**

Aidha tunawashukuru kwa mchango wenu wa hali na mali mliotoa katika kipindi chote cha **MSIBA.**

***Tunasema asante sana kwa:-***

**TV WASHIRIKA:**
1. CLOUDS TV
2. AZAM TV
3. TBC
4. STAR TV
5. CHANNEL 10
6. TV ONE
7. TV E
8. TOP TV UKONGA
9. RISE AND SHINE TV
10. WASAFI TV
11. DIRA TV
12. UPENDO TV

**RADIO WASHIRIKA:**
1. CLOUDS FM
2. MAGIC FM
3. E FM
4. TIMES RADIO
5. RADIO FREE AFRICA
6. RADIO 5
7. PASSION FM
8. PAMBAZUKO FM IFAKARA
9. TOP RADIO MOROGORO
10. HIGHLANDS FM
11. PLANET FM
12. KILI FM MOSHI
13. SUNRISE RADIO ARUSHA
14. UHAI FM
15. UPENDO RADIO
16. WASAFI RADIO

**MITANDAO:**
1. CLOUDS DIGITAL
2. GLOBAL ONLINE TV
3. MILARD AYO
4. MICHUZI BLOG
5. POA TV
6. AZAM DIGITAL
7. WASAFI DIGITAL

**MAGAZETI:**
1. MWANANCHI/THE CITIZEN
2. DAILY NEWS/HABARI LEO
3. MTANZANIA
4. TANZANIA DAIMA
5. GLOBAL PUBLISHERS
6. UHURU/MZALENDO
7. JAMHURI
8. MAJIRA
9. TAZAMA

***Na kwa wengine wote walioshiriki nasi kwa njia moja au nyingine tunasema AHSANTE SANA NA MUNGU AWABARIKI.***

# Waliobinafsishwa viwanda sasa wanukia Mahakama ya Mafisadi

**Na Sanula Athanas, DODOMA**

SERIKALI imetangaza kuwachukulia hatua kali za kisheria wawekezaji waliobinafsishiwa viwanda kisha kuvichukulia mikopo mikubwa benki na kushindwa kulipa.

Akiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana, hotuba ya makadirio kwa mwaka ujao wa fedha, Waziri wa Viwanda na Biashara, Joseph Kakunda, aliwataka wawekezaji hao kuhakikisha wanamalizana na benki walikochukua mikopo kufikia Mei 31, mwaka huu.

Alisema hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wote watakaokaidi agizo hilo la serikali kwa kuwa kwa kuchukua mikopo hiyo mikubwa walitenda kosa la uhujumu uchumi, hivyo kuwa hatarini kufikishwa kwenye Mahakama ya Mafisadi.

"Nachukua nafasi hii kuwatahadharisha wahusika wote walioko ndani na nje ya nchi kwamba kwa kufanya hivyo walitenda kosa la uhujumu uchumi. Nawaonya kwamba wahakikishe wamemalizana na mabenki kwa kulipa mikopo yao yote ifikapo Mei 31, mwaka huu," alisema.

Kakunda aliongeza kuwa serikali haitaongeza muda ambao walipaswa kuleta maelezo yenye kueleweka serikalini kuhusu viwanda hivyo.

Kakunda alibainisha kuwa kati ya viwanda 156 vilivyobinafsishwa, 88 vinafanya kazi huku 68 vikiwa havifanyi kazi.

Alisema kati ya viwanda 88 vinavyofanya kazi, 42 vinafanya kazi vizuri sana, 46 vinafanya kazi kwa kiasi cha kuridhisha na 20 vimefutwa kwa sababu ubinafsishwaji wake ulifanywa kwa kuuza mali moja moja na vingine kuruhusiwa kubadili matumizi.

"Viwanda vingine 48 wamiliki wameshindwa kuviendesha kwa mujibu wa mkataba wa mauziano na hivi sasa, tayari viwanda 16 vimerejeshwa serikalini na vingine 32 wamepewa notisi ya kuwasilisha mipango ya kuviendeleza kabla ya Mei 31, mwaka huu," alisema.

Aliongeza kuwa viwanda 13 havikubinafsishwa kutokana na sababu mbalimbali na hivyo kuendelea kuwa mali ya umma chini ya Msajili wa Hazina. Pia alisema baadhi ya viwanda hivyo vinafanya kazi kwa kusuasua na vingine havifanyi kazi.



Wateja wakinunua mihogo katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam juzi. Mihogo hutumika kwa wingi kwa ajili ya futari kipindi hiki cha mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Shahidi adai Mbowe alishawishi maandamano

**Na Hellen Mwango**

SHABAN Abdallah (19), amedai mahakamani katika kesi ya uchochezi inayowakabili vigogo tisa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kuwa alimwona Mwenyekiti wa Taifa wa chama hicho, Freeman Mbowe, akiwahamasisha wananchi kuendelea kuandamana kuwasogelea askari hata baada ya tangazo la kuwaamuru kutawanyika kutolewa.

Abdallah ambaye fundi wa kuchomea vyuma na mkazi wa Kinondoni Moscow, Dar es Salaam, ni shahidi wa pili wa upande wa Jamhuri katika kesi hiyo, alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu Paul Kadushi, shahidi huyo alidai kuwa Februari 16, 2018 asubuhi alikuwa katika eneo lake la kazi Kinondoni Moscow anakoendesha shughuli zake za kumwingizia kipato kwa kutengeneza vitanda na vyuma.

Siku hiyo, alidai kuwa saa 11 jioni, alipewa fedha na bosi wake kwa ajili ya kwenda Mkwajuni kununua vifaa vya kazi na alifika dukani kwa mtu aliyemtaja kwa jina la baba John na kununua vitu hivyo.

"Nikiwa pale dukani wakati tunaendelea kufanya hesabu kabla ya kuchukua mzigo, kwa mbali tulisikia vurugu lakini hatukuzifuatilia sana. Muda ulivyozidi kwenda vurugu zilizidi kutusogelea, tulitoka dukani na kwenda nje kuangalia tukaona watu wengi katikati ya barabara wakitokea eneo la Morocco wakielekea Magomeni huku wakiwa wameshika mawe na marungu," alidai.

"Waandamanaji hao walionekana kuwa katika hali ya ugomvi na shari. Walikuwa wakiimba 'Hatupoi mpaka mmoja afe watatuua'. Kwa kuwaangalia mimi na baba John tuliweza kuwatambua kuwa ni watu wa Chadema kwa kuwa walikuwa wamevaa sare za chama hicho, skafu na bendera huku viongozi wao wakiwa mbele. Nilimwona na kumtambua Mbowe, Halima Mdee, John Mnyika na Esther Matiko," alidai shahidi huyo.

Alidai kuwa wakati wakiendelea kuwaangalia waandamanaji hao waliona gari la askari likija nyuma yao huku likiwatanga

INAENDELEA UK 8

## Vigogo 7 watumbuliwa Tume ya Umwagiliaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewasimamisha kazi Wakurugenzi saba wa Tume ya Umwagiliaji akiwamo Kaimu Mkurugenzi Mtendaji, ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazowakabili.

"CAG afanye haraka uchunguzi wa kina, tunataka kujua ni nani alikuwa mlango wa ubadhirifu huu. Hatutamuonea mtu, wote watakaothibitika kuhusika na matumizi mabaya ya fedha watachukuliwa hatua."

Waziri Mkuu alifanya uamuzi huo jana wakati wa kikao na viongozi wa tume hiyo kilichofanyika jijini Dodoma na kuhudhuriwa na Mawaziri, Manaibu Waziri na Makatibu Wakuu.

Mbali na kuwasimamisha kazi wakurugenzi hao, pia Waziri Mkuu ameagiza watumishi wengine 21 wa tume hiyo wachukuliwe hatua za kinidhamu kutokana na utendaji usioridhisha kwenye miradi mbalimbali inayosimamiwa na tume hiyo.

Waziri Mkuu amesema Serikali imechukua hatua hiyo kutokana na udhaifu wa kiutendaji ndani ya tume hiyo ikiwamo matumizi mabaya ya fedha za miradi, rushwa, matumizi mabaya ya madaraka, upendeleo na kukosa umakini. "Hatua kali zitachukuliwa dhidi ya ubadhirifu uliofanyika katika miradi ya umwagiliaji."

Alisema hali ya kilimo cha umwagiliaji nchini hairidhishi na Serikali haijafurahishwa na utendaji wa Tume ya Umwagiliaji licha ya kuwekeza nguvu kubwa, hivyo inataka kuona mabadiliko.

"Miradi mingi inayotekelezwa na Tume ya Umwagiliaji nayo ina hali mbaya zaidi. Miradi mingi ya tume hiyo imejikita katika mafunzo, semina na warsha badala ya kujenga na kuendeleza skimu za umwagiliaji."

Alisema tume hiyo imeshindwa kusimamia miradi takribani 10 katika maeneo mbalimbali nchini na kusababisha sekta ya umwagiliaji kushindwa kupata mafanikio yaliyotarajiwa kutokana na ubadhirifu.

Miongoni mwa miradi hiyo ni pamoja na mradi wa umwagiliaji wa Luiche unaokadiriwa kumwagilia hekta 3,000 ambao upo katika hatua za awali za utekelezaji lakini tayari pamekuwapo na matumizi mabaya ya fedha za mradi.

**HABARI KITAIFA**



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Spika wa Bunge, Job Ndugai, katika Viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Fatma Karume atishia kuishtaki upya serikali

**Na Enock Charles**

WAKILI wa kujitegemea, Fatma Karume, ametofautiana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kutishia kufungua kesi nyingine mpya.

Amesema atafanya hivyo iwapo kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Uchaguzi kinachoipa mamlaka Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), kuwateua wakurugenzi wa majiji, manispaa, miji kuwa wasimamizi wa uchaguzi na 7(3) kinachoipa mamlaka Nec kuteua wasimamizi wa uchaguzi miongoni mwa watumishi wa umma vitaendelea kutumika.

Akizungumza na gazeti hili jana, jijini Dar es Salaam, Mwanasheria huyo alisema ni makosa kuendelea kutumia sheria iliyobatilishwa na Mahakama mpaka hapo rufaa inayohusu kesi hiyo itakaposikilizwa.

"Nimesikia Dk. Kilangi anasema kuwa ile sheria itaendelea kutumika sasa nitampeleka mahakamani kwa kukiuka amri ya mahakama kwa sababu chini ya sheria yetu kama athari ya uvunjifu wa Katiba ni athari endelevu, sheria hiyo haiwezi kuendelea kutumika," Fatma alisema.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Dk. Adelardus Kilangi, alisema kuwapo kwa hukumu ya Mahakama Kuu iliyobatilisha vifungu 7(1) na 7(3), hakutaweza kuathiri chaguzi nyingine zijazo zikiwamo za marudio kwa kuwa baada tu ya kuwasilisha taarifa hiyo utekelezaji wa hukumu hiyo husimama.

Katika kesi ya msingi iliyofunguliwa na mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Bob Wangwe, akitetewa na Wakili Fatma Karume, mwanachama huyo aliiomba mahakama kubatilisha vifungu 7(1) na 7(3) vya Sheria ya Uchaguzi vinavyoipa mamlaka Nec kuwateua wakurugenzi wa majiji, manispaa, miji kuwa wasimamizi wa uchaguzi na 7(3) kinachoipa mamlaka Nec kuteua wasimamizi wa uchaguzi.

Akisoma hukumu hiyo wiki iliyopita mbele ya jopo la majaji watatu , Jaji Atuganile Ngwala, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi kifungu 7(1) na 7(3) ni batili kwa sababu kinatoa nafasi kwa wateule wa Rais ambao si waajiriwa wa Nec kusimamia uchaguzi wakati Katiba inasema Nec inapaswa kuwa huru.

Jaji Ngwala alisema kutokana na vielelezo vilivyowasilishwa mahakamani hapo na upande wa waleta maombi, vimeonyesha pasina shaka kuwa wasimamizi wa uchaguzi wana masilahi na wateule wao na kutokana na hali hiyo mahakama imeona vifungu hivyo ni batili.

Akizungumza na Nipashe jana, wakili mwingine wa kujitegemea Jebra Kambole, alisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali anayo haki ya kukata rufaa kuhusu uamuzi huo wa mahakama, lakini hana mamlaka ya kusimamisha hukumu hiyo bila kuiomba mahakama kufanya hivyo.

"Mahakama yenyewe ndiyo inaweza kutoa amri ya kuipa muda serikali wa kubadilisha sheria kama hukumu inasema hivyo hapo sawa, lakini kama mahakama ilibatilisha sheria hiyo, lakini si sahihi kusema iendelee kutumika eti kwa kuwa imekatiwa rufaa," Wakili Kambole alisema.

## Bunge lataka ushuru 15% uagizaji sukari ufutwe

**Na Mwandishi Wetu, DODOMA**

BUNGE limeishauri serikali kuachana na mfumo wa ushuru wa forodha wa asilimia 15 kwa waagizaji wa sukari ya viwandani.

Vilevile, limeshauri serikali kuwa makini wakati wa upangaji wa viwango vya kodi kwa kulinganisha na Jumuiya za Kikanda ambazo Tanzania ni mwanachama ili kuendana na masoko mengine na kuepuka kuwa soko la bidhaa za wengine.

Akiwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira bungeni jijini Dodoma jana kuhusu makadirio ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka ujao wa fedha, Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, Kanali mstaafu Masoud Alli Khamis, alisema mfumo huo ulianzishwa kwa lengo la kuwasimamia waingizaji wa sukari ya viwandani kuhakikisha wanaingiza nchini bidhaa hiyo kwa kuzingatia mahitaji halisi ya kiwanda.

"Utaratibu huu ni kuwa waagizaji wanatoa asilimia 15 ya import duty na fedha hizo zitarudishwa baada ya kuwasilishwa matumizi ya sukari hiyo. "Kamati inatambua nia njema ya serikali ya kuanzisha mfumo huu, lakini utekelezaji wake umekuwa na changamoto ambapo kwa miaka minne mfululizo tangu umeanzishwa, serikali imeshindwa kurejesha fedha hizi kwa wahusika, jambo lililopelekea kiasi cha mitaji wazalishaji kushikiliwa na serikali na kuwapunguzia mitaji yao.

INAENDELEA UK 8

## Mil. 800/- kutumika kuwalinda tembo

**Na Happy Severine, MEATU**

ZAIDI ya Sh. milioni 800 zinatarajiwa kutumika kwenye zoezi la kuwafungia tembo mkanda wenye mawasiliano na satelaiti, unaotumika kurusha taarifa ya mahali mnyama alipo.

Zoezi hilo lilizinduliwa jana kwenye Hifadhi ya Jamii ya Makao wilayani Meatu Mkoa wa Simiyu na Waziri wa Maliasili na Utalii, Khamis Kigwangalla.

Waziri Kigwangalla alisema idadi ya tembo imeongezeka kutokana na kupungua kwa ujangili, na kuongeza kuwa teknolojia hiyo itasaidia kujua tembo aliko au anakoelekea.

Alisema zoezi hilo litasaidia pia kuwalinda tembo sambamba na mali za wananchi, huku ikitambua idadi halisi ya tembo wanaoongezeka.

"Makundi ya tembo yameongezeka, ukijaribu kupita kwenye hifadhi zetu utaona idadi kubwa ya watoto wa tembo ...ukiona tembo wadogo ni wengi na taswira nzuri ya kujua ongezeko ni kubwa, hapa tunajua kuna uhai na mwendelezo," alisema Kigwangalla. Naye Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alisema uwapo wa hifadhi hizo katika mkoa wake umekuwa chachu ya kuongeza kasi ya maendeleo mkoani hapo ukiwamo ujenzi wa miundombinu ya shule na hospitali.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Simiyu, Enock Yakobo, aliomba mkoa uongezewe vifaa vya GPS kutokana na uwapo wa idadi kubwa ya tembo, huku akiongeza kuwa vifaa hivyo vitasaidia kuwawezesha wananchi kupata msaada kwa haraka kutokana na kuonekana walipo.

Dk. Emmanuel Masenga, kutoka Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI), alisema wanatarajia kuwafungia tembo 18 kifaa hicho kwenye Pori la Akiba la Maswa na Hifadhi ya Jamii ya Makao, na kuongeza kuwa zoezi hilo limefadhiliwa na Fredkin Conservation Fund kwa kushirikiana na serikali ya Tanzania.

Wakuu wa wilaya, Joseph Chilongani (Meatu) na Festo Kiswaga (Bariadi), walishukuru matukio ya ujangili wa tembo kupungua, na kubainisha kuwa matukio yaliyobakia ni tembo kuvamia na kuharibu mashamba na nyumba za watu.


**HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA**

**TAARIFA KWA UMMA**

Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) linapenda kutoa taarifa kwa Umma kwamba matangazo ya ajira yanayosambaa katika vyombo mbalimbali vya mawasiliano **SI SAHIHI** na kwamba TANAPA haijatangaza nafasi zozote za kazi kama inavyosambazwa.

Aidha, Shirika linaufahamisha umma kuwa mara baada ya kuainisha nafasi mbalimbali za ajira zinazotakiwa kujazwa, matangazo hutolewa kwenye vyombo mbalimbali vya habari kama magazeti na tovuti ya Shirika. Maombi ya nafasi za kazi hutumwa kwa njia ya mtandao "Aruti recruitment Portal" na **SI VINGINEVYO.**

Hivyo, tunapenda kutoa angalizo kwamba utaratibu wowote wa matangazo ya ajira kwa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania utakaoenda kinyume na huu, tafadhali upuuze.

**Imetolewa na**
**Kamishna wa Uhifadhi**
**Hifadhi za Taifa Tanzania**
**S. L. P 3134**
**ARUSHA.**

**Barua pepe: info@tanzaniaparks.go.tz**
**dg@tanzaniaparks.go.tz**

**Simu: +255 (27) 297 0404-07**

215229302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Miundombinu iboreshwe kuepusha mafuriko Dar

**KWA** takribani siku nane ambazo mvua za masika zimenyesha mfululizo katika Jiji la Dar es Salaam, athari zilitokea, vikiwamo vifo vya watoto wawili, hivyo funzo tunalolipata ni kuwa mwarobaini ni kuboreshwa kwa miundombinu.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, tukio la kwanza lilitokea Mei 8, mwaka huu, saa 9:00 alasiri maeneo ya Goba wilayani Kinondoni, ambapo mtoto mmoja alifariki dunia, baada ya kutumbukia kwenye kisima cha futi 30 kilichokuwa wazi nyumbani kwao.

Kamanda Mambosasa alisema mtoto mwingine ambaye anakadiriwa kuwa na umri wa miaka (4-5), alifariki dunia Mei 12, maeneo ya Mongo la Ndege, kwamba mwili wake ulikutwa ukielea katika Mto Msimbazi bila kuwa na jeraha lolote.

Mbali na vifo hivyo, wakazi wa maeneo kadha ya Jiji la Dar es Salaam wameathirika kutokana na nyumba zao kuzingirwa na maji.

Kadhalika, mvua hizo zimesababisha usumbufu mkubwa kwa wakazi wa Jiji kutokana na maji kuathiri miundombinu hususan baadhi ya barabara, hivyo baadhi kufungwa kwa muda, huku baadhi wakikwama kupita kwenye baadhi ya maoeneo kwenda kwenye shughuli zao za ofisi, biashara na za kijamii.

Baadhi ya miundombini ya taasisi iliathirika. Kwa mfano, Kamanda Mambosasa alisema, mvua hizo zimesababisha uharibifu wa baadhi ya majengo ya Shule ya Msingi Mwale iliyopo Kiwalani, Majani ya Chai Kiwalani na Shule ya Sekondari Kibasila iliyopo Manispaa ya Temeke ambayo imejaa maji na kusababisha kushindwa kuendelea na masomo.

Kutokana na hali hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ametoa tahadhari kwa wakazi wa jiji hilo waishio mabondeni kuhama maeneo yao.

Aliyataja maeneo yaliyofurika ni Jangwani, Magogoni Kigamboni, Ilala Kata ya Mchikichini, Kipunguni, Viwege, Majohe, Kata ya Tabata Madona na Temeke Shule ya Sekondari Kibasila.

Mengine ni Kinondoni Kata ya Kigogo, Tandale, Bunju eneo la Basihaya, Mwananyamala Mitaa ya Bwawani, Kambangwa, Msisiri 'A', Mbezi darajani na katikati ya Jiji.

Alisema Serikali inaendelea kuchukua hatua kurekebisha athari zilizojitokeza ili kuwaondolea adha wananchi kwa kuhakikisha mifereji iliyoziba inazibuliwa, kuweka madaraja ya muda pale madaraja yalipoharibiwa na maji, na kurekebisha barabara ili wananchi waendelee na shughuli zao.

Suala la kuboresha miundombimu lina umuhimu wa pekee katika kukabiliana na athari za mara kwa mara pale mvua zinapokuwa zinanyesha.

Hatua hizo zonaweza kuwa ujenzi wa madaraja ya muda katika maeneo ambayo yanakumbwa na mafuriko kama akivyosema Makonda, lakini pia ipo haja ya kujenga madaraja katika maeneo sugu kwa kuathiriwa na mafuriko kama Jangwani ili kurahisishia wananchi usafiri wakati wa mvua. Tukio la Jumatatu lililowasababishia usumbufu wakazi kadhaa wa jiji na kulazimisha kulipa nauli ya Sh. 1,000 hadi 2,000 kutoka Jangwani hadi Posta na Kariakoo baada ya barabara kujaa maji na kufungwa kwa muda, linapaswa kuchukuliwa kama somo, ili kujengwa miundombinu ya uhakika.

Ushauri wetu ni kuwa pamoja na mamlaka zetu kuwataka wananchi kuondoka katika maeneo ya mabondeni, pia zijishughulishe na kujenga mitaro ya maji katika maeneo mengi yanayoathirika kwa maji na barabara kutokupitika wakati wa mvua, ingawa sio ya mabondeni.

Ni matumaini yetu kuwa hatua za dharura zinaweza kuchukuliwa sasa kutokana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), kueleza kuwa mvua kubwa za masika zitaendelea kwa siku kadhaa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Wakati umepita wa kila kitu kufanywa na serikali

Na Raphael Kibiriti

MOJA ya mada zinazovuta mjadala mkubwa sehemu yoyote ile na katika kada mbalimbali za kimaisha, huwa ni ya maendeleo.

Ukianzisha mada ya kwa nini kwa mfano kanda fulani imeendelea ama mkoa, wilaya, tarafa, kata, mtaa, kijiji, kitongoji na hata mtu binafsi, utakumbana na hoja zenye mtazamo tofauti juu ya mada hiyo.

Si ajabu kukumbana na mitizamo isiyokubaliana juu ya vigezo vya maendeleo ya nchi zilizoendelea, zinazoinukia na hata jamii au mtu aliyeendelea.

Aidha, kuna mitazamo tofauti juu ya nani anayeleta maendeleo ya mtu ama watu katika jamii au maeneo yao.

Na ndiyo maana ya kusikia watu wakiilalamikia serikali kutojenga daraja, kutuchonga barabara, kutoleta kariveti kwenye mtaro ama hata kwa nini haijakata miti inayohifadhi vibaka katika maeneo yao.

Kwamba kila changamoto ya maendeleo, hata iwe ndogo kiasi gani iliyo kwenye uwezo wa wananchi, bado kuna watu katika baadhi ya maeneo watabaki wakisubiri serikali itatue changamoto hiyo.

Binafsi mtazamo huo sikubaliani nao, nikiongozwa na dhana kuwa, maendeleo ya watu huletwa na wao wenyewe kwa ushirikiano na serikali.

Ninajua kwamba, serikali ina wajibu na majukumu yake ya kufanya katika dhana nzima ya kuchangia maendeleo ya watu wake.

Na baadhi ya majukumu na wajibu wa serikali katika hilo ni pamoja na kudumisha amani kupitia sheria na amri zake mbalimbali na kulinda maisha na mali za watu wake.

Lakini pia kukuza demokrasia, haki za binadamu, kuzalisha ajira, kukuza maendeleo ya kiuchumi na kutoa huduma za kijamii kwa wananchi.

Huduma kama zile za kujenga miundombinu, hospitali, mabomba ya maji, umeme, elimu na zingine zenye mchango mkubwa wa kuboresha kiwango cha maisha ya wananchi.

Hivyo ni kweli kuwa serikali ina wajibu na majukumu ya kufanya kwa watu wake katika hiyo dhana nzima ya kuleta maendeleo.

Lakini, ambacho sikubaliani nacho ni kitendo cha wananchi kuiachia serikali kila kitu, hata kwa vitu ambavyo kimsingi viko kwenye uwezo wao.

Mara nyingi nimesoma malalamiko katika vyombo vya habari, nimesikia redioni na hata kuona kwenye televisheni wananchi wakiilalamikia serikali kwa changamoto ambazo wangeweza kuzitatua kwa kutumia rasilimali zao.

**Lakini, ambacho sikubaliani nacho ni kitendo cha wananchi kuiachia serikali kila kitu, hata kwa vitu ambavyo kimsingi viko kwenye uwezo wao.**

Kwamba wananchi wameshindwa 'kujiongeza' hata katika suala la kununua koki ya maji ili bomba liendelee kuwahudumia kwa muda mrefu, badala yake wanasubiri serikali ilete koki, ili waendelee kupata maji.

Unakuta wananchi wanailalamikia serikali kutowajengea kivuko ama daraja dogo la mbao au miti kwenye bonde dogo linalopitisha maji wakati wa masika, na hivyo kusababisha watoto wao wasiende shule, wakati wangeweza 'kujiongeza' kidogo tu na kutatua changamoto hiyo.

Nimesikia malalamiko ya wananchi dhidi ya serikali kwamba imeshindwa kudhibiti utoro wa wanafunzi wanaozagaa katika mitaa yao wakati walipaswa kuwa shuleni, kana kwamba hilo hawawezi kulidhibiti, wakisubiri serikali ije isaidie kupiga doria.

Muungwana hakubaliani na hili asilani la kuacha kutatua baadhi ya changamoto kwa msingi wa kuisubiri serikali izitatue, wakati wananchi wenyewe wangeweza kuzitatua mapema iwapo 'wangejiongeza'

Tuna maeneo hapa nchini ambayo yaliona umuhimu wa 'kujiongeza' muda mrefu kwa kutoitegemea serikali, na sasa yamepiga hatua kubwa sana za kimaendeleo.

Maeneo hayo hayakufungwa na upofu wa kuitegemea serikali kwa kila kitu na hata kwa changamoto zilizo chini ya uwezo wao.

Maeneo hayo yamepiga hatua kubwa za za kimaendeleo katika nyanja nyingi kama vile elimu, afya, maji na miundombinu kutokana na kulibaini hilo mapema.

Muungwana anatoa rai kwamba, sasa si muda wa wananchi kusubiri kila kitu kifanywe na serikali, na badala yake wahamasishane wao wenyewe kutatua changamoto za kimaendeleo zilizo chini ya uwezo wao.

# TANGAZO

## USHETU DISTRICT COUNCIL

**INVITATION OF TENDER FOR GEOPHYSICAL SURVEYING,DRILLING OF TWO (2) BOREHOLES AND PUMPING TESTING FOR BUTIBU VILLAGE IN USHETU DISTRICT COUNCIL.**

**Tender No: LGA/162/2018/2019/W/RWSSP/01-1**

**Date: 15th May 2019**

1. The Government of the United Republic of Tanzania has set aside funds for the operation of the **Ushetu District Council** during the financial year 2018/2019. It is intended that part of the proceeds of the fund will be used to cover eligible payment under the contract for the Geophysical Surveying, drilling of two (2) boreholes and pumping testing for Butibu Village in Ushetu District Council.

2. Ushetu District Council now invites sealed Tenders from eligible National contractors *(Surveying and drilling)* registered or capable of being registered in Class VII( Seven) and above for carrying out Geophysical Surveying, drilling of two (2) boreholes and pumping testing for Butibu Village in Ushetu District Council.

3. Tendering will be conducted through the National Competitive Tender specified in the Procurement Regulations, 2013 – *Government Notice No.446 and is open to all Tenderers* as defined in the Regulations unless otherwise stated in the Tender Data Sheet.

4. Interested eligible Bidders may obtain further information from and inspect the Tendering Documents at the office of the Secretary of the Tender Board at Ushetu District Council Office from **07:30 to 03:30pm** on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.

5. A complete set of Tendering Document(s) in English and additional sets may be purchased by interested Tenderers on the submission of a written application to the address given under paragraph 7 below and upon payment of a non-refundable fee of TSh. 100,000.00. Payment should either be by Cash, Banker's Draft, or Banker's Cheque, payable to District Executive Director – Ushetu District Council.

6. All Tenders must be accompanied by a Tender securing Declaration in the format provided in the Tender Documents.

7. All Tender in one original plus Three (3) Copies, properly filled in, and enclosed in plain envelopes marked Geophysical Surveying, drilling of two (2) boreholes and pumping testing for Butibu Village in Ushetu District Council and must be delivered to the address of Secretary of the Ushetu District Council Tender Board (PMU'S Office) P. O. Box 50 – Ushetu-Kahama before **28th May 2019 at 11:30 hrs.** Tenders will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend in the opening at **Ushetu District Council Head quarter's PMU's Office.**

8. Late Tenders, portion of Tenders, electronic Tenders and Tenders not received, Tender not opened at the Tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**MICHAEL MATOMORA**
**District Executive Director**

215229402

## HALMASHAURI YA WILAYA YA KAHAMA

**TANGAZO LA ZABUNI 2019/2020**
**ZABUNU Na. LGA/162/2019/2020/NC/01-10**
**KWA AJILI YA ZABUNI YA UWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO**

**Tarehe: 15/05/2019**

1. Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu inawatangazia wananchi wote,Taasisi, Mashirika na watu binafsi, inatarajia kukusanya mapato yake ya ndani kupitia vyanzo vyake vya mapato kwa ajili ya kuendesha shughuli zake mbalimbali za kimaendeleo kwa njia ya kubinafsisha vyanzo hivyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa kipindi cha Julai 2019 – Juni 2020.

2. Unakaribishwa kuleta maombi yako ukitaja kiasi ambacho unaweza kukusanya na kulipa Halmashauri ya Ushetu kwa utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa hapo juu, kwa vyanzo mbalimbali vya mapato kama ilivyoainishwa hapa chini;

**A. ZABUNI ZA WAKALA WA KUKUSANYA USHURU WA MIFUGO KATIKA MINADA.**

| S/N | JINA LA ZABUNI | KIJIJI | KATA | NAMBA YA ZABUNI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ushuru wa mifugo mnada wa Uyogo | Uyogo | Uyogo | LGA/162/2019/2020/NC/01 |
| 2 | Ushuru wa mifugo mnada wa Chona | Kasigili | Chona | LGA/162/2019/2020/NC/02 |
| 3 | Ushuru wa mifugo mnada wa Bugomba "A" | Bugomba | Ulewe | LGA/162/2019/2020/NC/03 |
| 4 | Ushuru wa mifugo mnada wa Nyamtengela | Nyamtengera | Idahina | LGA/162/2019/2020/NC/04 |
| 5 | Ushuru wa mifugo mnada wa Chambo | Chambo | Chambo | LGA/162/2019/2020/NC/05 |

**1. ZABUNI ZA WAKALA WA KUKUSANYA USHURU WA KATIKA MAGETI, IKIWA NI MAZAO MCHANGANYIKO, MAZAO YA MISITU NA MATUNDA**

| S/N | JINA LA ZABUNI | KIJIJI | KATA | NAMBA YA ZABUNI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ushuru katika geti la Kisuke | Kisuke | Kisuke | LGA/162/2019/2020/NC/06 |
| 2 | Ushuru katika geti la Igunda | Igunda | Igunda | LGA/162/2019/2020/NC/07 |
| 3 | Ushuru katika geti la Busenda | Busenda | Chona | LGA/162/2019/2020/NC/08 |
| 4 | Ushuru katika geti la Mpunze | Ifunde | Mpunze | LGA/162/2019/2020/NC/09 |
| 5 | Ushuru katika geti la Mwabomba | Mwabomba | Idahina | LGA/162/2019/2020/NC/10 |

3. Maombi yote ya zabuni yazingatie masharti yafuatayo:-

I. Nyaraka za zabuni zinapatikana kwa kulipa ada ya Tsh 50,000/= ambazo hazitarejeshwa na zinapaswa kulipwa kwenye ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa tisa na nusu alasiri kwa siku za kazi kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa. Kila uwakala utakao omba unajitegemea, kwa waombaji wa mawakala wa kukusanya ushuru, wanashauriwa kutembelea eneo la Biashara kabla ya kuchukua nyaraka ya zabuni ambayo itatolewa katika ofisi ya katibu wa Bodi ya zabuni iliyopo katika jengo la ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ushetu, iliyopo mtaa wa Nyamilangano.

II. Ombi la zabuni liwe na jina na anuani halisi ya mwombaji, aidha aonyeshe mahali ofisi zake zilipo au anapoweza kupatikana (Physical address)

III. Mwombaji awe na leseni hai ya biashara ,TIN ya TRA pamoja na dhamana ya fedha taslimu ambayo ni sawa na kiasi atakacho taja kulipwa kwa kila mwezi,ambapo atatakiwa kulipia miezi miwili kwanza kama dhamana.

IV. Mwombaji atakaye chaguliwa atalipwa asilimia kumi(10%) ya makusanyo yaliyo wasilishwa.

V. Zingatia kuwa fomu ya maombi ya zabuni inajazwa na kusaniniwa na mwenye uhalali wa kisheria (Power of attoney) katika zabuni hii.

VI. Mwombaji wa zabuni, endapo atachaguliwa atahitaji kulipa fedha za makusanyo yote kwenye akaunti ya Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu namba 30610004660, **UDC OWNSOURCE COLLECTION ACCOUNT** katika benki ya NMB- Kahama.

VII. Makusanyo yote yatakusanywa kwa kutumia mashine za kielectronic (Pos)

VIII. Mwombaji awasilishe zabuni zote ziwe na nakala halisi moja (orginal na nakala kivuli mbili zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa **NAMBA NA JINA LA ZABUNI HUSIKA,** kazi inayoombwa kwa orginal na copy na anwani iliyotajwa hapo chini bila kuwekwa alama yoyote na kufungwa kwa lakiri.

IX. Mwombaji atakayeshindwa masharti haya atakuwa amejiondoa mwenyewe kwenye mchakato mzima wa zabuni.

X. Halmashauri hailazimiki kuchagua zabuni yoyote.

XI. Zabuni zitawasilishwa kwa katibu wa bodi ya zabuni Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu kwa anuani ifuatayo:

**KATIBU WA BODI YA ZABUNI**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**
**S.L.P 50, KAHAMA**

XI. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi haya ni tarehe 28/05/2019 saa 5.30 asubuhi siku ya Jumanne. Maombi yote yatafunguliwa hadharani muda mfupi baadae, mbele ya wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguzi wa zabuni katika ukumbi wa Halmashauri iliyopo kata ya Nyamilangano barabara ya Ulowa kwa gharama zaowenyewe.

XII. Zabuni zitakazochelewa ,zabuni zitakazo letwa sehemu ya zabuni tu, zabuni za kieletroniki, na zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufungaji wa zabuni, kwa hali yoyote ile zabuni hizo hazitakubaliwa kwa tathimini.

**MICHAEL MATOMORA**
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**
**USHETU**

215229402

# Kabudi, Gavana wakaliwa kooni

INATOKA UK 2

kali kwa kutumia vyombo vyake kufanya uchunguzi wa kampuni hiyo.

"Haiingii akilini kwamba vyombo vyote walishindwa kujua uwezo wa kampuni husika. Ni kwa bahati mbaya haya yanatokea na mawaziri waliohusika wako ofisini utadhani hakuna kilichotokea

"Pamoja na udhaifu huo, matamko na maelekezo ya serikali kuhusu biashara ya zao la korosho yamesababisha hasara kubwa kwa wakulima na taifa kwa sababu ambazo zingeweza kuepukwa.

"Kutokana na sakata hili la korosho, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inawataka wahusika wote wajitafakari kama wanatosha kuendelea kushika nyadhifa walizo nazo ama wanapaswa kupisha ofisi hizo za umma kuongozwa na watu wengine kwa kuwa uamuzi wa CCM umelisababishia taifa hasara ya Sh. trilioni 1.18.

"Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni pia inataka kufahamu ni gharama kiasi gani ambazo serikali ilitumia kukusanya zao hili la kibiashara kutoka kwa wakulima na kuzipeleka kwenye maghala ya serikali?

"Baada ya gharama zote zilizotumiwa na serikali, je, serikali ilitegemea kuuza korosho kwa bei gani? Mwambe alihoji.

Waziri Kivuli huyo pia alisema kambi yao inaishauri serikali kuboresha kwanza sekta ya kilimo na kujielekeza katika viwanda ambavyo vitaongeza thamani katika mazao ya mifugo kama vile maziwa, nyama, ngozi, damu, kwato, pembe na kusindika mazao yatokanayo na uvuvi.

Mwambe pia aliitaka serikali kuongeza bajeti ya wizara hiyo huku akiitaka ilieleze Bunge kiwango ambacho viwanda vyote vilivyopo nchini vinachangia kwenye Pato la Taifa.

Mwambe pia alisema bado wafanyabiashara wanakumbana na kadhia utitiri wa kodi na manyanyaso kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA).

Alisema kwa kipindi kirefu, TRA imeshindwa kubuni mkakati wa makusanyo ya kodi na badala yake wanatumia vibaya mamlaka katika kutekeleza majukumu na kusababisha malalamiko ya kuwapo vitendo vya rushwa.



Wafanyausafi wakiondoa mchanga kwenye mitaro ya maji ya mvua kando ya Barabara ya Uhuru, eneo la Ilala Bungoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Shahidi adai Mbowe alishawishi maandamano

INATOKA UK 4

zia watawawanyike lakini waliendelea kuandamana

kulisogelea gari la askari na kuanza kuwarushia chupa za maji na mawe.

Akifafanua zaidi, alidai kuwa alipoangalia, alimwona Mbowe akiwahamasisha wananchi kuendelea kuandamana kuwasogelea askari huku wakiwa na viongozi wengine.

"Baada ya waandamanaji kukaidi amri ya polisi tusikia askari wakipiga mabomu ya mochozi na kila mtu alitawanyika kukimbilia njia yake," alidai Abdallah.

Kesi hiyo inaendelea kusikilizwa kesho ushahidi wa Jamhuri.

Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine ni katibu Mkuu wa Chadema Djk. Vincent Mashinji; Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa; Naibu Katibu Mkuu Zanzibar; Salum Mwalimu; Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na John Heche wa Tarime Vijijini.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka jana, wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam, kwa pamoja walikula njama ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi.

Ilidaiwa kuwa Februari 16, Bulaya alishawishi kutenda kosa la jinai katika viwanja vya Buibui vilivyopo Kinondoni, jijini Dar es Salaam alishawishi wakazi wa eneo hilo kutenda kosa la jinai kwa kufanya maandamano yenye vurugu.

Ilidaiwa Februari 16, barabara ya Kawawa eneo la Kinondoni Mkwajuni, kwa pamoja washtakiwa walifanya mkusanyiko na kukaidi amri halali ya ofisa wa jeshi la polisi Gerald Ngiichi na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi kujeruhiwa.

Ilidaiwa siku ya tukio la kwanza na la pili, katika viwanja vya Buibui vilivyoko Kinondoni jijini Dar es Salaam, kwenye mkutano wa hadhara mshitakiwa Heche alitoa lugha ya kuchochea chuki alitamka matamshi kwamba "Kesho patachimbika upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii...wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano...watu wanapotea...watu wanauawa wanaokotwa kwenye mitaro lazima ukome... "alinukuliwa na kudaiwa kuwa maneno yaliyoelekea kuleta chuki kati ya serikali na Watanzania.

## Bunge lataka ushuru 15% uagizaji sukari ufutwe

INATOKA UK 5

"Sekta ya sukari pia imegubikwa na malalamiko juu ya viwango vya sukari inayoingia nchini ukilinganisha na mahitaji halisi ya nchi. Kamati inaishauri kuweka umakini wakati wa kutoa vibali vya kuingiza bidhaa hiyo nchini na kwamba vibali hivyo vitolewe baada ya serikali kufanya tathmini na kubaini upungufu wa sukari uliopo," alisema.

Kamati hiyo pia ilisema Tanzania imeendelea kushuka katika orodha ya nchi zenye mazingira mazuri ya kufanyia biashara, ikieleza kuwa kumechangiwa na changamoto zinazolalamikiwa na wafanyabiashara.

Kanali Masoud pia alisema mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni tani 700,000 na uzalishaji wa bidhaa hiyo nchini ni tani 210,000.

Alisema takwimu hizo zinadhihirisha kuwa ili kukidhi mahitaji ya soko, ni lazima tofauti iliyopo ishughulikiwe kwa kuruhusu kuingizwa kwa bidhaa hiyo kutoka nje ya nchi.

"Changamoto ni kwamba viwanda vya mafuta ya kula vinavyoingiza mafuta kutoka nje ya nchi, vimekumbana na changamoto ya mgongano wa uamuzi baina ya mamlaka za udhibiti juu ya vipimo vinavyobainisha aina ya mafuta yaliyoingizwa, jambo ambalo linapelekea ucheleweshaji wa kutoa mafuta hayo bandarini na kuongeza gharama za uhifadhi," alisema.

Kiongozi huyo wa kamati aliishauri serikali kuzisimamia kwa ukaribu mamlaka hizo kuhakikisha watekeleza majukumu kwa maslahi mapana ya nchini.

Akichangia mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara hiyo jana, Mbunge wa Nzega Mjini, Hussein Bashe (CCM), alisema bado kuna ukiritimba katika utoaji vibali kwa wawekezaji wanaoanzisha viwanda nchini.

Alisema ili kuondokana na vikwazo hivyo katika utoaji vibali kutoka taasisi mbalimbali za serikali, ni muhimu kwa serikali kuweka mfumo wa pamoja kwa taasisi hizo kukusanya tozo na kutoa vibali.

Mbunge wa Monduli, Julius Kalanga (CCM), alisema hakuna ushirikiano kwenye wizara za serikali katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Alisema wananchi wa Monduli walitoa ardhi kwenye mradi wa magadi ulipo Engaruka, lakini hakuna hata kilometa moja ya barabara kutoka Mto wa Mbu kwenda kwenye eneo la mradi iliyojengwa.

"Hivi kuna mwekezaji gani anayeweza kwenda kuchukua magadi wakati hakuna hata kilometa moja ya barabara iliyojengwa kuelekea kwenye mradi? Ni bora wananchi wetu waambiwe waendelee kuyatumia maeneo yao ambayo wameyatoa kwa bei rahisi," alisema.

Mbunge huyo pia aliishauri serikali kuruhusu ngozi kuuzwa nje ya nchi hadi pale viwanda vya ndani vitakapokuwa na uwezo wa kununua ngozi kama hatua ya kuwasaidia wafugaji.

Naye Mbunge wa Gairo, Ahmed Shabiby (CCM), aliitaka serikali kuchukua hatua kutokana na kufungwa kwa biashara na kuhakikisha kiwanda cha matairi cha General Tyre, jijini Arusha kinafufuliwa.

HABARI KITAIFA

# Wawekezaji wa madini wahakikishiwa usalama

**Na Boniface Gideon, MKINGA**

KAMANDA wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, ametoa onyo kali kwa watu watakaojaribu kutishia amani ya mkoa huo, akisema kwamba hawatasalimika bali watakamatwa na kushughulikiwa.

Bukombe aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa halfa ya ufunguzi wa soko la madini ya vito wilayani Mkinga uliofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella, uliohudhuriwa na wadau wa madini

Alisema sehemu kunapokuwa utulivu na amani, wapo watu ambao wanataka kujaribu kuiondoa, hivyo aliwatahadharisha kwamba hawatafanikiwa badala yake wataishia kwenye vyombo vya dola.

"Kwa wale ambao watajaribu kutishia usalama wa Mkoa wa Tanga niwaambie kwamba tutawashughulikia kweli kweli, na hakuna atakayesalimika," alisema Bukombe.

Aliwaambia wadau wa madini kwamba mkoa huo upo salama na wamejipanga kuhakikisha unakuwa kivutio cha wawekezaji, na kwamba mazingira ya usalama wataendelea kuyasimamia kwa kuwa huwezi ukawekeza maeneo yasiyokuwa usalama.

Kwa mujibu wa Bukombe, watafanya hivyo kwa sababu huwezi kuwekeza mahali pasipokuwa na usalama, hivyo wamejipanga kuhakikisha Amani iliyopo inaendelea kuwapo ili kuwavutia wawekezaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga, Rashid Gembe, alisema uwapo wa fursa ya soko la madini utawanufaisha wachimbaji wadogo wasiokuwa na soko la uhakika kwa kuwa watapata mahali pa kuuzia.

Alisema kwa sababu awali walikuwa wanategemea watu wa kati (brokers), hivyo uwapo wa soko hilo utasaidia kuwafanya wanunuzi kutoka nje ya nchi kwenda kununua madini hapo. Kadhalika, Mkurugenzi huyo alisema uwapo wa soko hilo utawasaidia kuiongezea mapato halmashauri kwa kuwa awali walikuwa wakiuziana kinyemela.



Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Walemavu), Stella Ikupa (kulia), akikabidhi sehemu ya mifuko ya saruji kwa wanachama wa Jumuiya ya Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kituo cha kulelea watoto, jijini Dodoma jana. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Wanaume wa vijijini waonywa michepuko

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WANAUME wa vijiji vilivyopo Kata ya Usanda, Shinyanga Vijijini, wameonywa tabia ya kuendekeza masuala ya kuwa na mahawala nje ya ndoa maarufu kama ichepuko, hasa wanapovuna mazao yao na kuyauza.

Kwamba hali hiyo ni hatari kwa kuwa inaweza kusababisha magonjwa ukiwamo Ukimwi.

Imedaiwa kuwa asilimia kubwa ya wanaume wa vijiji wanapouza mazao yao, wamekuwa na tabia ya kuendekeza ngono ikiwamo kuwa na wake nje ya ndoa, vitendo ambavyo ni hatari kwa afya zao.

Onyo hili lilitolewa juzi na Kaimu Mtendaji wa Kata ya Usanda Shinyanga Vijijini, Ester Pembelada, kwenye mkutano wa hadhara kwenye kijiji cha Buchamike, ulioandaliwa na Shirika la Agape la mjini hapa, kwa lengo la kutoa elimu ya afya ya uzazi na jinsia ikiwamo kuacha ngono zembe.

Aliwataka wanaume hao kuachana na michepuko badala yake wabaki na wake zao ili wawe salama, na kuacha vitendo vya kupapatikia wanawake wa nje hasa pale wanapokuwa na fedha za mavuno ya mazao.

"Mbali na kuendekeza masuala ya michepuko, pia nawaomba muache tabia ya kutongoza wanafunzi na kuwaozesha ndoa za utotoni, bali muwaache kwanza wamalize masomo yao," alisema.

Mmoja wa wanaume waliohudhulia mkutano huo, Jumanne Dotto, alilipongeza Shirika la Agape kwa kuwapatia elimu ya afya ya uzazi na jinsia, kwa kuwa wanaishi pembezoni mwa miji, kwa kuwa hawapati elimu hiyo tofauti na wa mjini, na kuahidi kuitekeleza kwa vitendo.

Mratibu wa mradi wa afya ya uzazi na jinsia kutoka Shirika hilo, Lucy Maganga, alisema wametoa elimu hiyo ili wanaume waache ngono zembe pamoja na kumaliza tatizo la mimba na ndoa za utotoni.

# Ujenzi holela kikwazo kwa Jeshi Zimamoto

**Na Lilian Lugakingira, BUKOBA**

TATIZO la ujenzi holela wa nyumba za makazi katika Mkoa wa Kagera, limetajwa kusababisha kukwamisha jitihada za kikosi cha zimamoto na uokoaji, kwenda kuzima moto pindi unaopotokea katika baadhi ya maeneo, hali inayohatarisha maisha na mali za wananchi.

Akitoa elimu kwa wakazi wa mkoa huo kuhusu namna ya kukabiliana na majanga ya moto, mkaguzi msaidizi Jeshi la cha Zimamoto na Uokoaji, Thomas Majuto, alisema wamekuwa wakitoa ushauri kwa halmashauri zote ili ziweke mipango itakayowezesha maeneo kupangwa kabla watu hawajajenga, ili kupunguza athari zinazotokana na majanga ya moto.

"Tunachokifanya tu ni kushauri halmashauri husika ili zipange miji kwanza ndipo wananchi waende kujenga, tukifikia hatua hiyo wananchi watakuwa salama kabisa kuliko mfumo wa sasa wa mtu akipata hela ananunua kiwanja na kujenga, anapanga ataongea na jirani waanchi njia ya kupita bodaboda au gari ndogo, wakati magari yote ya zimamoto ni makubwa," alisema.

Askari wa Jeshi hilo, Sajenti Ramadhan Karata, ametoa elimu kwa vitendo namna ya kutumia mitungi ya kuzimia moto, huku akiwataka wananchi kuzingatia maelekezo wanayopewa ili kukabiliana na majanga ya moto.

"Mitungi hii mnayotakiwa kuwa nayo katika majumba yenu inatumika moto unapoanza kabla haujawa mkubwa, moto ukiwa mkubwa haiwezi kutumika tena, mnachopaswa kufanya pindi unapotokea moto, mnapaswa kutoa taarifa haraka kwetu ili tuweze kufika haraka na kuokoa maisha ya watu na mali zenu," alisema Karata.

Mmoja wa wananchi walioshiriki mafunzo hayo, Fadhili Christopher, aliwasihi wananchi wenzao kufuata taratibu za ujenzi ili kuliwezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuwafikia kwa urahisi kabla moto haujaleta madhara makubwa zaidi, ikiwamo uharibifu wa mali na vifo.

Naye Mugisha Kasaju, mkazi wa Manispaa ya Bukoba, aliliomba Jeshi hilo kuendelea kutoa elimu kupitia njia mbalimbali ikiwamo vyombo vya habari na mikutano ya serikali za mitaa na vijiji, ili elimu hiyo iweze kuwafikia wananchi wengi.

# Mbunge ahoji ukosefu wa vipimo

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

MBUNGE wa Viti Maalum (Chadema), Devotha Minja, ameitaka serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro ambayo inahudumia wagonjwa 500 kwa siku inakuwa na vipimo vyote muhimu kikiwamo cha 'full blood picture'.

Akiuliza swali la nyongeza jana bungeni, Minja alisema hospitali hiyo licha ya kuwa na wagonjwa wengi, kwa takriban miezi minne sasa haina kipimo hicho na mashine ya oksijeni.

"Naomba kujua serikali ina mpango gani wa haraka wa kusaidia hospitali hiyo iweze kutoa huduma kwa wagonjwa?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, alisema hana taarifa juu ya hayo anayozungumza mbunge huyo na kuahidi kufuatilia ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma.

"Sina taarifa ya hili analolisema sasa hivi. Nimwombe mbunge baada ya kikao hiki tufuatilie ili kuhakikisha hiyo huduma ambayo ni ya msingi kwa wagonjwa ipatikane katika hospitali hii," alisema.

Aidha, katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ester Mahawe, alitaka kujua ni lini serikali itapeleka watumishi katika kituo cha afya cha Dongobesh.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Josephat Kandege, alisema katika mwaka wa fedha 2019/20, Tamisemi imepeleka maombi ya kuajiri watumishi 15,000 wa kada ya afya na kibali kitakapopatikana, kituo hicho kitaachwa.

Katika swali la msingi la Mahawe, alihoji ni lini serikali itapandisha hadhi kituo cha afya Dongobesh ili kuhudumia wananchi wa Mbulu Vijijini na kupunguza msongamano katika Hospitali ya Rufani ya Haydom.

"Je, ni lini serikali itaongeza watumishi wa Afya, dawa na vifaa tiba katika kituo hicho cha afya?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kandege alisema kwa kuwa hospitali ya wilaya inajengwa katika eneo la Dongobesh, hakuna sababu ya kituo hicho kupandishwa hadhi kuwa hospitali.

Hata hivyo, alisema serikali imeendelea kuongeza idadi ya watumishi katika kituo hicho na mwaka 2017/18 watumishi sita waliajiriwa na kufanya jumla ya watumishi kuwa 37.

Pia alisema serikali inatuma Sh. Million 320 Bohari Kuu ya Dawa (MSD) kwa ajili ya kununua vifaa tiba na hadi sasa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 73 vimepokelewa kituoni hapo.



Mbunge Viti Maalumu Mkoa wa Mara, Agness Marwa (kulia,), akishiriki kuwapikia ugali wageni wake, waliotembelea Bunge na shamba la Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, eneo la Zuzu, jijini Dodoma jana, wakiwa katika ziara ya mafunzo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri: Hakuna kesi madhara ya raia

BUNGE limeelezwa kuwa katika kipindi cha mwaka 2010-2015, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora haijafungua kesi yoyote mahakamani kuhusu madhara yanayofanywa na vyombo vya dola dhidi ya raia.

Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Augustine Mahiga, alisema hayo jana bungeni jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (Chadema), Dk. Immaculate Semesi.

Mbunge huyo alisema kwa mujibu wa Ibara ya 13(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.

"Kumekuwa na kiwango cha juu cha matukio na kesi zinazohusu kuvunjwa kwa haki za kiraia kwa kufanywa na vyombo vya dola. Kwa kipindi hicho kesi ngapi zimefunguliwa na kuchukua muda gani kutolewa hukumu?

"Je, kesi hizo zimekuwa zikigharamiwa kwa kiasi gani kutoka mfuko wa fedha za umma tangu mwaka 2010-2015 na je, serikali inafanya jitihada gani kuhakikisha wananchi wake pamoja na vyombo vya usalama wanapata elimu ya uraia?"Alihoji.

Mbunge huyo alihoji pia kama serikali haioni ni wakati mwafaka kuja na mikakati thabiti wa kufanya tathmini kuhusu masuala yanayohusu haki za binadamu.

Akijibu maswali hayo, Dk. Mahiga alisema tume imekuwa inapokea malalamiko ya uvunjwaji wa haki za binadamu dhidi ya vyombo vya dola na kuyashughulikia kwa kufanya uchunguzi wa kawaida, usikilizwaji hadharani na kufanya usuluhishi na upatanishi.

"Mbinu hizi zimeonesha mafanikio makubwa katika kuwapatia wananchi haki zao, hivyo kutokuwa na umuhimu wa kufungua mashauri mahakamani. Ikumbukwe kuwa ufunguaji wa mashauri mahakamani ni hatua ya mwisho iwapo njia zingine zote zimeshindikana," alisema.

"Kama ambavyo nimesema hakuna kesi yeyote iliyofunguliwa kwa kipindi hicho, hivyo basi hakuna gharama zozote za ufunguaji wa mashauri mahakamani zilizotumika," aliongeza. Waziri huyo alibainisha kuwa kwa kipindi hicho, tume imefanya jitihada mbalimbali ili kuhakikisha wananchi pamoja na vyombo vya usalama wanapata elimu ya uraia.

"Jitihada hizo ni pamoja na kuelimisha umma kupitia vyombo mbalimbali vya habari, mikutano, maadhimisho, machapisho na warsha mbalimbali,"alisema.

Alieleza kwa kipindi hicho vipeperushi 48,638, nakala 18,300 za Mpango Kazi wa Taifa wa Haki za Binadamu na vipindi vya redio na runinga 115. Alilihakikishia bunge kuwa wataendelea kubuni mbinu na mikakati mbalimbali itakayowezesha kuendelea kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Kadhalika, alisema wanatarajia kuanzisha somo la haki za binadamu ambalo litawekwa kwenye mitaala yote katika shule mbalimbali nchini.

# Azam sasa kuonyesha chaneli za ndani bure

WIZARA ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imesema kituo cha televisheni cha Azam kimepokea leseni ya kuonyesha chaneli za ndani bure na ndani ya miezi saba watajenga mfumo wa kurusha chaneli hizo.

Naibu Waziri wa wizara hiyo, Atashasta Nditiye, alisema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Mlalo (CCM), Rashid Shangazi.

Shangazi katika swali lake, alihoji serikali ina mkakati gani kuruhusu kuonekana kwenye visumbuzi mbalimbali chaneli hiyo.

Akijibu swali hilo, Mhandisi Nditiye alisema kati ya watu waliopeleka maombi kutaka waruhusiwe kuonyesha chaneli zao kwenye visumbuzi ni Azam TV.

"Jana (juzi) kituo hiki kimepokea leseni ya kuonyesha chaneli za ndani bure na wametuhakikishia ndani ya miezi saba watajenga mfumo wa kurusha chaneli hizo," alisema Nditiye.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Nyamagana (CCM), Stanslaus Mabula, alisema serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imefungia chaneli za ndani kutoonekana kwenye baadhi ya ving'amuzi nchini zikiwamo Azam TV na DSTV.

"Je, serikali haioni kwa kufanya hivyo imewanyima wananchi fursa ya kujua mambo yanayoendelea kwenye taifa lao na je, ni lini itatoa mwafaka wa jambo hili?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Nditiye alisema serikali inatambua umuhimu wa wananchi kupata fursa ya kujua mambo yanayoendelea kwenye taifa. Alisema kwa misingi hiyo imetoa leseni zenye masharti tofauti ikiwamo ya utangazaji wa umma na matangazo huruhusiwa kurushwa na watoa huduma wote.

"Kwa hivi sasa matangazo ya umma ni TBC1 na TBC3 maarufu kama Safari Channel. Kampuni zinazomiliki visimbuzi vya DSTV, Zuku na Azam hayakustahili kutoa huduma ya kubeba chaneli za ndani zisizolipwa kutokana na masharti ya leseni zao," alisema.

Alibainisha kuwa utoaji wa huduma za maudhui kupitia visumbuzi vyao uko kwenye mfumo wa kukidhi soko la kimataifa na maudhui yake kuwa ya kulipia.

Nditiye alifafanua kuwa masharti ya leseni hizo na mfumo wa kutofautiana na masharti ya leseni za watoa huduma za maudhui ya ndani ya nchi.

Pia alisema kuruhusu chaneli za ndani kuonyeshwa kwa kutumia leseni za matangazo ya kimataifa kutazifanya kuwa za kulipia badala ya kuonekana bure.

Aliongeza kuwa serikali kupitia TCRA imefanya jitihada ikiwa ni pamoja na kukaribisha maombi ya leseni ya kubeba maudhui ya chaneli za ndani kutoka kwa wanaohitaji kutoa huduma zikiwamo kampuni za Azam, DSTV na Zuku ili kupata leseni stahiki na kuweza kutoa huduma za kubeba/kuonesha maudhui ya ndani kupitia visumbuzi vyao. Naibu Waziri huyo alisisitiza kuwa kwa sasa TCRA inashughulikia maombi yaliyopokewa ili kushauri kuhusu utoaji wa leseni stahiki.

## Mbulu walia na vitambulisho vya wajasiriamali

**Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA**

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu Mkoani Manyara, Joseph Mandoo, amesema wamepoteza vyanzo vya mapato kwa kuwapo kwa vitambulisho vya wajasiriamali kwenye eneo hilo na kusababisha upungufu wa mapato ya halmashauri hiyo.

Mandoo aliyasema hayo jana kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo cha robo mwaka kilichofanyika mjini Mbulu.

Alisema uwapo wa vitambulisho hivyo vya ujasiriamali umesababisha changamoto ya kupoteza vyanzo vyao vya mapato hasa kwenye minada na magulio mbalimbali vijijini.

Alisema hivi sasa hawana uwezo wa kukusanya mapato waliyokuwa wanakusanya kwa wajasiriamali hao zaidi ya kufanikisha vyanzo walivyobaki navyo katika halmashauri hiyo.

"Hata hivyo tunatakiwa kujipanga upya ili kuhakikisha tunakusanya mapato ya ndani tuliyonayo kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kutoa asilimia 10 kwenye mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu," alisema Mandoo.

Alisema vyanzo vya mapato vilivyopo chini ya halmashauri hiyo vinapaswa kusimamiwa kikamilifu ili makusanyo hayo yapelekwe kwenye miradi mbalimbali iliyopo katika kata na vijiji.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Hudson Kamoga, alisema hivi sasa wamejipanga kuhakikisha wanaendelea kukusanya vyanzo vya mapato vilivyopo ili malengo ya makusanyo yafikie.

Kamoga alisema kwa kushirikiana na madiwani pamoja na watumishi wa halmashauri hiyo watafikia lengo la kukusanya asilimia 80 ya makusanyo ya ndani kama walivyodhamiria.

"Ushirikiano mkubwa tulionao hivi sasa tuuendeleze ili kuhakikisha tunakusanya mapato ya halmashauri yetu ipasavyo na kwa moyo mmoja na nguvu moja kama tunavyoshirikiana kwenye mambo mengine," alisema.

Diwani wa Viti Maalum wa Tarafa ya Dongobesh, Emiliana Shishi (Chadema), alisema wanapaswa kubuni vyanzo vipya baada ya vingine kuchukuliwa kwenye vitambulisho vya wajasiriamali.

Shishi alisema baada ya vyanzo hivyo kuchukuliwa hawatakiwi kukata tamaa zaidi ya kusonga mbele ili kuhakikisha hawateteteki kwenye ukusanyaji wa mapato.

**"Hata hivyo tunatakiwa kujipanga upya ili kuhakikisha tunakusanya mapato ya ndani tuliyonayo kwa ajili ya miradi ya maendeleo na kutoa asilimia 10 kwenye mikopo ya wanawake, vijana na wenye ulemavu," alisema Mandoo.**

# Watalii wafurahia wanyama Ngorongoro

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WATALII zaidi ya 200 kati ya 336 kutoka nchini China jana wametembelea Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro na kufurahia wanyama mbalimbali waliowaona kwenye shimo kubwa lililopo hifadhi hiyo maarufu kwa jina la Kreta.

Watalii hao waliwasili hifadhini hapo saa 5 :00 asubuhi wakitokea Arusha Mjini walikokuwa wamelala, kwa magari maalumu ya kitalii waliyoandaliwa nchini na kupokelewa kwa ngoma za asili za kabila la Kimasai na Watatoga.

Baada ya kuingia lango kuu la hifadhi walionekana wakiwa na furaha, huku baadhi yao wakionekana wakipiga picha msitu mnene waliouona na wanyama.

Aidha, walilazimika kushuka baadhi ya maeneo na kupiga picha kwenye miti mikubwa na magogo ya miti iliyolala.

Baadhi ya watalii hao walihudhuria kongamano la uwekezaji lililofanyika ukumbi wa kimataifa wa mikutano AICC uliopo Mjini Arusha, huku wenzao wakitangulia Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro.

Awali Mwenyekiti wa Kampuni ya Touchroard International Holdings Groups ya China, He Lei Hiu, alisema wamefurahishwa na ukarimu wa Watanzania na mapokezi makubwa waliopatiwa. Alisema katika ziara hiyo, jana wameanza kwa kutembelea vivutio vya utalii vya Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro na kujionea wanyama wa kila aina waliowavutia.

Alisema leo watatembelea hifadhi ya Serengeti na baadaye wataenda Zanzibar kujionea vivutio vya asili vilivyopo Tanzania.

Kwa upande wake Meneja Mkuu wa Hoteli ya Serena iliyopo Ngorongoro ambayo ilihudumia chakula cha mchana kwa wageni hao, Nickson Kanika, alipongeza serikali kufanilisha kuleta kundi kubwa la watalii toka China.

"Hatujawahi kupokea kundi kubwa la watalii toka China, lakini kwa jitihada za serikali kupitia wizara husika TANAPA na Bodi ya Utalii (TTB) wamefanikisha zoezi hili muhimu la kihistoria," alisema.

Alisema anaamini kwa ujio huo kila Mtanzania atanufaika kwa namna moja au nyingine kupitia fedha watakazoziacha kwa kununua vitu mbalimbali na kuangalia vivutio hivyo.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Augostino Senga, akielezea namna majambazi wawili walivyoshambuliwa kwa risasi na polisi ambapo mmoja alikufa na mwingine kujeruhiwa katika wilaya ya Kiteto juzi. Kulia ni Mkuu wa Upelelezi na Makosa ya Jinai wa mkoa huo, Joshua Mwafulambo. **PICHA: GIFT THADEY**

# Vijana 28,000 wanolewa ujasiriamali

**Na Allan Isack, ARUSHA**

TAASISI isiyokuwa ya kiserikali ya Arusha Municipal Community (AMCF), kwa kushirikiana na Shirika la Foundation for Civil Society (FCS), kupitia mradi wa majukwaa ya vijana, wametoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana 28,000, wa kata tatu za Halmashauri ya Jiji la Arusha kwa lengo la kuwakomboa na wimbi la umasikini.

Akizungumza wakati wa mashindano ya maonyesho ya bidhaa kutoka kwa vijana hao, Ofisa Tawala Msaidizi wa Shirika la AMCF, Anna Mushi, alisema mafunzo hayo, walitoa kupitia majukwaa ya vijana wa Kata za Lemara, Unga limited na Sokoni One, lengo likiwa kuwasaidia vijana kiuchumi kwa kuwafundisha njia za uhakika za kuzalisha bidhaa bora ili waweze kujiajiri.

Alisema, kupitia mradi huo, wamekuwa wakiwakusanya vijana kwa pamoja katika kata hizo, kwa ajili ya kutoa mafunzo ya uongozi, utawala bora, mafunzo ya kushiriki katika shughuli za kiserikali kwa ajili ya maendeleo, kutambua fursa zilizopo kwenye jamii na kushiriki katika ngazi za kutoa maamuzi.

Aliongeza kuwa kupitia mradi huo, wamefanikiwa kutoa elimu kwa vijana ya ujasiriamali na masoko, biashara na ubunifu ili waweze kukuza na kuongeza vipato vyao vya kiuchumi.

"Tunawahamasisha vijana nchini kuwa wajasiriamali wasitegemee kuajiriwa wa waliopo vyuoni, tuanze kufikiria hili ili serikali inapofanya kampeni ya kuwa na nchi ya viwanda tunawashauri kujiunga katika makundi mbalimbali kwa ajili ya kuanzisha viwanda vidogo ambavyo vitaifanya nchi uchumi wake kukua kwa kasi," alisema Anna.

Ofisa Idara ya Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Jiji la Arusha, Hanifa Ramadhani, alisema katika bajeti ya mwaka 2018/19, halmashauri hiyo, ilitoa mikopo ya Sh. milioni 665 kwa vikundi 118, kutoka kata 25 za Jiji la Arusha.

Alisema maelekezo ya serikali mwaka wa bajeti kila halmashauri inatakiwa kutenga asilimia 10 ya mapato kwa vikundi vya vijana, wanawake na wenye ulemavu.

"Muongozo wa serikali katika asilimia hizo 10 ya mapato tuliyokusanya. tunatoa asilimia nne kwa vijana, nne zingine kwa wanawake na asilimia mbili kwa wenye ulemavu," alisema Hanifa.

Wakizungumza kwa niaba ya vijana wengine walioshiriki katika maonyesho hayo, Ibrahimu Kikoti na Sara Mosess, walisema kuwa kupitia mafunzo hayo, wameongeza maarifa ya kuwa wabunifu wa kuchangamkia fursa kwa kuzalisha bidhaa bora na kutafuta masoko ya uhakika.

Walisema kilichowafanya kuingia katika ujasiriamali ni kutokana na faida nyingi ikiwamo kuwa na uhuru wa kufanya kazi ambayo utaweza kuirithisha kizazi.

"Kilichonifanya mimi kuingia katika ujasiriamali ni mafanikio na maendeleo yanakuja pindi watu wanapochukua jukumu la kujiajiri inawasaidia kukuza kipato kwa kuwa kazi anayoifanya ni yake hivyo ataweza kuimudu kwa njia yoyote," aliongeza Sara.

Alisema vijana wengi wamekuwa wakilalamika kuwa ajira zimekuwa chache na hazipatikani kwa urahisi, suala hilo linatokana na wengi kutokujishughulisha na kazi na kuwa na ubunifu mdogo na kushindwa kutumia fursa.





## NMB sasa yachangamkia ujio watalii

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

WAKATI watalii 343 kutoka nchini China, wakiendelea na ziara yao ya siku tano katika baadhi ya Hifadhi za Taifa nchini pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Benki ya NMB imejitwisha jukumu la kupeleka huduma za kubadili fedha za kigeni katika kila eneo wanakapofika watalii hao.

Taarifa iliyopatikana jana na kuthibitishwa na Meneja wa NMB anayeshughulikia Dawati la China, Agness Mulolele ilieleza kuwa lengo la kusogeza huduma hiyo kwa Wachina hao ni kuunga mkono jitihada za serikali katika kuendelea na kukuza utalii nchini.

"Ni kweli tumeamua kusogeza huduma karibu ili kuweza kuwahudumia watalii wote katika huduma zote za kifedha. Huduma hiyo ya kubadili fedha za kigeni itawahusu zaidi wafanyabiashara na watu maarufu, wawekezaji kutoka kampuni 27, waandishi wa habari 40, maofisa wa serikali ya China na mawakala wa kampuni za utalii waliokuja kutembelea vivutio mbalimbali vya utali," alisema Mulolele

Alisema wameamua kwenda kutoa huduma zao kama sehemu ya kusaidia nchi kufikia malengo makubwa ya maendeleo ikiwemo kuweka mazingira bora kwa watalii wanapotembelea nchini ili waweze kupata huduma bora za kibenki ikiwemo kubadirisha fedha za kigeni.

Juzi, Waziri Mkuu, Kassim Mjaliwa, akizungumza na watalii hao baada ya kuwapokea katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), alisema Tanzania na China ni nchi zenye historia ndefu na ni marafiki wa siku nyingi.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Hamis Kigwangalla, akimkaribisha Waziri Mkuu kuzungumza na watalii hao, alisema bado Tanzania itazidi kufanya mambo makubwa hasa katika sekta ya utalii.

Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii nchini (TTB), Jaji mstaafu Thomas Mihayo, alisema, "Labda niseme kuwa sasa serikali imeanza kutuelewa sisi watu wa sekta ya utalii maana mbali na wageni hawa ambao ni zaidi ya 300, bado muda si mrefu tutapokea watalii tena 1000 lakini pia mwishoni mwa mwaka huu tutakwenda Russia kwa masuala ya utalii. Kwa hiyo naomba nitoe wito pia Watanzania kuwa ni muda sasa wa kujifunza lugha tofauti tofauti ili iwe fursa nzuri ya kujipatia ajira."

Aidha, alisema dhamira ya Bodi hiyo ya Utalii nchini ni kutangaza utalii katika soko la China na kwamba Juni mwaka huu, wanatarajia kufanya ziara ya kutangaza utalii katika miji ya Nanjing, Hanzhou na Changsha,"

**"Ni kweli tumeamua kusogeza huduma karibu ili kuweza kuwahudumia watalii wote katika huduma zote za kifedha. Huduma hiyo ya kubadili fedha za kigeni itawahusu zaidi wafanyabiashara na watu maarufu, wawekezaji kutoka...**

# Mghwira azipa somo taasisi za ubora bidhaa kupunguza urasimu

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MKUU wa mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, ameagiza mamlaka nne za serikali zinazosimamia ubora wa bidhaa za chakula na vifaa, kuanzisha haraka Kituo cha Pamoja (One Stop Centre) cha kuhudumia kada hiyo ili kumaliza urasimu unaolalamikiwa.

Mghwira alikuwa akizungumza mjini hapa na wadau mbalimbali, wakati akifungua kikao cha mawakala wa uingizaji wa bidhaa kupitia mipaka ya Holili, Tarakea na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

"Tunahitaji iundwe mara moja One Stop Centre (kituo cha pamoja), wekeni Ofisi ya TBS, Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Mamlaka ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Acheni urasimu na rahisisheni upatikanaji wa huduma zenu," alisema.

Mghwira akieleza kuwa urasimu unaofanywa na baadhi ya watendaji wa serikali, unakwamisha ukuaji wa maendeleo ya sekta ya biashara na uwekezaji.

Aidha, Shirika la Viwango nchini (TBS), limetakiwa kujitathmini na kuboresha huduma zake ikiwamo kuwachukulia hatua wafanyakazi wachache wanaoharibu taswira ya shirika.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya viongozi na watendaji kukwamisha taratibu au vibali, jambo ambalo linaathiri ustawi wa biashara na ukuaji wa kisekta hasa biashara.

Alitaka TBS kukutana na mamlaka nyingine za serikali ili kujiridhisha kama mahitaji ya huduma baina ya mamlaka moja na nyingine hazifanani ili kupunguza usumbufu kwa wateja wao.

Pia Mghwira aliwataka wafanyabiashara kufuata taratibu za kuingiza bidhaa na kuacha kushawishi kukwepa kutimiza matakwa ya kisheria ya uingizaji wa bidhaa kwa kutoa rushwa kwa watendaji wanaosimamia. Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TBS, Jabir Jabir, alisema kikao hicho kina lenga kutoa elimu kwa wafanyabiashara kufuata taratibu ili kuepuka hasara inayotokana na kwenda kinyume cha sheria za nchi.



Watoto wa jamii ya wafugaji kutoka mikoa ya Shinyanga na Tabora, wakichunga ng'ombe katika eneo la Zinga, wilayani Kilwa, Mkoa wa Lindi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Wamiliki mabasi, madereva waingia mgogoro mpya

**Na Mwandishi Wetu, SIHA**

MGOGORO mpya unafukuta kati ya madereva na wamiliki wa mabasi madogo katika kituo cha mabasi cha Sanya Juu katika Wilaya ya Siha, baada ya kikundi cha watu wachache kudaiwa kukusanya kila siku Sh.1, 000 kwa kila basi dogo, wakidai zinakwenda kusaidia madereva.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya madereva wameeleza kukasirishwa na jambo hilo la ukusanyaji wa kiasi hicho cha fedha na wengine kuwanyanyasa madereva wanaoonyesha kupingana nao, wamemuomba Mkuu wa Wilaya hiyo, Onesmo Buswelu kuingilia kati.

Mmoja wa madereva hao aliyejitambulisha kwa jina moja la Mmari, ameitaka serikali kukichunguza kikundi hicho ikiwa ni pamoja na wanaojiita Umoja wa Madereva na Wasimamizi wa Stendi kama wamefuata taratibu kwa mujibu wa sheria.

Kwa nyakati tofauti jana, baadhi ya madereva ambao wengine hawakutaka kutajwa majina yao, wamelalamikia kiwango hicho cha fedha kinachokusanywa kila siku, wakitaka kufanyika uchunguzi kubaini wanaokusanya fedha hizo kama wanatambuliwa na mamlaka za serikali.

"Tunalipa ushuru wa halmashauri Sh. 500 kwa siku, lakini kwa hawa watu wanaojiita umoja wa madereva au wasimamizi wa stendi ni tofauti, watu hawa wanataka uwalipe tena Sh. 1,000 kwa kila mzunguko utakaoufanya kwa gari aina ya Noah na kwa Toyota Hiace ni Sh. 2,000 kwa kila mzunguko utakaoenda. Wengi hatukubaliani nao tunaomba serikali itusaidie," alisema Frank Samson.

Inadaiwa watu hao wanafanya kazi hiyo katika vituo mbalimbali Wilaya ya Siha ambavyo wanakusanya fedha katika vituo vidogo vya magari yanayofanya safari za kutoa huduma kwa abiria wanaokwenda Naibili, Karansi, Ngarenairobi na kituo cha Sanya Juu kwenda Bomag'ombe.

"Tunanyanyaswa na hawa watu, kulazimishwa kulipa fedha hizo na ukikataa wanapiga simu kwa askari Polisi wa usalama barabarani na unakuja kukamatwa na kupigwa faini kwa madai kuwa umevuruga utaratibu.

"Kuna mwenzetu majuzi alipigwa na hawa jamaa, baada ya kupishana kauli lakini tunashangaa hawajakamatwa licha ya taarifa kufika kituoni,"alisema

Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo Hassam Hassan ambaye anadaiwa kushambuliwa na wanaodaiwa kuwa wasimamizi wa stendi ya Sanya Juu, alisema alipigwa na watu watatu na gari lake kuharibiwa.

Hata hivyo, mmoja wa watu ambaye alisema yeye siyo kiongozi lakini ni mwanachama wa Umoja wa Madereva, Ramadhan Rashid, alikiri kupokea fedha hizo kama kikundi cha madereva cha kusaidiana.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Onesmo Buswelu, alipoulizwa kuhusiana na suala hilo alisema: "Sina taarifa ya malalamiko ya madereva kutozwa 1000 kwa kila trip (mzunguko).

"Lakini Kitendo cha kupiga mtu siyo cha kiungwana, pia kuhusu kikundi cha hao madereva kama kipo kisheria hilo nalifuatilia ila naonya wasifanye kazi kinyume na katiba yao, nalifuatilia hili jambo ili nijue ukweli wake."



Ukurasa 15

**ANC yazidi kupungua nguvu lakini bado inadhibiti siasa Afrika Kusini**

Tamu, chungu za mitandao ya kijamii kwenye siasa



Ukurasa 18



Ukurasa 19

**Mahakama kuwaengua Wakurugenzi kusimamia uchaguzi, wadau wanena**


# siasa

JUMATANO MEI 15, 2019

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU




Ukurasa 20

**Hadhi ya Bobi Wine upinzani nchini Uganda yapanda zaidi**

# Wanasiasa katika Jiji la Mbeya walivyochuana mbele ya JPM

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

APRILI 26 mwaka huu, Rais John Magufuli, alifanya Mkutano wa Hadhara katika uwanja wa CCM, Ruanda Nzovwe jijini Mbeya, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya kihistoria katika Mkoa huo tangu alipochaguliwa kuongoza taifa mwaka 2015.

Mkutano huo ulipambwa na sare za vyama vya siasa hasa Chama cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), ambacho ndicho chama Kikuu cha Upinzani nchini.

Mbali na sare za vyama hivyo kupamba mkutano, lakini pia kulikuwa na vijembe na kejeli za chini chini kati ya wanachama, wafuasi na wakereketwa wa vyama hivyo viwili, ambapo wanachama wa CCM walikaa mbele na wa Chadema walisimama nyuma.

Wanachama wa Chadema walikuwa wanalalamika kutengwa kwenye mkutano huo ambapo Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' alilisema suala hilo mbele ya Rais, akidai Wanachadema wamewekwa nyuma ili wasionekane.

Ukiacha mbwembwe hizo za wanachama wa vyama hivyo pamoja na vituko vingine vilivyokuwa vinaonekana kwenye mkutano huo, uliohudhuriwa pia na mawaziri na manaibu waziri kadhaa, wanasiasa wenye nguvu katika Jiji la Mbeya nao walionekana kuchuana.

Viongozi hao wenye nyadhifa tofauti za kitaifa, kila mmoja alikuwa anaonyesha kujifagilia binafsi na kuwasaidia wananchi kuwasilisha kero zao kwa Rais.

**DK. TULIA**

Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, ndiye aliyekuwa wa kwanza kujimwaga jukwaani ambapo alianza kwa kumshukuru Rais Magufuli kwa kumteua kuwa mmoja wa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kisha akachaguliwa kuwa Naibu Spika.

Alisema wananchi wa Jiji la Mbeya wanafurahia heshima waliyopewa na Rais Magufuli ya kumteua katika nafasi hiyo kwa madai kuwa baadhi ya wananchi hao yeye ni mtoto wao,

INAENDELEA UK.16



Rais John Magufuli. **PICHA: MTANDAO**

**Upinzani na hatima ya Uchaguzi Mkuu katika jumuiya ya EAC** Ukurasa 14

# Upinzani, hatima ya Uchaguzi Mkuu katika jumuiya ya EAC



Viongozi wa upinzani Tanzania, Mwenyekiti wa CUF, Prof. Ibrahim Lipumba (kushoto), Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe (katikati) na Mwenyekiti wa NCCR-MAGEUZI, James Mbatia. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mashaka Mgeta**

KWA takribani miaka minne mfululizo kuanzia mwakani, nchi tano zilizo wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), zitakuwa na Uchaguzi Mkuu wa marais na wabunge.

Tanzania na Burundi zitafanya uchaguzi huo mwakani, wakati Uganda itakuwa mwaka mmoja baadaye (2021), Kenya (2022) na Rwanda (2024).

Pamoja na changamoto za Uchaguzi Mkuu kutofautiana kati ya nchi moja hadi nyingine, lakini 'tishio' la nguvu za upinzani limekuwa kubwa kwa muda mrefu, kiasi cha kutishia 'uhai' wa utawala kwa mataifa hayo.

Hata hivyo, wakati mataifa hayo yakijiandaa kwa uchaguzi huo, mazingira ya kisiasa yanaonyesha kupungua kwa nguvu za upinzani kunakotokana na mikakati tofauti ya kisiasa inayoundwa na kutekelezwa na viongozi waliopo madarakani.

Mwanaharakati ambaye pia ni mchambuzi wa masuala ya siasa na uchaguzi, Thomas Munanka, anasema ingawa kuna tofauti ya mfumo na ushiriki wa wananchi katika siasa na uchaguzi, mazingira ya jumla yanadhihirisha kuwapo kazi kubwa kwa wapinzani kushindana na watawala.

"Ukiona matukio mengi ya kisiasa yanayotokea kama kule Kenya ambapo Rais Uhuru Kenyatta alishikana mkono wa amani na mpinzani mkubwa wa siasa nchini humo, Raila Odinga na hapa kwetu ukiona kurejea kwenye Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa wapinzani akiwamo Waziri Mkuu mstaafu Edward Lowassa, ni dhahiri kwamba kunapunguza nguvu za wapinzani," anasema.

> Septemba Mosi, mwaka juzi, Jaji David Maraga aliyafuta matokeo kufuatia shauri lililofunguliwa na wapinzani hususani Odinga, na kuamuru kufanyika uchaguzi wa marudio ambao hata hivyo, Odinga aliususia.

Munanka anasema kabla ya kushikana mkono kwa Rais Kenyatta na Odinga, palikuwa na uhasama wa kisiasa uliochagiza vuguvugu la mageuzi kuwapo nchini humo, lakini hivi sasa ni kama Wakenya wanaongea lugha moja.

"Kwa wafuasi wa Odinga, ilikuwa mshtuko sana pale kiongozi wao alipojitokeza hadharani na kushikana mkono na Rais Kenyatta, kwa maana waliamini na wengine bado wanaamini kwamba Odinga alistahili kuwa mtawala lakini akaibiwa kura," anasema.

Katika Uchaguzi Mkuu wa Agosti 8, mwaka juzi, Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC) ya Kenya ilimtangaza Rais Kenyatta kushinda katika awamu ya pili ya utawala kwa tofauti ya kura milioni 1.4 dhidi ya Odinga, lakini wapinzani walikwenda Mahakama ya Juu ya nchi hiyo kupinga ushindi huo.

Septemba Mosi, mwaka juzi, Jaji David Maraga aliyafuta matokeo kufuatia shauri lililofunguliwa na wapinzani hususani Odinga, na kuamuru kufanyika uchaguzi wa marudio ambao hata hivyo, Odinga aliususia.

IEBC ilitangaza uchaguzi wa marudio kufanyika Oktoba 26, mwaka juzi ambapo Rais Kenyatta alishinda kwa asilimia 98, ingawa idadi ya watu waliojitokeza kupiga kura ilitajwa kupungua kwa takribani asilimia 40.

Matokeo hayo yaliibua ghasia nchini Kenya huku upinzani ukimtangaza na kumuapisha Odinga kuwa Rais wa Wananchi.

Hata hivyo, vurugu hizo 'zilizimwa ghafla' Machi 9, mwaka jana wakati Rais Kenyatta alipopeana mkono na Odinga, kisha 'wakawekeana ahadi' ya kushirikiana kuwaunganisha Wakenya na kushiriki shughuli za maendeleo ya taifa hasa zinazokuza uchumi na ustawi wa wananchi.

Pamoja na Wakenya kushtushwa na tukio hilo na baadaye kulipokea kwa namna tofauti, wapo ambao hawakulifurahia.

Miongoni mwa mwanaotajwa ni wanasiasa wa chama cha Jubilee kilichoanzishwa Septembe 8, 2016, wanaomuunga mkono Naibu Rais, William Ruto kuwania urais katika Uchaguzi Mkuu ujao.

Pia, kushikana mkono kwa Rais Kenyatta na Odinga, kuliwaleta pamoja wanasiasa hao wanaotoka kwenye `familia rafiki' za wapigania uhuru wa taifa hilo, Jaramogi Oginga Odinga na Rais wa kwanza wa taifa hilo, Jomo Kenyatta. Wote hao wamefariki.

Kuwa pamoja kwa Rais Kenyatta na Odinga kunatanua wigo wa kutofautiana kati ya mtawala huyo (Kenyatta) na Naibu wake (Ruto) huku Odinga na washirika wake wakidaiwa kupewa fursa nyingi zinazowafanya washiriki kampeni zisizo rasmi za kumsaidia Odinga dhidi ya Ruto anayeonekana kuwa na nguvu kubwa za kisiasa.

Mwanasiasa kijana nchini, Sophia Shamte, anasema tathmini ya hali hiyo inaonyesha kumuathiri Odinga, kwa vile wafuasi wake wengi waliokuwa wanamtegemea, wanaweza 'kumuona' kuwa msaliti mwenye kujali maslahi yake zaidi ya watu wengine.

"Unajua Odinga ana wafuasi wengi, sasa kama ikitokea kule kupeana mkono na hizi fursa anazozipata, na Wakenya wanasema nyingine ni nyingi zaidi ya zile za Ruto, basi tafsiri rahisi ni kwamba anaweza kuonekana msaliti, hivyo wasimwamini sana kama awali," anasema.

Kwa namna itakavyokuwa, Odinga bado atakuwa na ushindani mkubwa dhidi ya Ruto kutokana na ukweli kwamba Rais Kenyatta atakuwa anamaliza utawala wake, hivyo kutotumia nguvu kubwa kumuunga mkono mgombea urais yeyote kati ya watakaojitokeza, hasa wawili hao.

**WAPINZANI KUMUUNGA MKONO MAGUFULI**

Nchini Tanzania, kasi ya waliokuwa wapinzani katika ngazi tofauti hasa za uwakilishi wa wananchi kurudi ama kujiunga CCM ili kuunga mkono jitihada za serikali ya Rais John Magufuli, kunaelezwa kufifisha nguvu za upinzani.

Kuporomoka kwa wabunge na madiwani wanaojiondoa kwenye vyama vya upinzani hasa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) ambacho ni chama kikuu cha upinzani na Chama cha Wananchi (CUF), kunaakisi kufifia kwa nguvu za kambi hiyo dhidi ya chama tawala katika Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Kujiunga katika CCM kwa aliyekuwa mgombea urais wa Chadema mwaka 2015, akiungwa mkono na vyama vinne vilivyounda Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), Edward Lowassa, kunaweza kusababisha kupungua kwa idadi ya watu watakaowachagua (wapinzani) na ikiaminika kwamba mwanasiasa huyo ana wafuasi wengi wanaomuunga mkono.

Pia kuna 'kusambaratika' kwa CUF kulikotokana na mgogoro wa uongozi uliodumu muda mrefu kati ya pande mbili zilizomuunga mkono Profesa Ibrahim Lipuma (Mwenyekiti aliyekuwa akitambuliwa na Msajili wa Vyama vya Siasa) na ile ya aliyekuwa Katibu Mkuu, Maalim Seif Sharif Hamad.

Hata hivyo, kambi ya Maalim Seif ilijiondoa CUF na kujiunga Alliance for Change and Transparency (ACT-Wazalendo), hatua ambayo inatafsiriwa na baadhi ya wachunguzi wa masuala ya siasa kwamba inaweza kurudisha nyuma jitihada za 'kujipanga' kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Mbali na hayo, Mhadhiri mmoja wa sayansi ya siasa ambaye hataki jina lake kuandikwa gazetini, anasema mazingira yaliyopo sasa hayatoi fursa pana kwa wanasiasa wa upinzani kuwafikia wananchi ama sauti zao kusikika, hivyo kuweza kuwa sababu ya kutofanya vizuri katika uchaguzi huo.

**KAGAME NA MSAMAHA WA WAFUNGWA WA KISIASA**

Ingawa hatua ya Rais Paul Kagame kuongezewa muda wa utawala kufika mwaka 2034 iliwachukiza baadhi ya raia wa nchi hiyo, lakini 'machozi yao yalifutwa' na tamko la msamaha wa waliokuwa wafungwa wa kisiasa 2140.

INAENDELEA UK.15

# ANC yazidi kupungua nguvu lakini bado inadhibiti siasa Afrika Kusini

**Na Ani Jozeni**

CHAMA cha Ukombozi wa Afrika Kusini, ANC kimepata kura chini ya asilimia 60 kwa mara ya kwanza.

Takwimu zote za kiwango cha matokeo ya awali wakati kura zilipopigwa Mei 8 zilionyesha kuwa itakuwa tabu kwa chama hicho kufikia asilimia 60, licha ya asilimia 62.5 ilizopata wakati wa uchaguzi mkuu mwaka 2014.

Hapa nchini, mabadiliko hayo ya uungwaji mkono wa ANC miongoni mwa wapiga kura nchini Afrika Kusini yalimwibua kwa mara nyingine tena aliyekuwa katibu mtendaji mkuu wa CCM ilipoanzishwa mwaka 1977 na pia mmoja wa waliosuka katiba yake, Pius Msekwa.

Aliwaasa viongozi CCM 'kujifunza' kutoka uchaguzi wa viti vya ANC.

Hata hivyo, zipo tofauti za kina kati ya Afrika Kusini na Tanzania, kiasi ambacho kuwaasa viongozi wa CCM wajifunze jambo kutoka uchaguzi mkuu ambako ANC imepoteza umaarufu kwa kiwango fulani kunaweza kubishiwa, wengine wakisema ni kulinganisha maembe na mananasi.

Yumkini, kuna kanuni ya jumla ambayo mwanazuoni Msekwa alikuwa akiitanguliza, kuwa hata hivi vyama kongwe vya kupigania uhuru ambavyo kimsingi ni pacha, ANC na CCM kupitia TANU, navyo hatimaye vitasombwa na mageuzi.

Itakumbukwa kuwa kiongozi wa kihistoria wa ANC, Nelson Mandela, alipata mafunzo ya kijeshi Algeria kwa hati ya kusafiria ya hapa.

Nchini Algeria chama chake cha ukombozi kimekaa madarakani tangu washinde Ufaransa katika vita vya mitaani Algiers ambako Wazungu wengi walidhurika kwa kuchomwa visu na Waalgeria wengi waliteswa katika vituo vya polisi vya Wafaransa ili waeleze mifumo, mitandao ya FLN, jeshi la ukombozi.

Chama hicho kimekuwa madarakani na kuona viongozi kadhaa hasa wakitokana na jeshi la ukombozi, wa kiraia mara kadhaa wakipinduliwa, na aliyekaa muda mrefu wa miaka 20.

Ni Abdelaziz Bouteflika aliondolewa madarakani mwezi uliopita, kwa njia ya katiba kumaliza maandamano ya muda mrefu. Pia yuko Jenerali Omar al Bashir.

Alichosema Msekwa na kinachoonekana bayana ni kile ambacho katika sayansi kinajulikana kama 'sheria ya mpauko,' (law of atrophy) kuwa hakuna kitu kinachodumu kuwa chema wakati wote, kwani kila kitu kina udhaifu mahali, na baada ya muda kupita udhaifu huo unakuwa kero.



Spika mstaafu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Pius Msekwa. **PICHA: MTANDAO**

"Ni Abdelaziz Bouteflika aliondolewa madarakani mwezi uliopita, kwa njia ya katiba kumaliza maandamano ya muda mrefu. Pia yuko Jenerali Omar al Bashir.

Udhaifu kwa vyama vya siasa unaendana na mazingira ya nchi husika, hivyo inakuwa vigumu kueleza 'makosa' ya ANC na kufananisha na CCM, au kumlinganisha Nyerere na Mandela, Mbeki na Mwinyi, Zuma na Mkapa au Kikwete, halafu/mwisho Ramaphosa alinganishwe na Magufuli. Itakuwa ni jaribio la kulazimisha hisia, hivyo iishie katika kujikanganya.

Katika mazingira hayo, unaweza kusema kuwa somo analotaka kutoa Msekwa ni la kweli kutokana na kanuni ya jumla ya mpauko wa vyama vya siasa, kama ulivyo mpauko wa uongozi kwa jumla, kama ilivyo katika awamu tofauti.

Ni kawaida kuwa utawala mpya unaanza kwa shangwe na mambo mapya na kwa jumla hutawala jinsi watu wanavyofikiri, kuweka vigezo vipya vya kuangalia kipi kinaenda na kwa kasi gani, na kipi bado, halafu kuna maeneo yasiyotawaliwa na kinachofanywa na serikali bali ni matokeo ya jinsi kazi yake inavyoingiliana na hali halisi.

Ndiyo hapo matokeo yanaonekana katika uchaguzi mkuu unaofuata, kuwa watu wamechoka kiasi gani. Somo la jumla ambalo mwanazuoni huyo alitaka kuainisha inaelekea ni hili suala la kushuka kutoka asilimia 50 na kuingia katika asilimia 50 na zaidi, ikiwa na maana kuwa kuhakikisha ANC ina robo tatu ya viti kama wakati ubaguzi ulipoondolewa na uchaguzi mkuu kufanyika 1994 sasa ni historia.

Na kushuka kutoka asilimia 62.5 (kama CCM ilivyopata katika uchaguzi mkuu wa 1995 halafu pia wa 2015, upinzani ukishuka na kupanda katika vipindi tofauti) ni ishara kuwa kimsingi chama tawala kinaweza kushindwa.

Tume ya Uchaguzi ya Afrika Kusini iliorodhesha vyama 48 vilivyoweka wagombea katika uchaguzi wa majimbo na kitaifa, ambako Afrika Kusini hakuna majimbo kwa maana ya mbunge wa eneo fulani ila mikoa au kanda ndizo zinatoa orodha ya wagombea wa chama husika.

Idadi ya wanaoingia bungeni au mabaraza ya uwakilishi kikanda inaamuliwa na asilimia gani ya kura zinazopatikana, hivyo kuweka asilimia ya walioorodheshwa kuingia bungeni endapo chama hicho kingechukua viti vyote, au nusu yake, n.k.

Baadhi ya vyama vya upinzani vina wapiga kura wengi katika majimbo kadhaa, lakini ni ANC peke yake inayoungwa mkono kwa dhati kote nchini.

Ripoti zinaonyesha kuwa ANC iliongeza wingi wa viti katika uchaguzi mkuu 1999 na pia 2004 lakini baada ya hapo imekuwa inapoteza viti kiasi tu, uchaguzi wa 2009 na pia 2014.

Alichokuwa anasema Msekwa ni kuwa hali hii ya kupungua ushawishi wa ANC ndiyo sasa hali yake ya 'kukomaa,' kuwe ule ujana wa kuchukua madaraka na wananchi kuogopa njama za makundi yanayojazwa manoti kupambana na ANC, au wengine walipelekwa kwa mihemko ya kikanda na kikabila, walikuwa wanapungua.

Lakini ukinzani ndani ya ANC ulikuwa lazima uongezeke chama hicho kinavyodumu madarakani, hasa kupigana na kivuli chake cha sera za kimapinduzi.

Kivuli hicho kilizaa ukinzani wa kina ndani ya ANC ambako kiongozi wa vijana, Julius Malema alianza kuwa maarufu kwa kutaka ANC irudi katika mwelekeo wake wa jadi wa kutwaa ardhi iliyochukuliwa kwa mabavu na Wazungu wakati wa ukoloni na ubaguzi wa rangi.

Ni chama cha EFF (economic freedom fighters) ambacho wafuasi wa Malema walianza kugawanyika katika vikundi na vyama tofauti, kama ni ardhi tu au ni pamoja na njia kuu za uchumi ziwe za taifa.

Kwa upande mwingine makundi ya Wazungu pia yamekuwa yakitafuta uelekeo na kuna chama kinachotaka eneo la Wazungu au ukanda/majimbo/miji ambako ni wengi yajitegemee, yawe na tawala za ndani (hali inayokumbusha sera za Bantustan, za majimbo yenye uhuru bandia wakati wa ubaguzi).

Kwa vile vyama vyote hivyo hasa ni vya makundi tofauti ya jamii yanayoweka madai ya kupunguza kuwezo wa serikali kuu kwa sababu hii au ile, bado hayana uwezo wa kimsingi wa kuipangua ANC madarakani, hata kama wako wengi ndani ya ANC wanaohofia mwenendo wa utawala.

Mfano mmoja ulikuwa ni tatizo la rushwa wakati wa utawala uliopita wa Jacob Zuma, lakini ukiangalia unakuta Malema amejazwa mapesa yasiyojulikana yalikotoka, na huwezi kusema kuwa waliomjaza mapesa hayo wana dhamira njema ya kisiasa na kiuchumi endapo atafika madarakani.

Hivyo, CCM haiwezi kujifunza chochote moja kwa moja kutoka uchaguzi mkuu wa Afrika Kusini, nje ya kwamba chama tawala 'kinachokwa' na madai ya makundi maalum yanapozidi, ni hatari

## Upinzani na hatima ya Uchaguzi Mkuu katika jumuiya ya EAC

**INATOKA UK.14**

Msamaha huo uliotolewa mwaka jana, uliwahusisha watu tofauti wakiwamo waliohukumiwa kwa makosa mbalimbali.

Miongoni mwa waliokuwa wafungwa hao ni Mwenyekiti wa chama cha Force Democratique Unies du Rwanda (FDI) Victorie Ingabire ambaye pamoja na mwanamuziki Kizito Mihigo, walihukumiwa mwaka 2010.

Ingabire alifungwa baada ya kupatikana na hatia ya kuchochea raia kuiasi serikali, kuunda makundi ya silaha ili kuivuruga nchi na kupuuza mauaji ya kimbari ya 1994 dhidi ya Watutsi.

Lakini kwa sehemu kubwa, hatua ya Mahakama nchini humo kumuachia huru mpinzani mkuu wa Rais Kagame, Diana Rwigara, Desemba mwaka jana, kuliibua hisia mpya za upinzani kupata nguvu nchini humo.

Mwanasiasa huyo (Rwigara) alihukumiwa kifungo cha miaka 22 jela baada ya kuzuiwa kuwania urais katika Uchaguzi Mkuu uliopita nchini humo, akitajwa kuwa mpinzani mkuu wa Rais Kagame

**Itaendelea Jumatano ijayo.....**

**Mwandishi wa makala haya anapatikana kupitia simu namba 0754691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com.**

# Wanasiasa katika Jiji la Mbeya walivyochuana mbele ya JPM

INATOKA UK.13

dada yao, mama yao na baadhi ni shangazi yao.

"Mheshimiwa Rais, jana (Aprili 25) ulipokewa kwa kishindo na ulisimama maeneo mbalimbali kwa sababu wananchi hawa walitamani sana wakuone na wazungumze na wewe," alisema na kuongeza:

"Hata hivyo kutokana na muda, wanafahamu wazi kuwa fursa inaweza ikawa ndogo... kwa sababu hiyo mimi kijana wao, dada yao na mtoto wao nitawasilisha salamu zao."

Baada ya salamu hizo aliwasilisha changamoto za wananchi akianzia na za wananchi wa Kata ya Nzovwe ambao waliathirika kufuatia mafuriko yaliyotokea hivi karibuni kutokana na mvua zilizokuwa zikiendelea kunyesha.

Dk. Tulia alisema zaidi ya kaya 100 ziliathiriwa na mafuriko hayo na kwamba ameshafuatilia na kubaini kuwa kuna mipango ambayo Serikali inaendelea kuifanya ili kudhibiti sababu za mafuriko katika eneo hilo.

"Taarifa zilizopo ni kuwa itachukua miezi 18 kutengeneza mitaro ili maji yasiingie kwenye makazi," anasema.

Mbali na taarifa hiyo, pia Dk. Tulia aliwasilisha kilio cha wafanyabiashara wadogo wadogo maarufu 'machinga', akidai kuwa kundi hilo linakabiliwa na changamoto ya kukosa maeneo ya kufanyia biashara zao.

Alimuomba Rais Magufuli kuwasaidia wafanyabiashara hao kwa kuidhinisha eneo la Uwanja wa Ndege wa Zamani libadilishwe matumizi na kuwa la wafanyabiashara hao kufanyia shughuli zao.

"Nianze kwa kumpongeza Mkuu wa Mkoa (Albert Chalamila) kwa kazi anazofanya hapa jijini Mbeya na Mkoa mzima, lakini sisi machinga tumepata changamoto kidogo, tunaomba mheshimiwa Rais useme neno nasi tutapona," alisema Dk. Tulia.

Aidha akasema, wananchi wa Jiji la Mbeya wanamshukuru Rais Magufuli kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha sekta ya Afya, hasa katika vituo vya afya vya Kata za Nzovwe na Iyunga ambavyo kwa ujumla vilipatiwa zaidi ya Sh. Bilioni 1.1.

### MBUNGE MBILINYI (SUGU)

Baada ya Dk. Tulia kumwaga sera zake aliyefuata alikuwa ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' ambaye alianza kwa kukumbushia tukio la kufungwa jela mwaka jana.

Akitumia lugha ya kisanii, Sugu alisema wakati akiwa gerezani alipata taarifa kuwa Rais Magufuli yuko Iringa na hivyo akawaza kuwa pengine akitoka huko angefanya ziara mkoani Mbeya na hivyo angemkosa.

"Niliposikia kuwa umeondoka na Mbeya utafanya ziara baadaye, nikasema inshallah ukija utanikuta na nashukuru umenikuta niko nje Mungu ni Mwema sana," alisema.

Hata hivyo, wakati Sugu akitoa maelezo hayo wafuasi wa CCM walisikika wakisema 'ulifungwa kwa matakwa yako...endelea hivyo.'



Sehemu ya umati wa wananchi waliojitokeza kumlaki Rais John Magufuli katika mojwapo ya maeneo aliyopita.

> "...sasa nakuhakikishia endapo utawezesha mradi huo kukamilika, hakuna legacy (urithi) kubwa utakayokuwa umeacha kama hiyo kwa jiji letu.

Baada ya kukumbushia masuala hayo Mbunge huyo alianza kuusaka umaarufu kwa kutaja changamoto zinazowakabili wananchi wa Jiji la Mbeya, akianza na tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama maeneo mbalimbali ya Jiji hilo.

Alisema kwa mujibu wa taarifa alizozipata wakati anafuatilia katika mamlaka ya Maji ya jiji hilo ni kwamba ni asilimia 60 tu ya wananchi wa Jiji la hilo ndio wanaopata maji na asilimia zilizobakia hawapati kabisa.

Sugu alisema wataalamu walipofanya tathmini walikuja na suluhisho la kudumu kwa kutaka kuchukua maji kutoka chanzo cha Mto Kiwira ambalo lingemaliza changamoto hiyo katika Jiji hilo na maeneo ya jirani.

"Wataalamu walishafanya upembuzi yakinifu wa mradi ule na walisema zinahitajika Sh. bilioni 70... sasa nakuhakikishia endapo utawezesha mradi huo kukamilika, hakuna legacy (urithi) kubwa utakayokuwa umeacha kama hiyo kwa jiji letu," anasema.

Alibainisha kwamba kwa mujibu wa wataalamu, endapo mradi huo utatekelezwa kuna uwezekano maji hayo yakapelekwa mpaka Mji wa Tunduma mkoani Songwe, umbali wa zaidi ya Kilomita 100 kutoka Mbeya Mjini.

Aidha, Sugu aliungana na Dk. Tulia kuwasemea wamachinga akisema hata yeye aliwahi kufanya biashara ya umachinga katika Soko la Mwanjelwa baada ya kuhitimu kidato cha nne kabla hajaingia kwenye mziki.



Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, katika moja ya shughuli zake mkoani Mbeya. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Mbunge huyo alibainisha kuwa wamachinga ni tofauti na wafanyabiashara wengine na hivyo hawatakiwi kuwekewa eneo maalumu la kuuzia biashara zao na badala yake wanatembeza biashara zao barabarani.

"Kwenye 'ishu' ya wamachinga nakuunga mkono kwa asilimia 100 mheshimiwa Rais, kama ulivyosema jana barabara tumejenga wenyewe na wewe ulikuwa Waziri wa Ujenzi... ulisimamia vizuri na ukasema wamachinga wako huru... machinga si wa kuwekewa eneo maalumu," alisema.



Mbunge wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu'.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila.

Alisisitiza kuwa kwenye miji iliyoendelea duniani kama New York Marekani, Beijing China, Tokyo Japan na miji mingine iliyoendelea machinga wanatembeza bidhaa zao barabarani na kwamba kinachotakiwa ni kuwekewa utaratibu mzuri.

Vilevile alimuomba Rais Magufuli kuwezesha upanuzi wa barabara Kuu ya Tanzania na Zambia (Tanzam), katikati ya Jiji la Mbeya na kufanywa kuwa yenye njia nne.

Alimsisitizia Rais kuwa wananchi wa Jiji la Mbeya wanamkubali tofauti na taarifa ambazo zimekuwa zikizushwa kuwa kuna mgawanyiko wa kisiasa na akaomba yeye atumike kuandaa majadiliano ya kisiasa kuondoa mafundo fundo hayo ya kisiasa.

### DK. MARY MWANJELWA

Baada ya Mbunge Mbilinyi mtaalamu wa muziki wa 'Hip Hop' kujimwaga, alifuata Mbunge wa Viti Maalumu wa Mkoa wa Mbeya (CCM), Dk. Mary Mwanjelwa ambaye alianza kwa kumwaga sera zake mithiri ya mhubiri.

Mwanjelwa alimumwagia sifa mbalimbali Rais Magufuli kuwa ni Rais wa wanyonge, kipenzi cha Watanzania na akamshukuru kwa kufanya ziara katika Mkoa wa Mbeya kwa mara ya kwanza tangu alipochaguliwa mwaka 2015.

Kama ilivyokuwa kwa Naibu Spika, pia alimshukuru kwa kumteua kuwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa madai kuwa uteuzi huo ni heshima kwa wana Mbeya.

"Mtunosisye bha kukaja, Mheshimiwa Rais tunakushukuru kwa heshima uliyotupa wana-Mbeya, kwanza kwa kufanya ziara ya siku nane ambapo utapita katika wilaya zote... ulipokuwa unaingia ulipokewa na umati mkubwa akiwamo mbunge wa Jimbo hili na madiwani wote," alisema Dk. Mwanjelwa.

Baada ya kumwaga sifa hizo alimuomba Rais Magufuli kuharakisha mradi wa upanuzi wa barabara katikati ya Jiji la Mbeya ili kupunguza msongamano wa magari.

Vilevile aliomba mradi wa ujenzi wa barabara ya mchepuko kwa ajili ya magari ya mizigo kutoka Uyole mpaka Songwe uharakishwe ili kupunguza ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara.

### CHALAMILA ANG'AKA

Kabla ya Kumkaribisha Rais Magufuli kuhutubia umati wa wananchi waliokuwa wamehudhuria Mkutano huo, Mkuu wa Mkoa Albert Chalamila, alizungumzia masuala mbalimbali.

Chalamila alitoa takwimu za miradi mbalimbali pamoja na fedha zilizotumika kuitekeleza, ikiwamo miradi ya barabara, elimu na afya ambapo alisema serikali imetoa fedha nyingi.

Alikumbushia ufisadi uliofanywa na baadhi ya watendaji wa Soko la Kimataifa la Mwanjelwa ambalo alidai kuwa ni miongoni mwa masoko katika Afrika Mashariki na Kati ambayo yalijengwa kwa ufisadi mkubwa.

Aliwataka wafanyabiashara wa Jiji la Mbeya kuendelea kuitumia fursa ya soko hilo licha ya ufisadi uliofanyika na waache kutaka kupanga bidhaa zao chini kuzunguka soko hilo.

"Unapoamua kujenga choo kizuri ndani basi ubaki humo humo ndani, lakini ukianza tena kwenda kwenye migomba watu watakuona kama mchawi... soko lile lilijengwa kwa Sh. Bilioni 19.5 lakini hiyo si sababu ya watu kulikimbia," alisema Chalamila.

Hata hivyo, alionyesha kumkuna zaidi Rais Magufuli alipotoa takwimu za ukusanyaji wa mapato katika Jiji la Mbeya ambapo alisema makusanyo yamepanda kwa kiasi kikubwa.

Alisema kabla hajateuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa huo, Jiji la Mbeya lilikuwa linakusanya Sh. milioni nane mpaka 10 kwa mwezi, lakini baada ya kuingia yeye na kudhibiti mianya ya upotevu soko hilo linaingiza milioni 40 mpaka milioni 42 kwa mwezi.

Aidha, alisema katika Soko la Sido vilijengwa vibanda zaidi ya 900 baada ya Soko la Mwanjelwa kuungua mwaka 2007 na kwamba wafanyabiashara hao walikuwa hawalipi kodi na kwamba wakihojiwa wanadai wao ni wahanga.

"Nilisema huo uhanga una mwisho wake na mpaka sasa ninapozungumza kodi iliyokwishawasilishwa kwa Mkurugenzi wa Jiji ni milioni 422, lakini kodi ambayo imekusanywa na TRA, wakiwa hawajawahi kukusanya huko nyuma ni Sh. milioni 687," anasema.

### JPM ANENA

Baada ya Chalamila kumaliza kujimwaga alimkaribisha Rais Magufuli awahutubie wananchi ambapo mbali na mambo mengine alianza kwa kuwahakikishia wananchi wa Mkoa wa Mbeya kuwa hawezi kumuondoa Chalamila katika Mkoa huo.

> "Taarifa zilizopo ni kuwa itachukua miezi 18 kutengeneza mitaro ili maji yasiingie kwenye makazi.

Alisema kiongozi huyo anafanya kazi nzuri na wote wanaompiga vita wamekwama na akamtaka aendelee kuchapa kazi ya kuunyosha mkoa huo kama alivyokuwa ameomba mwenyewe awali.

Vilevile aliwashukuru wananchi mkoani humo kwa kujitokeza kwa wingi kumpokea kuanzia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (Sia) mpaka alipoingia mjini wakiongozwa na viongozi mbalimbali akiwemo mbunge Sugu pamoja na madiwani wa upinzani.

Alimtania Sugu kuwa anaonekana ni mpinzani kwa sura lakini moyoni ni CCM na kwamba ndio maana alishiriki mapokezi na kumsindikiza mpaka Ikulu ndogo.

Hata hivyo, alikata kiu ya wamachinga kwa kuidhinisha eneo la Uwanja wa ndege wa zamani ambalo waliombewa na viongozi litumike kwa ajili ya wamachinga na akaagiza miundombinu muhimu iwekwe na Serikali, tamko ambalo linasababisha shangwe kulipuka uwanjani hapo.



Waandamanaji Sudan wakiwa mtaani. **PICHA: MTANDAO**

## Duru mpya ya mazungumzo yaanza

• Waandamanaji wasalia Makao Makuu ya Jeshi

VIONGOZI wa kijeshi wa Sudan na waandamanaji wameanza duru mpya ya mazungumzo kwa ajili ya kufikia makubaliano ya kukabidhi madaraka kwa utawala wa kiraia, huku waandamanaji wakiendelea kupiga kambi nje ya Makao Makuu ya Jeshi.

Jumamosi iliyopita, Muungano wa Uhuru na Mabadiliko ambao ni mwamvuli wa vuguvugu la waandamanaji, ulisema viongozi wa kijeshi walituma mwaliko wa mazungumzo mapya baada ya mkwamo wa siku kadhaa.

Msemaji wa muungano huo Rashid al-Sayed alisema awali mazungumzo hayo yalikuwa yafanyike siku hiyo ya Jumamosi, lakini yakaahirishwa hadi juzi yalipoanza rasmi tena.

Sayed hakufafanua kwanini mazungumzo hayo yalisogezwa mbele, lakini vyanzo tofauti ndani ya muungano vinasema kulihitajika muda zaidi kwa ajili ya mashauriano ya kiutawala.

Msemaji wa Baraza la Kijeshi linalotawala nchini humo, Luteni Shamseddine Kabbash, alithibitisha kuanza kwa duru mpya ya mazungumzo na kuongeza kuwa yanafanyika kwenye mazingira yenye kutia moyo ili kufikia makubaliano ya kipindi cha mpito.

"Tunakubaliana nao juu ya muundo wa jumla wa mfumo wa kiutawala wakati wa kipindi cha mpito kwa kuzingatia baraza huru, mfumo wa serikali, mfumo wa bunge na mifumo mingine," anasema na kuongeza:

"Tulichogundua ndani ya pendekezo lao lililowasilishwa kwetu ni kwamba waliondoa chanzo cha sheria...maoni yetu ni kwamba Sheria ya Kiislamu na tamaduni katika Jamhuri ya Sudan, viwe ndio chanzo cha sheria."

Duru hiyo mpya ya mazungumzo inakuja wakati maelfu ya waandamanaji wakiendelea kupiga kambi nje ya makao makuu ya Jeshi jijini Khartoum.

Wanasema wamedhamiria kulishinikiza Baraza la Kijeshi kukabidhi madaraka, kama ambavyo walivyomuondoa Omar al-Bashir.

Viongozi wa kijeshi na waandamanaji wanatofautiana juu ya nani ataliongoza baraza la mpito.

Jeshi linapendekeza baraza jipya liongozwe kijeshi, huku waandamanaji wakitaka uwakilishi mkubwa wa raia ndani ya baraza hilo.

Mwishoni mwa mwezi uliopita, muungano wa upinzani uliwasilisha mapendekezo yao kwa jeshi kuhusiana na serikali ya mpito, itakayoongozwa kiraia.

Wakati huohuo, waandamanaji wamezuia mtaa mkubwa ulioko kando ya mto Nile kwa kutumia mawe na miti, baada ya vikosi vya usalama kuwazuia kuingia eneo ambalo wenzao wamepiga kambi.

Baraza la kijeshi limelaani kitendo hicho likisema hakikubaliki na kinachochea vurugu, hivyo kufanya maisha kuwa magumu kwa raia wengine. **AFP**

# Tamu, chungu za mitandao ya kijamii kwenye siasa



Baadhi ya wabunge wakiwa katika majukumu yao. **PICHA: MTANDAO**

**Na Fransisko Mpangala**

MWISHONI mwa mwaka jana, simu yangu ya smartphone ilizima ghafla na kushindwa kuwaka tena. Kwa kuwa ilitokea ghafla sana, ilinichukua miezi miwili kujipanga upya ili kununua smartphone nyingine.

Kitendo cha kukosa smartphone kwa miezi miwili kilikuwa pigo kubwa sana kwangu kwani, matumizi ya simu ya kawaida (tochi) ambayo hayana huduma ya intaneti yalininyima fursa ya kupata habari na mijadala mingi ya kisiasa kupitia mitandao ya kijamii kama nilivyozoea. Hakika nimekuja kuithamini sana mitandao ya kijamii, hasa kipindi kile cha miezi miwili niliyoshindwa kuipata huduma yake (wanasema ukose kitu ndipo ujue umuhimu wake).

Kushindwa kuitumia mitandao hii kulinifanya kuitazama kwa namna ya kipekee na lazima nikiri kuwa msukumo wa kuandika makala hii unatokana na shauku ya kuelezea umuhimu wa mitandao ya kijamii ulioongezeka maradufu kipindi niliposhindwa kuipata huduma yake.

Mitandao ya kijamii inatafsiriwa kama nyenzo ya kuunganisha watu kwa kuwaleta pamoja na kujenga urafiki miongoni mwao ndani na nje ya nchi. Pia inaunganisha watu wenye shauku ya aina moja, kwa maana mtumiaji anapaswa kujitambua mapema, na kujiweka katika kundi analodhani linamfaa au lina manufaa zaidi kwake.

Binafsi ninapenda kufuatilia mambo ya siasa, kwa maana hii niligeuza mitandao ya kijamii kama chombo cha habari kwa kupafanya mahali pa kujifunza, kuhabarika na 'kijiwe' cha kujadili mambo ya siasa.

Ingawa zipo faida nyingi za mitandao ya kijamii, itakuwa ni ajabu sana nikijisahaulisha kuwa hakuna changamoto zilizoletwa na mitandao hiyo. Hivyo, makala hii italenga kuchambua faida na hasara zilizoletwa na mitandao ya kijamii kwa upande wa siasa na wanasiasa kwa ujumla.

> Mitandao hii hasa ya kijamii ni kama 'maporomoko' ya habari mpya kila sekunde yakiitwa 'streaming', 'TL' na majina mengine...

**TAMU ZA MITANDAO YA KIJAMII**

Mitandao ya kijamii inatoa fursa ya kupata habari nyingi za kisiasa ndani ya muda mfupi.

Katika moja ya makala ya mwandishi Christian Bwaya inayohusiana na mambo ya teknolojia anasema: "Mitandao hii hasa ya kijamii ni kama 'maporomoko' ya habari mpya kila sekunde yakiitwa 'streaming', 'TL' na majina mengine... Kadri unavyofuatilia habari moja, ndivyo unaletewa 'mafuriko' ya zingine mpya...hukutani na ishara kuwa sasa umekaribia kufikia mwisho, kapumzike...matokeo yake unaweza kujikuta muda wote unaunganisha habari moja kwenda nyingine."

Ingawa mwandishi huyu alikuwa anajaribu kuzungumzia changamoto za kutumia mitandao hii (nitajadili mwishoni) lakini kwa upande mwingine maneno hayo yanaelezea faida kubwa iliyoletwa na mitandao ya kijamii kwa wadau wa siasa.

Mtumiaji ana uhakika wa kupata habari nyingi za kisiasa kadri muda na nafasi yake itakavyomruhusu.

Mtumiaji halazimiki kusubiria au kutegemea taarifa ya habari kwa kuwa ana uhakika wa kupata habari 'mithili ya mafuriko' muda wowote anaojisikia kiganjani.

**FURSA**

Mitandao ya kijamii kwa upande mwingine imezidisha fursa kwa wadau wa siasa kutoa maoni yao kuhusiana na habari, mijadala au makala mbalimbali kwa njia ya ujumbe mfupi 'comments'.

Kwa maana hii ushirikishwaji wa watu kutoa mawazo yao kuhusiana na mambo ya kisiasa umeongezeka maradufu.

Pia inatoa fursa kwa mtoa habari, mjadala au makala kujua maoni ya watu kuhusiana na taarifa husika.

**WANAHARAKATI**

Faida nyingine inayotokana na mitandao ya kijamii ni kuibuka kwa kundi la watu wanaojiita 'wanaharakati'.

Kwa kujua na kutambua nguvu ya mitandao ya kijamii katika kufikisha ujumbe, 'wanaharakati wa mitandao ya kijamii' hufanya kila wawezalo kuitumia ipasavyo kufikisha sauti zao zisikike na hatimaye kuleta tofauti inayokusudiwa kwa nia njema.

Hii imesaidia kufikisha kero mbalimbali kwa serikali au viongozi wao ili kusaidia kuzipatia ufumbuzi. Kwa maana hii, mtu akishindwa kufikisha kilio chake kupitia vyombo vya habari, bado anaweza kuwatumia 'wanaharakati wa mitandao ya kijamii' kufikisha kero zake kwa viongozi na wanasiasa kwa ajili ya ufumbuzi.

**KAZI ZA VIONGOZI**

Isitoshe mitandao ya kijamii imewarahisishia wananchi kuona kazi mbalimbali zifanywazo na viongozi wao. Kupitia ukurasa wa instagram wa mbunge wa Segerea Bonnah Kaluwa, napata fursa ya kuona kazi mbalimbali zinazofanywa na mbunge huyo katika jimbo lake.

Anaitumia pia kutoa taarifa mbalimbali kama ratiba ya mikutano kati yake na wananchi wa jimbo lake. Kwa maana hiyo mitandao ya kijamii imewasaidia wanasiasa kufikisha taarifa zao kwa urahisi na kuwaonyesha wapigakura kazi mbalimbali za kimaendeleo wazifanyazo kwenye maeneo yao.

**KAMPENI ZA KISIASA**

Mitandao ya kijamii pia inatoa fursa kwa wananchi na wadau wa siasa kuona vikao na kampeni za kisiasa 'mubashara'.

Hii imewarahisishia wanasiasa kutangaza sera na kufikisha jumbe zao kwa urahisi. Nakumbuka mwaka 2016 nilifuatilia kwa karibu kampeni za Rais Donald Trump wa Marekani kupitia facebook 'mubashara'.

**CHANGAMOTO**

Hata hivyo, hakuna zuri lisilokosa kasoro, zipo changamoto zilizoletwa na mitandao ya kijamii kwa upande wa siasa na wanasiasa.

Moja ya changamoto kubwa inayoikabili mitandao ya kijamii kwa upande wa siasa (na kwa ujumla wake) ni kuwepo kwa habari nyingi 'feki' na za kizushi.

Kwa kuwa mitandao ya kijamii haina uchujwaji wa habari (filtration) kama ilivyo kwa vyombo vya habari, mchanganyiko wa habari za ukweli, uongo au zilizozidishwa chumvi ni nyingi sana.

Shida inazidi kuwa kubwa kwa wapokeaji wa habari hizo ambao wanaupokea uongo uliotolewa kwa nia mbaya kama ulivyo.

Hii inatokana na watu wengi kuwa wavivu kuchambua kwa undani au kufuatilia ukweli wa taarifa mbalimbali. Wapo watu kwenye mitandao ya kijamii ambao kwa nyakati nyingine huitumia vibaya kuwadhalilisha viongozi wenye heshima na hadhi kubwa kwenye jamii.

Ingawa yawezekana baadhi ya tuhuma zinazoanzia kwenye mitandao ya kijamii zikawa na ukweli, lakini lugha inayotumika kuwasilisha zikawa si nzuri (matusi).

Wapo wenye chuki binafsi ambao huzusha kwa makusudi habari zilizojaa chuki kwa viongozi mbalimbali kwa lengo la kuwadhalilisha au kuwashushia hadhi yao.

Mara nyingi watu wa aina hii hung'ang'ania mambo yasiyo na msingi, lakini yenye madhara kwa hadhi na heshima ya mwanasiasa husika katika jamii.

Hakika hili si jambo zuri kwani viongozi na wanasiasa hawa ilichukua muda mrefu kuitengeneza hadhi na heshima waliyonayo, hivyo kutokea mtu au kikundi cha watu kuja kuwachafua kirahisi kwa sababu binafsi si jambo zuri.

Kwa sisi wadau wa kufuatilia mambo ya siasa huwa tunakutana na 'watumiaji wasumbufu' kwenye mitandao hii. Hawa ni wasumbufu kwa maana ya watu wanaovuka mipaka katika kupishana hoja kistaarabu hadi kufikia kashfa, matusi na udhalilishwaji.

**USHAURI**

Kutokana na mitandao ya kijamii kutengenezwa kwa mfumo wa kumvutia mtumiaji, wadau wanapaswa kuchukua tahadhari na kujidhibiti ili kuepuka kunogewa na kujikuta wanaitumia kila saa.

Wanapaswa kuepuka kugusagusa simu zao kuepuka 'mafuriko ya habari' za kisiasa zinazotoka kila saa, ambazo yawezekana nyingine mtumiaji hazihitaji.

Hii itasaidia wadau kuzidisha uzingativu wa shughuli wanazofanya kwenye maeneo yao ya kazi.

Lazima wadau wakumbuke kuwa mitandao ya kijamii ina mchanganyiko wa habari nyingi za ukweli na uongo na hivyo watumiaji wanapaswa kuwa makini na ikiwezekana kufuatilia habari iliyotolewa kwa kina ili kujua ukweli wa taarifa iliyotolewa.

Vipo vyanzo makini kwenye mitandao ya kijamii ambavyo vina hadhi (status) ya kutoa habari za ukweli, tuvitumie.

Kwa upande wa kumdhibiti mtumiaji msumbufu, njia pekee ya kukabiliana naye ni kumzuia kwa sababu jaribio lolote la kumuelimisha hata liwe la kistaarabu kiasi gani, litaishia kuzua balaa zaidi.

***Kwa maoni, mwandishi anapatikana kwa barua pepe franciscompangala08@gmail.com***

# Mahakama kuwaengua Wakurugenzi kusimamia uchaguzi, wadau wanena

## • Serikali kukata rufaa

**Na Sabato Kasika**

KATIKA vikao vya Bunge, Juni mwaka jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Mkuchika, alikaririwa na vyombo vya habari akiwashauri wabunge wanaopinga wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi, kupeleka hoja bungeni ili sheria ibadilishwe.

Alikuwa akimjibu Mbunge wa Mtambile, Masoud Abdalah Salum (CUF), aliyeuliza kama Serikali iko tayari kubadilisha sheria iliyowaweka wakurugenzi kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

Mbunge mwingine Ruth Mollel, Viti Maalum (Chadema), alidai wakurugenzi hao ni wanachama wa CCM walioshindwa katika kura za maoni, na kisha akauliza kama serikali iko tayari kutoa kauli endapo atapeleka orodha wakurugenzi wa aina hiyo.

"Mkurugenzi yeyote anayeteuliwa ni lazima awe na chama anachokipenda... nchi zote duniani rais aliyepo madarakani anapanga watu wake, hivyo kwa yeyote anayeona hakutendewa haki aende mahakamani," ndivyo Mkuchika alikaririwa na vyombo vya habari akijibu.

Sasa ni karibu mwaka tangu waziri atoe kauli hiyo, hatimaye Mahakama imetoa uamuzi kuhusu wakurugenzi hao kufuatia kufunguliwa kwa kesi ya kupinga wakurugenzi kusimamia uchaguzi.

Kumekuwapo na malalamiko ya muda mrefu kutoka vyama vya upinzani kuhusu utendaji wa wakurugenzi, wakidai kwamba wanapendelea upande mmoja.

Wiki iliyopita Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, imetoa hukumu iliyobatilisha uhalali wa wakurugenzi wa majiji, manispaa na halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi nchini.

Mahakama hiyo ilibatilisha kifungu cha Sheria ya Uchaguzi Namba 7 (1) na 7(3) kinachowaruhusu wakurugenzi wa majiji, manispaa na halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi nchini.

Uamuzi huo ulitokana na Kesi Namba 8/2018, iliyofunguliwa na mwanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Bob Wangwe, akiwakilishwa na wakili wa kujitegemea, Fatma Karume.

Katika kesi hiyo, walipinga kifungu cha Sheria ya Vyama vya Siasa, kinachotumiwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (Nec), kuwateua wakurugenzi hao kusimamia Uchaguzi.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Atuganile Ngwala, alisema kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi, Kifungu namba 7(1) na 7(3) ni batili kwa sababu kinatoa nafasi kwa wateule wa rais ambao pia si waajiriwa wa Nec, kusimamia uchaguzi.

Kwamba kifungu cha 7(1), kinasema kila Mkurugenzi wa Jiji, manispaa na halmashauri anaweza kusimamia uchaguzi, wakati viongozi hao ni wateule wa rais na si waajiriwa wa Nec, huku Katiba inasema Nec inapaswa kuwa huru na haki.

Kutokana na hali hiyo, Jaji Ngwala alisema kifungu hicho kinakinzana na Katiba mama ambayo inasimamia nchi.



Jaji Kiongozi Eliezer Feleshi. **PICHA: MTANDAO**

> Sijajua serikali itachukua hatua gani, lakini niishauri kwamba iandae muswada wa marekebisho ya sheria hii na kuupeleka bungeni ili kupata wasimamizi watakaoaminiwa na umma wa Watanzania.

Aliongeza kuwa kifungu cha 7(3) kinasema kuwa Nec inaweza kuteua mtu yeyote kuwa msimamizi wa uchaguzi bila ya kuainisha ni mtu wa aina gani.

Alifafanua kuwa Katiba inasema mtu yeyote aliyekuwa msimamizi wa uchaguzi hapaswi kuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa.

Kutokana na vielelezo vilivyowasilishwa mahakamani hapo na upande wa waleta maombi, vimeonyesha pasi na shaka kuwa wasimamizi wa uchaguzi wana maslahi na wateule wao.

Kufuatia hukumu hiyo kuwapiga 'stop' wakurugenzi kusimamia uchaguzi, wadau mbalimbali wa siasa walizungumza na gazeti hili na kutoa maoni yao kulingana na jinsi wanavyoichukulia hukumu hiyo.

### DEUSI KIBAMBA

Huyu ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania, ambaye anasema uamuzi wa Mahakama ni sehemu ya kazi kubwa ambayo wao wanaendelea kuifanya ya kupigania Katiba.

"Huu ni ushindi wa wapenda demokrasia... Tunaendelea kunyofoa kidogo kidogo vitu ambavyo vimekuwa ni kikwazo katika demokrasia na sasa tunaendelea na utaratibu wa kuwezesha mawakili ili kufungua kesi zenye maslahi ya umma ili ziweze kupatiwa ufumbuzi," anasema Kibamba.

Kibamba anasema suala wakurugenzi kusimamia uchaguzi wamelipigia kelele kwa miaka mingi ikiwamo kushawishi wabunge wawaunge mkono, lakini juhudi hizo zilikuwa hazijazaa matunda.

"Tunaamini kwamba wakurugenzi hawawezi kutenda haki katika uchaguzi, lakini ushawishi wetu kwa wabunge ulikuwa haujazaa matunda...bahati nzuri Bob Chacha Wange akafungua kesi na hatimaye Mahakama ikatoa uamuzi huo," anasema na kuongeza:

"Sijajua serikali itachukua hatua gani, lakini niishauri kwamba iandae muswada wa marekebisho ya sheria hii na kuupeleka bungeni ili kupata wasimamizi watakaoaminiwa na umma wa Watanzania."

Anaishauri serikali isihangaike kukata rufaa kwa madai kwamba kufanya hivyo ni sawa na kupoteza fedha za umma, ikizingatiwa kuwa Rais wa nchi anapinga matumizi mabaya ya fedha za umma.

### JOHN MREMA

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mambo ya Nje, Mawasiliano, Itikadi na Uenezi wa Chadema, John Mrema, anasema chama hicho kinapongeza uamuzi huo wa mahakama kwa uamuzi huo na kupendekeza mambo kadhaa yanayoweza kusaidia nchi kuendesha uchaguzi vizuri.

"Unaweza kuwekwa utaratibu mpya wa kuteua wajumbe wa tume watakaosimamia uchaguzi nchini, tofauti na huu uliopo sasa na hili litafanikiwa kwa kufanya utafiti kwa majirani zetu," anasema Mrema.

Anatolea mfano Kenya na kusema Tanzania inaweza kujifunza kutoka huko jinsi walivyopata wajumbe wa tume yao, ikiwamo kuangalia vigezo na kufanyiwa udahili.

"Nchi za wenzetu kama Ghana na Afrika Kusini wanafanya hivyo na siyo vibaya ukawapo mfuko maalum wa tume hiyo na pia ni vyema kuondolewa kwa zuio la kuishtaki tume mahakamani," anasema.

Anataja mapendekezo mengine kuwa ni matokeo ya urais kupingwa mahakamani, wanaopita bila kupingwa wapigiwe kura ya ndiyo au hapana na wasipofikisha asilimia 50, wahesabiwe kuwa wameshindwa.

"Jambo lingine ni kuruhusiwa kwa mgombea binafsi katika ngazi zote za uongozi ili kwamba makundi mbalimbali kwenye jamii yaweze kupata wawakilishi kuliko kutegemea kupitia katika vyama vya siasa," anasema.

### DK. ATHUMAN KIHAMIA

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi (Nec), Dk. Athuman Kihamia, baada ya hukumu hiyo alikakaririwa na vyombo vya habari akisema anasubiri nakala ya hukumu kutoka mahakamani.

Anasema hukumu hiyo ambayo imebadilisha kifungu cha Sheria ya Uchaguzi namba 7(1) na 7(3) kinachowaruhusu wakurugenzi wa majiji, manispaa na halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi ataipata kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) ndipo atajua cha kufanya.

### MWANASHERI MKUU WA SERIKALI

Profesa Adelardus Kilangi, ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), anasema serikali imewasilisha notisi Mahakama ya Rufaa kupinga sehemu ya uamuzi wa Mahakama Kuu katika kesi hiyo.

"Maamuzi ambayo serikali imeyakatia rufaa kuwa ni pamoja na Mahakama Kuu kubatilisha vifungu 7(1) na 7(3) vya Sheria ya Taifa ya Uchaguzi vinavyowataka wakurugenzi wa majiji, halmashauri, miji, wakurugenzi wa wilaya na wateuliwa wa Nec kutoka katika utumishi wa umma kusimamia uchaguzi kwa vile vinakinzana na Ibara ya 74(14) ya Katiba inayozuia anayehusika na uchaguzi kujiunga na chama chochote cha siasa," anasema.

Profesa Kilangi anasema pamoja na kwamba Ofisi yake haijapokea nakala ya hukumu, lakini tayari imewasilisha Mahakama ya Rufaa kupinga baadhi ya vifungu vilivyobatilishwa na Mahakama Kuu.

Mwanasheria huyo anasema mlalamikaji, Wangwe alitaka Mahakama ibatilishe Kifungu cha 6(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi kinachomtambua Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye anateuliwa na Rais

kwa madai kinakinzana na Ibara ya 21(1), 21(2) na 26(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

"Serikali inapinga hoja hizo kwani wakurugenzi ambao mlalamikaji anataka wanyang'anywe jukumu la kusimamia uchaguzi, hutekeleza jukumu hilo kwa kubanwa na masharti yanayosimamia uchaguzi chini ya Sheria za Uchaguzi na huwajibika chini ya sheria hiyo si vinginevyo," Prof. Kilangi anasema.

# Hadhi ya Bobi Wine upinzani nchini Uganda yapanda zaidi



Kiongozi wa upinzani nchini Uganda Dk. Kizza Besigye (kushoto), Rais wa Uganda, Yoweri Museveni (katikati) na mwanasiasa kijana anayeinukia nchini humo Robert Kyagulanyi maarufu kama Bobi Wine. **PICHA: MTANDAO**

**Na Nimi Mweta**

HADHI ya kiongozi wa upinzani kijana nchini Uganda, inapanda kwa kasi baada ya mgombea urais wa miaka mingi, Dk. Kizza Besigye kufanya mazungumzo rasmi na mbunge huyo wa Kyadondoi Mashariki, Robert Kyagulanyi maarufu kama Bobi Wine.

Pia kuna chama kinachoitwa Uganda Meritocracy Party (UMP), ambacho mwezi Februari kilifanya mazungumzo na mbunge huyo kuhusu matumizi ya nembo 'people power' ambayo ipo siku nyingi ila sasa imeanza kuambatanishwa na kampeni ya Bobi Wine.

Isitoshe, kupanda haraka katika chati ya siasa nchini Uganda kwa Bobi Wine kuanzia 2017 kumempa umaarufu duniani kama mbadala wa rais wa sasa.

Ilifikia mahali, tena ni mwaka 2017 akawaasa wananchi wa Uganda na hasa vyombo vya habari kumwita kiongozi na siyo mwanasiasa, huku wachunguzi wa habari katika nchi kadhaa wakimfananisha na kiongozi wa upinzani Afrika Kusini, Julius Malema.

Malema alikuwa kiongozi wa umoja wa vijana ANC na sasa 'wanagawana nyara.'

Chama chake cha 'kupigania uhuru wa kiuchumi' (RFF) kimezidi kupanda chati katika chaguzi tangu 2014 wakati aliposhiriki kwa mara ya kwanza alipohama kutoka ANC mwaka 2012 na kuunda EFF mwaka uliofuata.

Viongozi hawa wanafuata jadi ya Erneto Che Guevara aliyevuma kwa 'beret' nyekundu Cuba hadi akafa 1967 akiongoza vikundi vya kimapinduzi katika mapori Bolivia dhidi ya utawala unaoendeleza 'ukoloni mamboleo.'

> Mwaka jana Bobi Wine alikwepa au kukataa kujiunga na chama kikongwe cha upinzani cha FDC (Forum for Democratic Change) kinachoongozwa kihistoria na Dk. Besigye.

Suala la matumizi ya nembo ya 'people power' ilitokana na msisitizo wa Kyagulanyi katika hotuba zake na mahojiano kuwa 'nguvu ya watu ni zaidi ya nguvu ya watu walioko madarakani,' ambayo wachambuzi wa habari wanasema ilitoka kwa mwanaharakati wa Misri.

Ni Wael Ghonim ambaye alikuwa mstari wa mbele katika 'maandamano yasiyoisha' ya mwaka 2011 yaliyomwondoa Rais Hosni Mubarak madarakani.

Ni mshiriki wa mitandao na mtaalamu wa mifumo ya kompyuta, akaandika kumbukumbu ya harakati hizo kwa jina taaluma la Mapinduzi 2.0 (kana kwamba ni somo la mwaka wa pili chuo kikuu) usemi huo ulitolewa na ukaenea duniani.

Kuingia katika siasa rasmi za vyama vya siasa kulianza tangu Bobi Wine aliposhinda kiti cha ubunge mwaka 2017 na 'kumkanyagia mbali' mgombea wa chama tawala, National Resistance Movement (NRM) kilichoko madarakani tangu kuzifagia serikali za kijeshi na kiharamia 1986.

Mwaka jana Bobi Wine alikwepa au kukataa kujiunga na chama kikongwe cha upinzani cha FDC (Forum for Democratic Change) kinachoongozwa kihistoria na Dk.Besigye.

Licha ya kuwa chama hicho hivi majuzi kilitangaza mwenyekiti mwingine, bado inaelekea Dk. Besigye ndiye kiongozi halisi ambaye ana uwezo wa kujadili masuala ya kimkakati na Bobi Wine.

Ni miezi miwili iliyopita ambako Bobi Wine alianza kuonekana kikamilifu katika shughuli za vyama vya siasa, pale mwanaharakati aliposhinda jimbo la Arua (manispaa).

Ni Kassiano Wadri ambaye aliapishwa kuwa mbunge mwezi Agosti, wakati miezi michache kabla hapo aliwahi kukamatwa na kuteswa na polisi, kwa mujibu wa maelezo yake mwenyewe, kama ambavyo Bobi Wine aliwahi kukamatwa na kufunguliwa kesi ya uhaini katika mahakama ya kijeshi.

Ni jambo ambalo katika mazingira tofauti ingekuwa ndiyo mwisho wa kumsikia, lakini mazingira ya kitaifa na kimataifa hayawezeshi kwa urahisi siasa za mkato za aina hiyo, zisiwashe moto nchini.

Kimsingi wabunge hao wawili wa kujitegemea wana wafuasi wengi lakini hawana nguvu ya chama cha siasa, ingawa wamekuwa wanaharakati katika vyama vilivyopo huku kisiasa wakisimama kama watu binafsi.

Kutokana na umaarufu wake kupanda na kuhitajika kutokuchukua mwelekeo wa kugawa wafuasi wa vyama vikubwa vya upinzani vilivyopo sasa, Bobi Wine ameanza kutafuta maafikiano na vyama vikubwa vya upinzani, ikiwemo FDC ili kujiunga katika mwelekeo chanya unaoleta matumaini ya mabadiliko nchini humo.

Badala ya kupinga chama tawala cha NRM, Bobi Wine muda wote ameelekeza nguvu kutaka Rais Museveni atoke madarakani.

Ni kwa njia hiyo ambako inaelekea Bobi Wine anatazamia kuunda umoja mpana dhidi ya utawala huo katika kipindi kuelekea uchaguzi mkuu ujao, na ameshatangaza kuwa ana uwezo wa kumuondoa Museveni kitini endapo kunakuwa na uchaguzi huru na wa haki.

Ni mjadala mpana nchini humo ambako wengi wa washiriki hasa katika mitandao wanaonyesha hisia kuwa mfupa uliomshinda Dk. Besigye inawezekana Bobi Wine akawa na uwezo wa kuutafuna, iwe ni kumshinda Museveni kama uchaguzi ni huru na wa haki, au kukipatia taabu chama tawala kibaki na kichembe tu cha wingi wa viti bungeni. Ni mazingira ambayo yanajengeka polepole.

Mazungumzo ya hivi karibuni kuhusu matumizi ya nembo ya 'people power' yanatokana kwa upande mwingine na muungano wa kimkakati kati ya Bobi Wine na Dk. Besigye, wakati kuna kundi au chama cha siasa ambacho kinapenda kujitambulisha kwa nembo hiyo.

Ikafikia mahali kiongozi wa chama cha kisomi (Uganda Meritocracy Party) kinacholenga nchi hiyo kutawaliwa au kuongozwa na watu wenye weledi wa kutosha, kikasema kuwa anayetaka kutumia nembo ya 'people power' ajiunge na chama hicho, na punde akakataliwa katika jitihada ya kutaka hatimiliki ya 'people power' kuwa ya chama hicho. Ni kama "Movement for Change (M4C)' hapa, 2015.

Alipoona ugomvi huo hautamfikisha mbali, kiongozi wa UMP akaona aanze majadiliano na Bobi 'Wine pamoja na Dk. Besigye kuhusu matumizi ya nembo hiyo, kwani kuna wakati Dk. Besigye alianza harakati ya kuunda 'serikali mbadala' ya wananchi wa Uganda, kama ilivyokuwa Kenya na kwa ufinyu zaidi, Maalim Seif kule Zanzibar kwa miaka mingi.

Akizungumzia suala hilo Bobi Wine alisema amekuwa akifanya majadiliano na vyama tofauti vya siasa ikiwa ni pamoja na wafuasi na viongozi wa NRM, ambako kuna makubaliano mapana ya kuelekeza nguvu za upinzani katika kumwondoa madarakani Rais Museveni. Siyo suala la katiba mpya, mihula.

Moja ya vyanzo vinavyomsaidia Bobi Wine kupanda kisiasa ni kuwa anatokea katika familia ya wafuasi wa Democratic Party (DP), ambacho kimsingi ndiyo chama kikongwe cha upinzani wakati wa awamu ya kwanza ya Jamhuri ya Uganda hadi Jenerali Idi Amin alipopindua nchi mwaka 1971.

Wakati NRM imefagilia mbali utawala wa kijeshi uliovaa gwanda la kiraia la wafuasi wa Dk. Obote mwaka 1986, upinzani ulikuwa umeungana lakini miaka minane baadaye (2004) tofauti zikawa kubwa, na FDC ikaundwa na wafuasi wa NRM wasiokuwa na uvumilivu kwa kilichokuwa kinaendelea.

Kimejikita zaidi Kusini ya nchi hiyo, ambako miji mikuu ya Kampala na Entebbe pia ipo, lakini NRM imeshika viunga takriban vyote vilivyobaki kuacha Jinja, ambayo pia iko Kusini. Kuunda umoja mpana wa upinzani dhidi ya urefu wa utawala wa Museveni ni suala moja; la itikadi ni jingine.





# Kila kijiji kuwa na zahanati Mbarali 2020

**Na Grace Mwakalinga,**

**MBARALI**

SERIKALI wilayani Mbarali imejihakikishia kuwa hadi kufikia mwaka 2020 kila kijiji kitakuwa na zahanati na kila kata itakuwa na kituo cha afya lengo likiwa ni kusogeza huduma za afya karibu na wananchi.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani ambayo kiwilaya yalifanyika kwenye ukumbi wa polisi uliopo Kata Rujewa.

Mfune alisema katika kuboresha utoaji huduma za afya, atahakikisha ifikapo mwaka 2020 kila kijiji kitakuwa na zahanati na kila kata itakuwa na kituo cha afya na kwamba ataendelea kuhimiza pia ujenzi wa nyumba za watumishi wa sekta ya hiyo.

Alisema wauguzi ambao ndio kada yenye watumishi wengi kuliko zote wanatakiwa kutoa huduma rafiki kwa wagonjwa ikiwamo kuwahi maeneo ya kazi na kutoa lugha zenye staha.

"Kwa kipindi cha miaka mitatu nilichofanya kazi hapa mbarali sijawahi kupokea malalamiko yoyote yanayowahusu wauguzi, nawaomba muendelee kuwasaidia wagonjwa kwa kutumia weledi na ufanisi na utendaji kazi wenu uendane na mabadiliko ya sayansi na teknolojia," alisema Mfune.

Aidha, Mfune alimtaka Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Godfrey Mwakalila, kuweka utaratibu wa kutoa motisha kwa wauguzi ambayo wanafanya vizuri kwenye kazi zao na kwamba motisha hiyo italeta uwajibikaji.

Katika risala yao wauguzi walibainisha changamoto zinazowakabili ambazo ni kutopandishwa vyeo kwa wakati, kutolipwa malimbikizo ya nyongeza ya mishahara, uhaba wa maofisa tabibu, uhaba wa nyumba za watumishi, upungufu wa wauguzi kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Risala hiyo ilifafanua kuwa baadhi ya wazazi huchelewa kufika kwenye vituo vya kujifungulia hali inayosababisha baadhi yao kujifungulia njiani na kusababisha vifo.

**"Kwa kipindi cha miaka mitatu nilichofanya kazi hapa mbarali sijawahi kupokea malalamiko yoyote yanayowahusu wauguzi, nawaomba muendelee kuwasaidia wagonjwa kwa kutumia weledi na ufanisi na utendaji kazi wenu uendane na mabadiliko ya sayansi na teknolojia," alisema Mfune.**

# Mvua zasababisha mawasiliano kukatika

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MVUA zinazoendelea kunyesha katika wilaya za Rungwe na Kyela mkoani Mbeya, zimesababisha maafa ikiwamo nyumba kuezuliwa, mifugo kusombwa na uharibifu wa mazao na shughuli kusimama.

Wakizungumza na Nipashe jana wananchi wanaoishi katika Kata za Mwaya, Tenende na Ipande, wilayani Kyela walisema kuendelea kunyesha kwa mvua hizo kunaweza kusababisha majanga zaidi.

Miongoni mwa wananchi hao, Lutusyo Mwainyekule kutoka Kata ya Mwaya, alisema kuwa mvua hizo zimesababisha kukatika kwa mawasiliano kwenye barabara ya Ipinda- Matema katika eneo la Tenende ambayo ilizinduliwa hivi Karibuni na Rais Dk. John Magufuli.

Mwainyekule alisema eneo lote la Tenende ambalo ndio tegemeo kwa kilimo cha Mpunga kwa kiasi kikubwa limeathiriwa na mvua na kusababisha mpunga kufunikwa. "Kwa sasa wananchi wanaoishi maeneo ya Ipinda na Mwaya wanashindwa kufika mjini Kyela kwa sababu ya kukatika kwa mawasiliano ya barabara katika kipande cha Tenende na kulazimu kutumia mitumbwi au baiskeli kuvushwa," alisema Mwainyekule.

Nao wananchi wa maeneo ya Kata ya Bujonde, walisema mvua hizo zimesababisha madhara kwao kutokana na mifugo yao kusombwa na maji kuelekea maeneo ya mto Kiwira na Ziwa Nyasa.

Katika taarifa yake Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema mvua zinazoendelea kunyesha wilayani Kyela zimesababisha uharibifu wa makazi ya watu na majengo hasa Shule ya Msingi Mwaya na Sekondari ya Mwaya zilizopo katika Kata ya Mwaya ambazo zote mpaka sasa zimezingirwa na maji.

Aidha, alisema katika Wilaya ya Rungwe maeneo ya Igamba, Tukuyu mjini imesababisha maafa ikiwamo kubomoka kwa nyumba za wakazi wa maeneo hayo.

Aliwataka wazazi na walezi katika wilaya za Kyela na Rungwe kuwa makini na watoto wao kwa kuhakikisha hawachezi kando ya mito au mabwawa.



Kaimu Mtendaji wa Kata ya Usanda, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini, Ester Pembelada, akizungumza na wananchi wa vijiji vya Kata hiyo, katika mkutano wa hadhara uliofanyika Kijiji cha Buchamike, kuhusu athari za vitendo vya kuwapa ujauzito wanafunzi na kuwaozesha ndoa za utotoni. **PICHA: MARCO MADUHU**

# TAG watoa msaada vifaa vya matibabu

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WAUMINI wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God 'TAG' Jerusalem Tempo lililopo eneo la Sokomatola jijini Mbeya, wametoa msaada wa vifaa huduma kwa ajili ya wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Kiwanja Mpaka ikiwa ni sadaka kwaajili ya madhimisho ya miaka 80 tangu kuanzishwa kwa kanisa hilo nchini.

Akizungumza katika maadhimisho hayo, Makamu Askofu wa Kanisa la TAG, Jimbo la Mbeya Kaskazini, Mchungaji Adson Mwajunga, alisema vifaa ambavyo vimetolewa ni pamoja na magodoro, mashuka na vyandarua na kwamba waumini walitoa kama sadaka ikiwa ni maadhimisho ya miaka 80 tangu kuanzishwa kwa kanisa hilo.

Alisema Kanisa la TAG kama sehemu ya jamii ambayo imekuwa ikishiriki kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo katika maadhimisho ya miaka 80 tangu kuanzishwa kwa kanisa hilo wameamua kusaidia watu mbalimbali hasa wenye uhitaji.

"Tunapoadhimisha miaka 80 tangu kuanzishwa kwa kanisa la TAG tunajivua mambo mbalimbali ambayo tumefanikiwa kimwili na kiroho, lakini hatuwezi kufurahia peke yetu wakati wengine wanateseka hospitalini ndio maana mwaka huu tumeamua kuwatembelea wagonjwa na kutoa misaada," alisema Mchungaji Mwajunga. Akipokea msaada huo Ofisa Maendeleo ya Jamii Jiji la Mbeya, Vicent Msolla, kwa niaba ya Mkurugenzi wa Jiji, James Kasusura, alisema msaada huo ni muhimu na umekuja wakati muafaka kutokana na uhitaji uliopo.

Msolla alisema kuna changamoto mbalimbali zinazoikabili Sekta ya Afya hasa kwenye zahanati na vituo vya afya ikiwamo uhaba wa vifaa tiba na miundombinu mingine ya kutolea huduma alisema msaada huo utasaidia kupungua baadhi ya changamoto ikiwamo mashuka.

Naye Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Kiwanja Mpaka, Stella Moses, alisema kituo hicho kinakabiliwa na changamoto ya vifaa tiba na kwamba hali inayosababisha baadhi ya huduma kutolewa kwa wakati.

Aliiomba serikali kutenga bajeti kwa ajili ya kukisaidia kituo hicho kwa kuongeza wahudumu wa afya, vifaa tiba na miundombinu mingine ya afya ili kituo hicho kiweze kutoa huduma bora kwa sababu kinahudumia wakazi wengi wa Jiji la Mbeya.





# Waziri Lugola aonya ubadhirifu wa fedha

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amewataka watumishi wa ofisi yake kujiepusha na ubadhirifu wa fedha za umma na matumizi mabaya ya madaraka kwa kisingizio cha ukosefu wa fedha.

Lugola alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo jijini hapa.

Alisema katika kipindi hiki ambacho serikali inaendelea kutekeleza miradi mikubwa ya kiuchumi kumekuwapo na matatizo ya kifedha.

"Hata hivyo matatizo hayo ya kifedha sio kichaka kwa watumishi wa umma kukosa uaminifu, kutumia vibaya madaraka yao, kufanyakazi kwa upendeleo na kuendekeza maslahi binafsi," alisema.

Waziri Lugola alisema katika mwaka huu wa fedha unaoishia Juni 30, kumekuwa na mtiririko mzuri wa fedha za bajeti ambazo zimewezesha watumishi kulipwa baadhi ya stahiki zao.

Alisema mabaraza ya wafanyakazi katika kila chombo na taasisi za wizara hizo yanapaswa kujadili kwa uhuru na uwazi upungufu mbalimbali na kutoa njia mbadala za utatuzi.

Alisema upungufu na udhaifu usemwe kwa uhuru na uwazi ili ufahamike na kutatuliwa.

"Pia watumishi hakikisheni mnazingatia sheria, kanuni na nidhamu katika kutimiza majukumu yenu kwa kuwa serikali inaendelea kuboresha mazingira bora kwa watumishi wa umma," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa baraza hilo, Ramadhani Kailima, alisema kuwa katika kikao hicho watajadili bajeti na changamoto za watumishi na kuishauri wizara hatua za kukabiliana na changamoto hizo. Kailima ambaye pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani, alisema changamoto zote zitapokelewa na kutekelezwa.

Alieleza huwa baraza hilo ni chombo huru na kuwaomba watumishi wote waeleze changamoto zao kwa uwazi na zitafanyiwa kazi.



Baadhi ya kinamama wakiangalia ng'ombe wa maziwa wanaofugwa katika shamba la Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda, lililopo eneo la Zuzu, jijini Dodoma jana, wakiwa katika ziara ya mafunzo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Ikupa aisaidia UWT kujenga kituo cha watoto

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Stella Ikupa, ametoa msaada wa mifuko 30 ya saruji kwa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Dodoma (UWT), kwaajili ya kujenga kituo cha kulelea watoto jijini hapa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana baada ya kukabidhi mifuko ya saruji, Ikupa alisema kuwa, anaupongeza uongozi wa UWT Mkoa wa Dodoma kwa ubunifu mkubwa ambao wameendelea kuufanya ikiwamo wa kujenga kituo cha kulelea watoto ambacho kitakuwa kama mradi.

"Nampongeza sana Mwenyekiti pamoja na wale ambao anaambatana nao, kutokana na na mradi huu naamini wataondokana na utegemezi," alisisitiza Ikupa.

Aidha, alisema msaada huo wa saruji utawasaidia kuwasogeza na kuwaomba wadau mbalimbali waweze kujitokeza kusaidia.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Dodoma, Neema Majura, alisema wanamshukuru Waziri Ikupa kwa kuwa na moyo wa kipekee kwa kuwaletea msaada huo kwaajili ya kukamilisha ujenzi wa madarasa matatu.

Alisema ingawa mradi huo ni wa CCM mkoa, lakini utasaidia wilaya zote saba zilizopo Dodoma.

"Na lengo letu mara baada ya mradi huu kuanza ambao utakuwa na thamani ya Sh. Mil. 200, utaweza kufanya UWT Dodoma kuwa endelevu na utasaidia miradi mingine kila wilaya ili wanawake waweze kupata vitega uchumi kwa kujitegemea," alisema Majumre.

## Wanawake watakiwa kuchangamkia fursa

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

WANAWAKE nchini wameshauriwa kuchangamkia fursa ya sera ya serikali ya kuanzishwa viwanda kwa kulima mazao yatakayowezesha kuzalisha bidhaa zitakazoendana na soko la ndani ya nchi na nje.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mbunge wa Viti maalumu kutoka Mkoa wa Mara, Agnes Marwa, wakati alipokuwa akizungumza na kikundi cha kinamama wa Jumuiya ya Wanawake Tanzania (UWT) Wilaya ya Musoma Vijijini walipofika kutembelea shamba la Waziri Mkuu mstaafu Mizengo Pinda eneo la Zuzu jijini hapa.

Marwa, aliwashauri wanawake kote nchini kuchangamkia fursa ya kuanzishwa kwa viwanda kwa kuzalisha bidhaa na kulima mazao yatakayonunuliwa na wenye viwanda kama malighafi.

"Mmefika hapa kutoka Mkoa wa Mara kwa ajili ya kujifunza kilimo na ufugaji kila mtu ajifunze na kwenda kuufanyia kazi mradi atakaoona anaweza kuendesha," alisema.

Alisema mikoa mingi nchini ina makundi mengi ya wakulima na wafugaji hivyo wanawake wanatakiwa kuitumia fursa ya viwanda kwa kuzalisha bidhaa zinazoendana soko.

Alizitaja fursa hizo kuwa ni kulima mazao yanayoweza kupata soko kwenye viwanda kama kilimo cha miwa, maembe, machungwa na maparachichi pamoja na kilimo cha mahindi na mtama.

Alisema mazao hayo pamoja na kuhitajika viwandani, lakini yanaweza kununuliwa na watu binafsi kwa matumizi ya kawaida bila kutegemea soko la viwanda.

Aidha, alitaja fursa nyingine kuwa ni kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya kuzalisha bidhaa zinazoendana na soko la wakati huu.

Alibainisha kuwa mafunzo hayo yatafanyika kwa awamu kwa kinamama wa mkoa huo kwenda kujifunza kilimo cha shamba darasa kwenye shamba hilo la Pinda.

Mwajuma Shabani, mmoja wa kinamama aliyefika kujifunza kilimo cha shamba darasa, alisema wamejifunza kilimo na ufugaji ambacho wataenda kuanzisha miradi kule wanakotoka.

Kwa upande wake mmoja wa wasimamizi wa shamba la Waziri Mkuu mstaafu Pinda, Mariamu Fissoo, alisema katika shamba hilo kuna kilimo cha mazao ya kudumu na ya muda mfupi.

Aliongeza kuwa katika shamba hilo kuna ufugaji wa mifugo ya aina mbalimbali kama ng'ombe, mbuzi, kuku, bata na kondoo.

**"Mmefika hapa kutoka Mkoa wa Mara kwa ajili ya kujifunza kilimo na ufugaji kila mtu ajifunze na kwenda kuufanyia kazi mradi atakaoona anaweza kuendesha," alisema.**



# Serikali yadhibiti kasi ya ugonjwa wa ukoma

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Afya Zanzibar, imesema imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kudhibiti kasi ya ugonjwa wa ukoma na kwa sasa wapo wagonjwa 82 walioripotiwa Zanzibar.

Naibu Waziri wa Afya, Harusi Said Suleiman, alisema hayo wakati akijibu swali la mwakilishi wa Viti Maalumu Wanawake, Sada Ramadhan Mwenda, aliyetaka kujua wizara hiyo imefanikiwa kwa kiasi gani kutokomeza ukoma.

Suleiman alisema jumla ya wagonjwa 82 wameripotiwa na kutambuliwa kuugua ugonjwa wa ukoma na Mkoa wa Mjini Magharibi unaoongoza kwa kuwa na wagonjwa 43.

Aliutaja Mkoa wa Kusini Unguja ukiwa na jumla ya wagonjwa 26, wakati huo ukionyesha kuwapo kwa unafuu mkubwa kwa kisiwa cha Pemba chenye wagonjwa wanne.

''Tumepiga hatua kubwa ya mafanikio ya kupambana na ugonjwa wa ukoma kiasi ya kusema kwamba tumeutokomeza,' 'alisema.

Alieleza kuwa wagonjwa waliopo wanaendelea na matibabu na dawa za ugonjwa huo zinatolewa bure.

Alisema si kweli kwamba wagonjwa wa ukoma wametengwa kwa sababu za kunyanyaswa kama wanavyodai watu wengine.

''Wagonjwa wa ukoma hawajatengwa hata kidogo...waliwekwa sehemu mbali na wananchi kwa ajili ya uangalizi zaidi wa ugonjwa huo pamoja na kupata tiba sahihi,' 'alisema.

# Rais Shein apongezwa na Wawakilishi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wampongeza Rais wa Zanzibar, Dk.Ali Mohamed Shein, kwa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ikiwamo kufanikisha kazi za utafiti wa nishati ya mafuta na gesi.

Wakichangia bajeti ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2019-2020, Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake, Suleiman Said Sarhani, alisema Dk. Shein ameonyesha mfano wa utekelezaji wa ilani pamoja na ahadi zake katika kusimamia miradi mingi ya maendeleo ambayo ipo kwa maslahi ya taifa.

Alisema kuanza kazi za utafiti wa nishati ya mafuta na gesi nchini ni moja ya ahadi ya Rais Shein ambayo imo katika mpango wa utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya mwaka 2015-2020.

Sarhani alisema wapo watu waliokejeli na kusema kwamba Zanzibar haiwezi kufanya kazi za utafiti wa nishati na mafuta.

''Mheshimiwa Spika, Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amefanya kazi kubwa ya kutekeleza Ilani ya chama cha Mapinduzi na leo hii tunaendelea na kazi ya utafiti wa mafuta na gesi katika ardhi ya visiwa vya Unguja na Pemba,'' alisema.

Aidha, Mwakilishi wa Viti Maalumu Wanawake, Amina Iddi Mabrouk, alimpongeza Dk. Shein kwa juhudi zake katika kufanya kazi kwa maslahi ya wananchi wa Unguja na Pemba.

Alipongeza kazi za ujenzi wa barabara pamoja na madaraja likiwamo la Fuoni Kibonde Mzungu ambalo sasa limewawezesha wananchi kupita bila ya matatizo.

''Tunampongeza kwa dhati kabisa Rais Shein kwa juhudi zake za kuimarisha miundombinu ya barabara kwa kujenga madaraja ambayo yamesaidia kurahisisha usafiri wa wananchi na mawasiliano,'' alisema.

Mwakilishi wa Jimbo la Konde, Omar Seif Abeid, alimpongeza Dk. Shein kwa kufanya maadhimisho ya sherehe za miaka 55 ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kisiwa cha Pemba.

Alisema wapo wapinzani ambao walidiriki kusema kwamba Pemba hakutafanyika sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar na maadhimisho yote yatafanyika Unguja.

''Tunampongeza kwa dhati Rais Shein kwa kuonyesha uzalendo wa kuwapenda wananchi wake wa visiwa viwili vya Unguja na Pemba na mwaka huu sherehe za miaka 55 zilifanyika Pemba kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka minane ya uongozi wake,'' alisema.



Wawakilishi Simai Mohamed Said wa Tunguu (kushoto), Ahmada Yahya Abdulwakil (katikati) na Suleiman Sarhani Said wa Chakechake, wakibadilishana mawazo nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi mjini Zanzibar jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Ziara ya Indonesia yaleta ushirikiano kiuchumi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Issa Haji Ussi Gavu, ameliambia Baraza la Wawakilishi kwamba ziara iliyofanywa na Rais Ali Mohamed Shein nchini Indonesia imeleta faraja kubwa na manufaa katika sekta ya ushirikiano wa kiuchumi na kilimo.

Gavu alisema hayo wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Ofisi ya Rais kwa mwaka wa fedha 2019-2020.

Aliyataja maeneo yaliyozungumzwa na kufikiya makubaliano ya ushirikiano ni pamoja na kilimo cha Mwani, Minazi pamoja na mpunga ambapo nchi hiyo imepiga maendeleo makubwa.

Katika kilimo cha mwani, Indonesia imeonyesha utayari kusaidia kazi za utafiti katika zao hilo na kuona wakulima wanapiga hatua katika kujenga viwanda vya kusarifu zao hilo kwa ajili ya kuongeza thamani.

Aidha, katika sekta ya uvuvi, kampuni ya uvuvi ya Indonesia pamoja na Shirika la Uvuvi la Zanzibar (ZAFICO), wametia saini hati ya maelewano kati ya pande mbili hizo katika kufanya utafiti na kujua kiwango cha samaki kilichopo Zanzibar.

Alisema malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwawezesha wavuvi wadogo kuvua samaki katika kina kirefu cha maji baada ya kuwezeshwa kwa kupewa boti.

''Hiyo ndiyo mikakati na malengo yetu ni kuwawezesha wavuvi wetu kuvua samaki kwa kutumia mbinu za kisasa na vifaa vitakavyowawezesha kufika katika bahari kuu,'' alisema.

Alisema tayari makubaliano kati ya Zanzibar na Indonesia katika sekta ya uvuvi yameanza kufanyiwa kazi na Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar.

Dk. Shein alifanya ziara nchini Indonesia Agosti 6, mwaka 2018 kwa mwaliko wa mwenyeji wake Makamu wa Rais wa nchi hiyo, Muhamad Yussuf Kalla.

Aidha, Gavu alisema Rais Shein alifanya ziara nchini Kenya akimuwakilisha Rais wa Jamhuri ya Muungano Dk. John Magufuli na kufanya mazungumzo ya ujirani mwema na viongozi wa kaunti ya Mombasa.Alizitaja akaunti ambazo Rais Shein alikutana na viongozi wake kuwa ni jumuiya ya kaunti ya ukanda wa Pwani, ambazo ni Mombasa, Lamu, Taveta pamoja na Tana River.

Aidha, walikubaliana kuanzisha ziara kwa viongozi ikiwamo magavana, wakuu wa mikoa na watendaji wengine.

# Serikali yasisitiza marufuku ajira watoto sekta tumbaku

**Na Mathias Canal, TABORA**

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesisitiza marufuku aliyoitoa hivi karibuni kuhusu ajira kwa watoto chini ya miaka 18 katika sekta ya tumbaku.

Hasunga alipiga marufuku hiyo juzi wakati akizungumza kwenye mkutano wa wadau wa sekta ya tumbaku katika hafla ya ufunguzi wa msimu wa masoko ya zao hilo mwaka 2019 iliyofanyika katika maghala ya kampuni ya Alliance One Wilaya ya Urambo mkoani hapa.

Alisema suala la ajira kwa watoto ni miongoni mwa mambo yanazuiliwa kwenye Sheria za kimataifa kupitia Shirika la Kazi Duniani (ILO) na Sheria za Ajira nchini, hivyo mdau yeyote atakayebainika kukiuka maelekezo hayo atashtakiwa.

"Nawasihi wadau wote tuendelee kupiga vita ajira kwa watoto katika tasnia ya tumbaku kwa kuwa ni eneo ambalo limeendelea kulalamikiwa na wadau," alikaririwa Hasunga.

Kadhalika, Hasunga alisema katika kuhakikisha zao la tumbaku linaendelea kutoa mchango mkubwa katika pato la mkulima na Taifa, Wizara imejiwekea malengo ya haraka yanayopaswa kutekelezwa ambayo ni pamoja na kukamilisha usajili wa wakulima wote wa tumbaku ifikapo Juni 30, 2019, kuwapatia vitambulisho na kuwaingiza kwenye kanzidata ili kupata takwimu za uhakika za maeneo wanayoolima na kuiwezesha serikali kusimamia upatikanaji wa pembejeo kulingana na mahitaji yao.

"Malengo mengine ni tumbaku yote inayovunwa na wakulima sasa inauzwa ifikapo mwisho wa masoko Julia 31, mwaka huu, huku akiiagiza Bodi ya Tumbaku kushirikiana na wakulima wote kusimamia kwa makini masoko ili tuweze kuanza mapema maandalizi ya zao la msimu wa 2019/2020," alisema.

Aidha, mipango mingine ni kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo kwa wakati kwa kuweka utaratibu wa kumwezesha mkulima kujitegemea kwa pembejeo ili aache kuwa tegemezi wa mikopo ya mabenki yenye riba kubwa.

Mhe Hasunga ameiagiza Bodi na Tume ya Maendeleo Ushirika kuhakikisha wanashirikisha wakulima kupitia vyama vyao kuweka akiba ya fedha kununua pembejeo kwa kukatwa kiasi watakachokubaliana wakati wa mauzo ya tumbaku.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (mwenye kofia), akimsikiliza Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Daniel Chongolo (kulia), alipokuwa akimpa tathmini fupi ya mafuriko yaliyotokea katika eneo la Jangwani katika mto Msimbazi, yaliyotokana na mvua zinazoendelea kunyesha jijini. Wa pili kushoto ni Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Aron Kagurumjuli na Ofisa Elimu wa Mkoa, Hamis Lissu. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Ujenzi hospitali ya wilaya waenda kasi

**Na Sabato Kasika**

KAZI ya ujenzi wa hospitali yenye hadhi ya wilaya katika Wilaya ya Musoma Vijijini mkoani Mara, ambayo ilianza hivi karibuni imeshika kasi na majengo nane yamekamilika kwa hatua ya msingi.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, John Kayombo, aliliambia gazeti hili kuwa majengo hayo ambayo msingi wake umekamilika ni ya maabara, dawa na mama na mtoto. "Majengo mengine ni ya OPD, mionzi, utawala, kufua nguo na la kuchomea taka, ambayo kazi ya kumwaga jamvi itafanyika siku chache zijazo," alisema Kayombo.

Kayombo alisema hospitali hiyo inajengwa kwenye kitongoji cha Kwikonero katika Kijiji cha Suguti, Jimbo la Musoma vijijini na kwamba ufyatuaji wa matofali unaendelea, na kwamba hadi sasa yapo 75,000.

"Juzi tulitembelea eneo la ujenzi wa hospitali tukiwa na Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, Mwenyekiti wa Halmashuri ya Musoma Vijijini, Charles Magoma na wengine, na kushuhudia jinsi kazi inavyofanyika kwa kasi kubwa...wananchi wamekubali kuchangia mradi huu kwa hali na mali ili kuhakikisha unakamilika," alisema.

Alisema Musoma Vijijini ina kata 21, vijiji 68 na vitongoji 374, na taratibu za uchangiaji zimewekwa , ambapo viongozi wa ngazi mbalimbali kwenye maeneo yao wanahamasisha uchangiaji huo.

"Wananchi hao pia wanaishukuru serikali kuu kwa kutoa Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo ndani ya jimbo la Musoma Vijijini, ambayo itawapunguzia kusafiri umbali mrefu kufuata huduma ya afya," alisema.

Alisema Musoma Vijiji ina kituo cha Afya kikubwa cha Murangi ambacho kimekuwa kihudumia wakazi wa vijiji mbalimbali na kwamba kwa sasa zahanati za Bukima na Mungango zimepanuliwa na kuwa vituo vya afya.

"Hii yote ni juhudi za serikali za kuboresha huduma ya afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na wananchi wa maeneo husika, ambao wamehamasisha kwa ajili kushiriki katika shughuli mbalimbali za maendeleo," alisema.

Alitolea mfano wakazi wa Kata ya Nyambono ambao kwa sasa wanajenga kituo cha afya ambacho ujenzi wake ulizinduliwa mwishoni mwa mwaka 2017 na Mbunge wa Musoma Vijijini, Prof. Sospeter Muhongo.

# Tishio la mgomo ununuzi pamba

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

BAADHI ya kampuni za kununua pamba mkoani Shinyanga, zimetishia kugoma kununua zao hilo kutoka kwenye vyama vya msingi vya ushirika (Amcos), kutokana na kuondoa gharama ya usindikizaji pamba hiyo hadi kwenye kampuni yao.

Hali hiyo ni tofauti na awali, hivyo kumwachia mzigo huo mnunuzi mwenyewe na kuogopa kuingia hasara.

Awali kampuni za kununua pamba zilikuwa zikitoa Sh. 45,000 kwa kila Amcos, ikiwamo gharama ya usindikizaji wa pamba hiyo hadi kwenye kampuni, lakini kwa mwaka huu wameondoa gharama hiyo na kumwachia mnunuzi mzigo huo wa kuwa anaisindikiza mwenyewe.

Mmoja wa wamiliki wa kampuni za kununua pamba mkoani Shinyanga, Ally Habshy wa Kampuni ya Afrishian, alisema jana kuwa kuondolewa kwa gharama hizo na Amcos Sh. 45,000 kutawatia hasara kubwa ya kutafuta watu wa kuwa wanaisindikiza pamba hiyo kwa kila gari.

Alisema utaratibu wa awali wa kulipa Sh. 45,000 kwa kila Amcos ulikuwa mzuri, ambapo wao walikuwa wakiisindikiza pamba yote ambayo wameinunua hadi kwenye kampuni zao, lakini kwa kuondoa ulipiaji wa gharama hizo kutawafanya kuingia hasara na hata kukatika mitaji yao na kufilisika.

"Tangu msimu wa kununua pamba uanze Mei 2, mwaka huu hakuna hata kampuni moja ambayo unaiona inanunua pamba kwa sababu ya kuogopa kupata hasara, na sasa hivi ukienda vijijini wakulima wameanza kulanguliwa zao hilo kwa Sh. 800 kwa kilo moja, tofauti na bei elekezi ya Serikali 1, 200," alisema Habshy.

"Hivyo sisi kama wanunuzi wa pamba tunaomba suala hili liangaliwe upya, irudishwe gharama ya kutoa Sh.45,000 kwa kila Amcos ili kutotutia hasara," alisema na kuongeza:

"Na bei ya manunuzi ni kubwa Sh. 1,200 kwa kilo moja, huku dola kweye soko la kimataifa inakuwa nazo hazieleweki mara inashuka."

Meneja wa Bodi ya Pamba Kanda ya Ziwa, Jones Bwahama, alisema suala la Amcos kuondoa gharama ya Sh. 45,000 iliazimiwa kwenye mkutano wa wadau wa pamba jijijini Mwanza, kwa madai pale wanapoisindikiza pamba hiyo na kuifikisha kwenye kampuni huambiwa kilo zimepungua.

Alifafanua kuwa kutokana na lawama hizo za upungufu wa kilo, ndipo wakaona ni vyema suala la kusindikiza pamba hiyo wawaachie wanunuzi wenyewe ili kukwepa lawama, na kukiri ununuzi haujaanza, isipokuwa vikao vinaendelea kwa kila halmashauri kupitisha wanunuzi.

Pia aliwataka wakulima wawe na subira kwa kutoiuza pamba yao kwa bei ya hasara ya kulanguliwa.

# Museveni: Nchi za Afrika ziondoe ukomo urais

**KAMPALA,** Uganda

MWEZI mmoja baada ya Mahakama ya Juu nchini Uganda kuunga mkono hatua ya bunge kuondoa ukomo wa kuwania urais nchini humo, Rais wa nchi hiyo, Yoweri Museveni ameyataka mataifa ya Afrika yaondokane na sheria zinazozuia viongozi wenye umri mkubwa kuwania urais katika nchi zao.

Rais Museveni anataka nchi za Afrika kukubali kubadilisha katiba zao na kuondoa vizuizi vinavyowakataza viongozi wenye umri mkubwa na wale ambao wametawala kwa muda mrefu kuwania urais.

Rais Museveni amesema kwamba ukomo uliowekwa kwenye katiba kama vile ukomo kwa mihula na ukomo kwenye umri vinazuia Afrika kuwa na viongozi wazuri na wenye uzoefu.

Rais Museveni anajiandaa kuwania katika uchaguzi wa urais mwaka 2021 na endapo akishinda, atakuwa mmoja wa viongozi wa Afrika waliotawala muda mrefu zaidi (miaka 40).

Bunge la Uganda limebadilisha katiba mara mbili na kumpa nafasi Rais Museveni kuwania kwenye kiti cha urais.

**Kuna nchi inayoitwa Tunisia, walifanya mageuzi lakini walimtafuta mtu mwenye umri mkubwa wa miaka 88. Na huyo ndiye anawasaidia kwa sasa.**

Mwaka 2005, bunge la Uganda liliondoa ukomo wa mihula na mwaka 2017 likaondoa ukomo wa umri wa miaka 75 na kumpa nafasi Rais Museven kuwania tena nafasi ya urais.

Rais Museveni alitoa mfano wa nchi ya Tunisia, kuthibitisha kwa nini watu wenye umri mkubwa wanapaswa kuendelea kuwa viongozi kwa nchi za Afrika.

"Ukiwa na mwenye umri mkubwa wa miaka 75 kwa nini unasema aende wakati anaweza kusaidia? Kuna nchi inayoitwa Tunisia, walifanya mageuzi lakini walimtafuta mtu mwenye umri mkubwa wa miaka 88. Na huyo ndiye anawasaidia kwa sasa," alisema Rais Museveni.

Mwanasiasa wa chama cha NRM, Mike Mukul, ameunga mkono hoja hiyo ya Rais Museveni na kusema nchi za Afrika zinapaswa kuzingatia nasaha ya Rais Museveni.

"Mambo ambayo Rais Museveni ametaja ni lazima tuanze kuyafikiria kama Waafrika sababu ukiangalia nchi ambazo zimeendelea, hawana ukomo kwenye katiba zao," alisema Mukula.

Hata hivyo, kauli ya Museveni imefutiliwa mbali na upinzani nchini Uganda, ukisema kuwa kauli hiyo inapotosha.

"Kauli hiyo ni potofu kwa sababu itasababisha nchi nyingi Afrika kuongozwa na watu ambao wataendelea kusalia madarakani, na iwapo watafariki, kuna hatari familia zao kuendelea kutawala, jambo ambalo halikubaliki," alisema Gawaya Tegule, mwanasiasa wa upinzani ambaye pia ni mwanasheria.

Wataalam kuhusu mambo ya utawala wanasema viongozi wakisalia muda mrefu madarakani wanapaswa kujihusisha na upendeleo, rushwa na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Kauli ya Museveni inakuja wakati huu nchi nyingi barani Afrika zinakabiliwa na maandamano ya kiraia kushinikiza viongozi wao kuachia ngazi. **RFI**



Raia wa Sudan wakiwa wamechoma moto matairi baada ya wenzao watano kuuawa, wakati wa shambulio lililotekelezwa na watu wasiojulikana. **PICHA: REUTERS**

## Watu sita wauawa Sudan licha ya muafaka kupatikana

**KHARTOUM,** Sudan

WAANDAMANAJI watano na mwanajeshi mmoja mwenye cheo cha meja wameuawa nchini Sudan, katika mvutano ulioibuka saa chache baada ya Baraza la kijeshi na viongozi wa waandamanaji kukubaliana juu ya taasisi za uongozi wa mpito.

Vifo hivyo vilitokea katika makabiliano mbele ya makao makuu ya jeshi la Sudan mjini Khartoum, ambako maelfu ya waandamanaji wameendelea kuweka kambi kwa wiki kadhaa, kulishinikiza jeshi kukabidhi madaraka kwa raia baada ya kuangushwa kwa Rais Omar al-Bashir.

Msemaji wa baraza la kijeshi lililojipa mamlaka ya kuongoza kipindi cha mpito, Luteni Jenerali Shams al-Deen Kabashi, alisema kwamba watu wenye silaha wasiojulikana wamejipenyeza katika maandamano hayo, na ndio waliofyatua risasi.

"Makundi kadhaa yakiwamo yanayounga mkono serikali iliyoangushwa wamejipenyeza kwa lengo la kuyahujumu mapinduzi," alisema Kabashi na kuongeza

"wameeneza uvumi, na siku mbili zilizopita walishambulia gari lililokuwa likigawa kifungua kinywa, na ni dhahiri jeshi halikuhusika."

Msemaji huyo aliyashutumu makundi hayo kueneza uvumi kwa madhumuni ya kugonganisha jeshi na kitengo chake cha kuingilia haraka katika mizozo. Alisema jeshi linaunga mkono maandamano, na kamwe halitowafyatulia risasi waandamanaji kwa sababu yoyote ile, ingawa pia halitavumilia matendo ya vurugu.

Vuguvugu la waandamanaji lijulikanalo kama 'Muungano kwa Ajili ya Uhuru na Mabadiliko' limekubaliana na maelezo hayo ya jeshi, kwamba waliosababisha vurugu ni wafuasi wa serikali ya zamani, walio na malengo ya kukwamisha majadiliano kati ya vuguvugu hilo na jopo la majenerali.

Mauaji hayo ya jana yalitokea baada ya jeshi na viongozi wa waandamanaji kuafikiana juu ya taasisi zitakazoiongoza nchi katika kipindi cha mpito.

Kulingana na msemaji wa vuguvugu la waandamanaji, Taha Osman, taasisi hizo ni baraza kuu, baraza la mawaziri pamoja na bunge. **DW**

# Waandishi kuishtaki mamlaka ya mawasiliano

**KAMPALA,** Uganda

WAANDISHI wa habari kutoka kampuni 13 za vyombo vya habari Uganda, walioagizwa wasifanye kazi na Mamlaka ya Mawasiliano nchini humo (UCC), leo wanatarajia kufungua kesi kupinga agizo hilo.

UCC iliziambia kampuni hizo zichukue hatua dhidi ya baadhi ya wasimamizi, wakuu wa vipindi baada ya kukiuka maadili ya utangazaji katika kuripoti matukio yanayomhusu mwanasiasa wa upinzani na mkosoaji wa serikali, Bobi Wine,

Kesi hiyo inayotazamwa kama mtihani mkubwa kwa uhuru wa vyombo vya habari nchini Uganda.

Waandishi kadhaa wa habari wamepewa majukumu mbadala ya muda kwa mwezi ila hawakusimamishwa kazi, kukisubiriwa matokeo ya kesi hiyo.

Katika mkutano wiki iliyopita na wamiliki vyombo vya habari, Mkurugenzi Mtendaji wa UCC, Godfrey Mutabazi, aliridhia kwamba waandishi waliotuhumiwa wakae kando wakati wa uchunguzi, kubaini iwapo tabia ya mtu iliambatana na kilichokuwa kinatangazwa hewani.

Muungano wa waandishi habari Uganda (UJA) unataka mahakama iizuie mamlaka hiyo ya mawasiliano dhidi ya kuagiza kusimamishwa kazi mara moja kwa waandishi habari hao.

Kadhalika, wanataka mahakama itoe agizo la kuizuia UCC kupata kanda ya taarifa ya habari iliyotangazwa Aprili 29.

Mei Mosi, 2019, mamlaka nchini Uganda zilitoa madai ambayo uhuru wa vyombo vya habari nchini humo na ukanda mzima wa Afrika Mashariki ulivyo mashakani.

Amri iliyotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano ya Uganda (UCC) imeagiza vituo 13 vya redio na Televisheni kuwafuta kazi ndani ya siku tatu waandishi waandamizi 39 kwa kutoa habari zilioitwa kuwa ni za upotoshaji na kuchochea ghasia kwa kutangaza taarifa zilizo na ujumbe wenye hisia kali.

Tume hiyo inasema kuwa vyombo hivyo vya habari vilikiuka kanuni ya kifungu cha 31 ibara ya 4 ya sheria ya mawasiliano ya Uganda ya mwaka 2013.

Japo kuwa haikufafanua jinsi sheria ilivyokiukwa katika agizo lake kwa vyombo hivyo vya habari, Vituo vya redio vilivyoangushiwa rungu hilo ni Akaboozi, Beat FM, Capital FM, Pearl FM, Sapientia FM and Redio Simba.

Hatua hiyo dhidi ya vyombo vya habari imezusha tuhuma na shutuma kwa serikali kwamba inabana uhuru wa vyombo vya habari nchini Uganda. **BBC**

# Maliasili waanza kumsaka chui Goba

**Na Romana Mallya**

ASKARI wanyamapori wameweka kambi usiku na mchana maeneo ya Goba, jijini Dar es Salaam, wakimsaka chui aliyedaiwa kuonekana eneo la Zone C maarufu kwa Prof. Msanjila.

Mkurugenzi wa wanyamapori kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Maurus Msuha, alisema jana kuwa tangu wapate taarifa hizo walituma askari wao wenye silaha aina ya shotgun kwa ajili ya kumsaka chui huyo ambaye hadi wakati huo walikuwa hawajampata.

Alisema mbali na silaha hiyo wameagiza kuwekwe mtego ili kusaidia kukamatwa kwake.

"Hadi sasa askari wenye silaha wapo huko wanaendelea kumsaka, wananchi walisema walimuona amepita na baadaye alitokomea msituni," alisema.

Juzi, kulizagaa habari za kuonekana kwa chui maeneo hayo na kuzua taharuki kwa wananchi.

Taarifa iliyopo mtandaoni iliwataarifu wananchi wa Kibululu kuwa Ofisi ya Serikali ya Mtaa imewataka wachukue tahadhari kwa sababu kuna chui ameonekana maeneo ya Zone C.

## Dk. Bashiru awatemea

INATOKA UK. 3

Pia aliwashauri kuchapisha orodha ya mambo yanayotakiwa na yasiyotakiwa kufanywa na wadau mbalimbali wanapokuwa katika mazingira ya hospitali na kisha kuyasambaza katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Kadhalika, aliwashauri liundwe jukwaa litakalojumuisha wanataaluma wa afya, watafiti kutoka vyuo pamoja na asasi za kiraia ili kusaidia kutafsiri tafiti kwenda kwenye uhalisia, kutoa elimu ya afya kwa wananchi na ushauri wa kisera kwa serikali.

Taasisi hizo zilimwomba Dk. Bashiru awasisitize wanasiasa kuwatangazia zaidi wananchi kiasi cha fedha zinazotolewa na serikali kuliko fedha zilizotengwa.

"Hii itasaidia kukuza uelewa na kuzuia migongano kati ya wanasiasa na wanataaluma kwa upande mmoja na kutoa huduma na wananchi kwa upande mwingine," ilieleza taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilieleza mambo mengine yaliyozungumzia kuwa ni pamoja na mwenendo wa utekelezaji wa bajeti ya afya, sera ya msamaha wa matibabu kwa makundi mbalimbali na umuhimu wa kila Mtanzania kuwa na bima ya afya.

"Mazungumzo hayo yaligusia changamoto za rasilimali watu katika utoaji wa huduma za afya, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, majengo na miundombinu," ilisema.

Pia MAT na Sikika walieleza kuridhishwa kwao na juhudi zinazoendelea kufanyika katika sekta ya afya ikiwamo uboreshwaji wa huduma za kibingwa na ujenzi wa vituo vya afya.



Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Ukuzaji Viumbe Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Kajitanus Osewe, akichangia mada kwenye semina ya kimataifa ya wadau wa baraza la kilimo na zao la samaki, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Serikali yaanza uhakiki taasisi za kidini, kijamii

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetangaza kuanza uhakiki wa asasi za kijamii na za kidini nchi zima na ambazo hazitafanya hivyo kwa muda uliopangwa zitaondolewa kwenye orodha ya msajili.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali Jacob Kingu, uhakiki huo utafanywa na Ofisi ya Msajili wa asasi za kijamii na taasisi za kidini na wizara husika.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa awamu ya kwanza ya uhakiki huo itafanyika kuanzia Mei 20 hadi 30, mwaka huu katika Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani.

"Uhakiki utafanyika katika kituo cha uhakiki cha iliyokuwa Ofisi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, jijini Dar es Salaam kuanzia saa mbili kamili asubuhi hadi saa kumi kamili jioni," ilieleza taarifa hiyo.

Pia ilisema wakati wa uhakiki huo nyaraka ambazo zinatakiwa kuwasilishwa ni pamoja na cheti halisi cha usajili na kivuli cha cheti hicho.

"Stakabadhi ya mwisho ya malipo ya ada iliyolipwa hivi karibuni, katiba ya asasi au taasisi husika iliyopitishwa na msajili, barua inayothibitisha uwepo wa asasi au taasisi hiyo toka kwa Ofisa Mtendaji wa Mtaa au Kata mahali ilipo ofisi ya jumuiya au taasisi husika," ilifafanua.

Kadhalika, taarifa hiyo ilieleza kuwa fomu ya uhakiki inapatikana kwenye tovuti ya wizara hiyo kwa anuaniwww.moha.go.tz na kwenye kituo cha uhakiki.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kwa taasisi ambazo zitashindwa kuhakikiwa kwa mujibu wa ratiba ya eneo husika zitalazimika kwenda Makao Makuu ya Wizara Dodoma kwa ajili ya uhakiki na iwapo zitashindwa kufanya hivyo, zitaondolewa kwenye orodha ya msajili.

"Kwa taasisi za dini na asasi za kijamii ambazo hazijasajiliwa zinatakiwa kufika wakati wa zoezi la uhakiki kwa ajili ya kupewa utaratibu wa kupata usajili," ilisema.

Pia taarifa hiyo ilieleza kuwa malipo ya ada yatafanyika wakati wa uhakiki kupitia mfumo wa malipo ya serikali kwa njia ya kieletroniki.



TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


## KUPOTEA KWA CHETI



**Christina B. Mitole** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0203-0032** kilichotolewa na Baraza la Mitihani Taifa mwaka 2013 katika shule ya Sekondari Iringa Girls mwaka.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi taarifa:
**MBT/RB/1727/2019**

215226702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;105/2019**

Ombi la **VULI PHOCAS TEMU** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **PHOCAS EDWARD TEMU**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/05/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/05/2019.

215226502

---

**SHERIA YA UANDIKISHAJI WA ARDHI (SURA 334)**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB NA:**
**CDA/ED/LA-15/52939/4**

MMILIKI ALIYEANDIKISHWA: MOHAMED SHABANI KIMOLO

ARDHI: **KIWANJA NA.59 KITALU 'A' ENEO LA** NALA
MUOMBAJI:**GIDEON CHARLES MHAGAMA – MNUNUZI**

**TAARIFA IMETOLEWA,** Kwamba barua ya toleo iliyotajwa hapo juu imepotea na inakusudia kutoa hati milki mpya badala yake iwapo hakuna kipingamizi kwa muda wa siku thelathini (30) tokea tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa

BARUA YA TOLEO NAKALA HALISI
ikionekana,irudishwe kwa :

Mkurugenzi, Halmashauri ya Jiji, P.O.BOX 1249 DODOMA.
Imetolewa na:

115227802

---

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**OLIVER PAUL CHITANDA**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya TOYOTA ALTEZA. yenye namba za usajili **T875 DET.**
Chassis **No.10-0009740.**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

Taarifa Polisi.
**TAN/RB/362/2019**

215227102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA: 116..2019**

**Mdai: ……………………DAUD CHAGULILO**

**DHIDI YA**

**Mdaiwa: ………………..PHILIMON SAIMON**

**Kwa: PHILIMON SAIMON – MAFIGA MOROGORO**

**Ombi la Mdai: DAUD CHAGULILO**
**Madai ya: PESA ZA PIKIPIKI TSH. 1,585,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 23 mwezi 05 mwaka 2019 saa 02:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 09 mwezi 05 mwaka 2019.

115228802

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**Bimkubwa Hamad Said** anatangaza kupotelewa na vyeti vya kidato cha nne vifuatavyo : index namba **P.0309-0005,** kilichotolewa na shule ya Sekondari Fidel Castro mwaka 2003, na cheti chenye index **namba P.1304-0015** kilichotolewa na Shule ya Sekondari Chanja Mjawiri mwaka 2007.

Yeyote atakeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa :
**PCHKA/A.16/VOL.IV/1676/2019**

115226802

---

## KADI YA GARI IMEPOTEA

**HUSSEIN HASSANI ALLY**
anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA IST.** yenye namba za usajili **T399 CNT.**

Chassis No. **NCP610071148.**
Engine **No. 1NZB109764**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

Taarifa Polisi.
**TAN/RB/858/2019**

215226402

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Opportunity Tanzania** Ltd inatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili wa namba **MC 738 AUG** aina ya BAJAJI BOXER yenye chassis namba **MD2A2A822FWC72889,** Engine namba **PFZWFC76384.**

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/OST/RB/13869/2019**

215226602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;110/2019**

**Ombi la LUCY FRANSIS MASSAWE Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu AFRICAN AQWILINE MASSAWE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 17/06/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 14/05/2019.

115228702

---


KWA MATANGAZO

MADOGO MADOGO

TUPIGIE

0767 223311



JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# OZIL AMGOMEA EMERY KUONDOKA ARSENAL

**LONDON,** England

MPANGO wa Kocha wa Arsenal, Unai Emery kuhakikisha kwamba, kiungo Mesut Ozil anaondoka klabuni hapo unaonekana kugonga mwamba, baada ya mchezaji huyo kusisitiza kwamba hawezi kuondoka kwenye kikosi cha Arsenal.

Ozil awali aliripotiwa kwamba angeondoka kipindi cha majira ya joto kinachokuja na kwamba amesisitiza atabaki hapo kwenye dimba la Emirates hadi mwisho wa mkataba wake.

Kiungo huyo raia wa Ujerumani amekuwa kwenye mapito mengi chini ya kocha Emery, ambaye amekuwa akidai kwamba anapiga hesabu za kumuuza mchezaji huyo ili kupunguza bili ya mishahara kwenye kikosi chake.

Ozil, alisaini dili jipya linalomwingizia pauni 350,000 kwa wiki kwenye kikosi hicho Januari mwaka jana wakati timu hiyo ilipokuwa chini ya Arsene Wenger, lakini baada ya ujio wa Emery, mwanzoni mwa msimu ilionekana kama Mjerumani huyo anakwenda kufunguliwa mlango wa kutokea mwishoni mwa msimu huu.

Lakini, sasa kiungo huyo haonekani kuwa na mpango wa kuondoka, akipanga kubaki hapo akivuna mshahara wake mnono hadi mwisho wa mkataba wake.

Wakala wake, Dr Erkut Sogut, amesema wazi kwamba hakuna mpango wowote wa mteja wake kuondoka kwenye timu hiyo na Ozil mwenyewe alisema: "Nimebakiza miaka miwili kwenye mkataba wangu.

"Sielewi kitakachotokea baada ya hapo, lakini kwa wakati huu siendi kokote," alisema Ozil.

Mkataba wa sasa wa Ozil kwenye kikosi hicho cha Arsenal utafika tamati mwaka 2021.

# *Barca kumtumia Pique kumnasa Griezmann*

**BARCELONA,** Hispania

TIMU ya Barcelona imeripotiwa kumpa kazi beki wake mkongwe, Gerard Pique kuhakikisha anamshawishi nyota wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann ili kujiunga na klabu hiyo ya Nou Camp msimu ujao.

Griezmann, ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Ufaransa aligomea uhamisho wa kujiunga na Barcelona kwenye dirisha la majira ya joto mwaka jana, kwa kutangaza uamuzi huo kupitia video maalumu iliyorushwa kwenye televisheni katika fainali za Kombe la Dunia 2018, zilizofanyika huko Urusi.

Baada ya kutupwa nje ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Barcelona wanaripotiwa kumrudisha Griezmann kwenye mipango yao ya kumnasa ili aende kuongeza nguvu kwenye kikosi hicho.

Barcelona wamedaiwa kuwa na uhakika wa kumnasa mtu wao katika dirisha lijalo la usajili na hivyo kumpa Pique kazi ya kuzungumza na mshambuliaji huyo ili ajiunge nao.

Barca wanaamini watampata Griezmann baada ya kuthibitika kwamba Diego Godin, moja ya sababu zilizomfanya mshambuliaji huyo asihame Atletico mwaka jana, ataondoka mwisho wa msimu huu baada ya mkataba wake kufika tamati.




# Guardiola: Sijafikiria kuondoka Man City



**MANCHESTER,** England

KOCHA PEP Guardiola ameripotiwa kwamba, amewaambia mabosi wake pale Manchester City kuwa hajawahi kuwaza na wala hana mpango wa kuihama timu hiyo katika kipindi cha miaka miwili ijayo.

Raia huyo wa Hispania, Jumapili aliweka rekodi ya kuwa kocha wa kwanza kutetea ubingwa wa Ligi Kuu England katika kipindi cha muongo mmoja uliopita wakati kikosi chake cha Man City kilipoifunga Brighton.

Wapizani wao kwenye mbio za ubingwa huo, Liverpool walikuwa na mchezo Uwanja wa Anfield dhidi ya Wolves na licha ya ushindi, lakini wakazidiwa pointi moja na Man City.

Ubingwa wa ligi umewafanya Man City kujiweka kwenye nafasi bora kabisa ya kubeba mataji yote ya ndani ya England, kwani kabla ya hilo ilikuwa tayari imeshabeba ubingwa wa Kombe la Ligi na imetinga fainali ya Kombe la FA.

Guardiola sasa amewatoa hofu mabosi wake kwa kuwaambia bado yupo kwenye kikosi hicho baada ya hivi karibuni kuwapo na uvumi kwamba kocha huyo amewekwa kwenye mipango ya Juventus wakimtaka mwishoni mwa msimu huu.

Kutokana na hilo, Juventus sasa wamehamishia nguvu yao kwa kocha wa Tottenham Hotspur, Mauricio Pochettino, ambaye wanamwona kuwa ni mtu sahihi wa kwenda kuchukua mikoba ya Massimiliano Allegri.

# MAHREZ ARIDHIKA BENCHI MAN CITY



**MANCHESTER,** England

RIYAD Mahrez kamwe hakuwa na shaka juu ya uwezo wake wa kufiti kwenye kikosi cha Manchester City na hana mipango ya kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England.

Mahrez hajaanza katika kikosi hicho cha kocha Pep Guardiola kwenye mchezo wa ligi tangu Aprili 3, mwaka huu, lakini alijumuishwa kwenye kikosi cha kwanza cha City katika mchezo wa mwisho dhidi ya Brighton and Hove Albion Jumapili iliyopita ambapo walishinda mabao 4-1.

Nyota huyo wa zamani wa Leicester City ambaye aliwaongoza kutwaa taji la Ligi Kuu msimu wa 2015-16 na alilipa imani ya Guardiola kwake baada ya kutoa pasi ya mwisho kwa Aymeric Laporte aliyeifungia City bao la pili baada ya Sergio Aguero kusawazisha lile la Glenn Murray na yeye kufunga kipindi cha pili.

Na licha ya kutokuwa kwenye kikosi cha kwanza, Mahrez amesisitiza kwamba mara zote aliamini yupo kwenye ubora wake.

"Si rahisi kwa timu ambayo ina wachezaji wengi wa kucheza," alisema akiiambia Daily Mail.

"Kikosi kilifanya kila kitu msimu uliopita. Nilijua kwamba isingekuwa kazi rahisi katika mwaka wangu wa kwanza, lakini najiamini na sina shaka kuhusu ubora wangu.

"Nilijua kwamba kama nilikuwa na nafasi nililazimika kutumia vizuri, nitajitahidi. Nilifunga dhidi ya Brighton na niliisaidia timu."

Uvumi umeenea kwamba, Mahrez angeweza kuondoka hapo City mwishoni mwa msimu, lakini mchezaji huyo raia wa Algeria amekanusha tarifa hizo.

"Nina furaha kubwa kuwa hapa," ameongeza kusema Mahrez. "Siendi popote pale kwa sababu sichezi. Ni sehemu ya mchezo.

"Nahitaji kuwa imara. Ni sehemu ya maisha yangu. Kamwe sijawahi kuficha chochote."

City ambao pia wameshinda Kombe la EFL inaweza kushinda taji lingine kwani ipo kwenye fainali ya Kombe la FA dhidi ya Watford itakayopigwa Jumamosi.

# Robertson aiambia City Liver inakuja kuwashika



**LIVERPOOL,** England

ANDY Robertson ameionya Manchester City kwamba, Liverpool bado ipo imara baada ya 'Wekundu' hao kuukosa ubingwa wa Ligi Kuu England msimu huu wa 2018-19 na kwamba wajipange vilivyo msimu ujao.

Liverpool ilipoteza mchezo mmoja msimu huu na imekusanya pointi 97, hata hivyo, hazikutosha kuwafanya vijana hao wa Jurgen Klopp kumaliza juu ya Man City na walitarajia kubeba taji lao la kwanza tangu mwaka 1990.

Licha ya kushindwa kulibeba taji hilo msimu huu, beki huyo wa kushoto wa Liverpool, Robertson amesisitiza klabu hiyo ambayo imeipita kwa pointi 25 Chelsea waliopo nafasi ya tatu, itaendelea kupigana msimu ujapo ili kulibeba taji hilo.

"Man City wanajua na natumaini tutaendelea kupigana msimu ujao; Liverpool ipo hapa kuhakikisha inalibeba taji hilo, wametuzidi nguvu safari hii," alisema Robertson, ambaye timu yake ya Liverpool itacheza dhidi ya Tottenham kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya Juni Mosi, mwaka huu.

"Halafu timu zote zinatakiwa kutukamia sisi ili kumaliza wigo wao kati ya nafasi ya pili na tatu. Wote tunatakiwa kuja kwa pamoja na kama watafanya hivyo itakuwa bora zaidi kwenye mbio za ubingwa msimu ujao."

"Vidole vimefungwa na hatutapoteza kwa yeyote," aliongeza kusema Robertson. "Sisi ni kundi gumu na hatutaki kupoteza kwa yeyote. Tutakwenda msimu ujao tukiwa imara zaidi."

# Madrid, Hazard wamalizana

**LONDON,** England

NYOTA wa Klabu ya Chelsea, Eden Hazard anatarajiwa kutangazwa rasmi kuhamia Real Madrid mara baada ya mchezo wa fainali ya Kombe la Ligi ya Europa dhidi ya Arsenal Mei 29, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Gazeti la Marca la Hispania, Hazard ataondoka kwa miamba hao wa Stamford Bridge mwishoni mwa msimu huu.

Kwa misimu kadhaa sasa Real imekuwa ikihusishwa kutaka kumsajili nyota huyo, na kwa sasa ipo tayari kutoa kitita cha euro milioni 100 ambacho ni sawa na pauni milioni 86.

Hazard amekuwa akihusishwa kuwa pendekezo la kocha wa sasa wa Real, Zinedine Zidane raia wa Ufaransa.

Kwa mujibu wa Gazeti la L'Equipe, makubaliano kati ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 na Real Madrid tayari yameshafanyika wiki moja iliyopita, huku taarifa ikitarajiwa kutolewa mara baada ya msimu kumalizika rasmi.

Ukweli huo utawekwa wazi Mei 29, baada ya Chelsea kuikabili Arsenal. Hata hivyo, Chelsea imemaliza kwenye nafasi ya tatu Ligi Kuu ya England na hivyo kufanikiwa kukata tiketi ya kufuzu kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Hazard amebakiza mwaka mmoja pekee wa kuendelea kusalia pale Stamford Bridge kabla ya mkataba wake kumalizika.



# DONDOO SOKA MAGAZETI ULAYA



# HUYU RONALDO KAMA IBRAHIMOVIC-ALLEGRI

## ●●● Msimu huu aliongezea ubingwa wa Serie A na Kombe la Supercoppa Italiana...

**TURIN,** Italia

MASSIMILIANO Allegri, amekuwa akimfananisha Cristiano Ronaldo na Zlatan Ibrahimovic, ambapo kocha huyo amemsifu nyota huyo wa Juventus kama mwenye njaa ya mafanikio.

**Baada ya kutimka Real Madrid na kujiunga na Juventus kuelekea msimu wa 2018-19, mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or, Ronaldo, msimu huu aliongezea ubingwa wa Serie A na Kombe la Supercoppa Italiana katika orodha ya mafanikio yake.**

Ronaldo alitwaa ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo wakati akiwa Madrid, ambapo nyota huyo wa kimataifa wa Ureno pia alibeba 'ndoo' ya La Liga mara mbili, hiyo ikiwa pia sehemu ya mafanikio yake.

Straika huyo mwenye umri wa miaka 34, bado hajaonyesha ishara ya kuporomoka hapo Turin, akiwa amefunga mabao 21 Serie A na 28 katika mashindano yote kwa Juventus na Kocha Mkuu, Allegri akimfananisha na nguli Ibrahimovic - ambaye alifanya naye kazi wakiwa AC Milan.

"Kwa suala la mawazo, ni imara kuliko yeyote yule. Kila siku hupata malengo binafsi ya kuibua na anaweza kutafuta ndani yake mwenyewe," alisema Allegri, ambaye mwaka 2011 alitwaa Scudetto akiwa na Milan kabla ya kujiunga na Juve mwaka 2014.

"Mchezaji ambaye alishinda kila kitu alichonacho kwa umri wake wa miaka 34, atapata ugumu kujisikia njaa, lakini ana mauti kwa maana hiyo. Ana uamuzi huu ambao ni wa ajabu.

"Tunapaswa kujifunza kutoka kwa Ronaldo, na mimi pia nimejifuza, kwa sababu si kila mtu anapata nafasi ya kufanya kazi na mchezaji bora duniani.

"Kwa mfano, Jumamosi asubuhi tunamchezo kati ya safu ya mafunzo. Anafurahi, lakini furaha yake ni kushinda mechi. Nilimuelezea hilo, na niliandika kitu kama hicho kuhusu Ibra katika kitabu, wazo lake la kujifurahisha ni kushinda, lakini nilimwambia si kila mmoja yuko hivyo na kwa baadhi kuna furaha nyuma ya kisigino.

"Nilikuwa na Ibra Milan, ambaye kila siku anakuwa na hasira kwa kutopewa pasi sahihi na nilimwambia kama kila mmoja angekuwa na kipaji kama yeye pasingekuwa na tatizo.

"Nilimwambia yeye ndiye aliyepaswa kujiweka kwa wengine, kama vile wanaofaa zaidi na wenye vipaji lazima daima wafanye na wenzao.

"Ni vigumu kwa wengine kukua hadi kiwango hicho, kwa hiyo unapaswa kuwa na unyenyekevu kwa kutofanya kuwa vigumu kwa yeyote aliye chini yako. Hiyo ni kweli ya maisha na siyo tu kwenye soka, kwa maana hiyo Ronaldo ni mzuri sana. "

## ZISIKUPITE

### HAZARD KIMEELEWEKA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Mbelgiji Eden Hazard, 28, atakamilisha uhamisho wake wa pauni milioni 86 wa kujiunga na Real Madrid baada ya fainali ya Europa League. ***(L'Equipe - in French)***

### REAL YAIITIA SPURS BALE

REAL Madrid imeipa ofa Tottenham nafasi ya kumsajili mchezaji wao wa zamani, Gareth Bale kwa mkopo wa pauni milioni 10. Klabu hiyo ya Hispania pia itaitaka Spurs kutoa nusu ya ruzuku ya mshahara wa mshambuliaji huyo wa Wales kiasi cha pauni 600,000 kwa wiki. ***(Sun)***

### PSG YATEGA WATATU MADRID

PARIS St-Germain imetega mitego yao kwa wachezaji watatu wa Real Madrid, Gareth Bale, Kiungo Mhispania Isco, 27, na Kiungo Mjerumani Toni Kroos, 29. ***(Le Parisien, via AS)***

### UEFA KUISHUSHIA RUNGU UTD

WACHUNGUZI wa Uefa watapendekeza Manchester City kufungiwa kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa takriban muda mdogo wa mwaka mmoja kutokana na madai ya klabu hiyo kupotosha wasimamizi wa kifedha wa soka Ulaya. ***(New York Times)***

### CITY KUFANYA FUJO SOKONI

MABINGWA wa Ligi Kuu England, EPL, Man City wanapanga kutumia pauni milioni 200 majira haya ya joto kwa kukiimarisha kikosi chao kwa sababu ya kukabiliwa na vita ya kufungiwa kusajili. ***(Mail)***

### COUTINHO ASIKILIZIWA CHELSEA

BARCELONA inatarajia kupokea ofa kutoka Chelsea kwa kiungo wao Mbrazil Philippe Coutinho, 26, kama klabu hiyo ya Ligi Kuu England kifungo chao cha kusajili kitacheleweshwa. ***(Goal)***

### OZIL YUPO SANA ARSENAL

KIUNGO wa Arsenal, Mjerumani Mesut Ozil, 30, amesema hana lengo la kuondoka katika klabu hiyo. ***(Dazn Dach, via Mirror)***

### CHEEK AIKOMALIA CHELSEA

KIUNGO wa England, Ruben Loftus-Cheek, 23, atasaini tu mkataba mpya Chelsea kama atahakikishiwa nafasi ya kucheza kikosi cha kwanza. ***(Sun)***

### GRIEZMANN, ATLETICO KUTETA

ATLETICO Madrid itafanya mkutano na straika Mfaransa Antoine Griezmann, 28, wakati akielezwa tayari amekubali kujiunga na Barcelona. ***(Cadena Ser - in Spanish)***

### RYAN AKARIBIA TOTTENHAM

TOTTENHAM inakaribia kukamilisha dili linalogharimu pauni milioni 25 kumnasa beki wa kushoto wa Fulham, Ryan Sessegnon, 18. ***(Mail)***

### VERTONGHEN KUIWAHI LIVER

BEKI wa Tottenham na Ubelgiji, Jan Vertonghen, 32, anaamini atapona majeraha ya kifundo cha mguu na kuwa fiti kucheza mechi ya fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool Jumamosi ya Juni Mosi, mwaka huu. ***(Guardian)***

## ZFF yamfungia nyota Mafunzo mechi saba

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KAMATI ya Kusimamia Mashindano na Ligi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), imemfungia mchezaji wa timu ya soka ya Mafunzo, Mohammed Shaibu Haji, kutocheza mechi saba mfululizo pindi msimu ujao wa 2019/20 utakapofunguliwa.

Mchezaji huyo ambaye klabu yake inashiriki Ligi Kuu Zanzibar, amefikwa na balaa hilo kufuatia kudaiwa kufanya vitendo vya utovu wa nidhamu.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Hussein Ahamada aliliambia gazeti hili juzi kuwa mchezaji huyo siku mechi ya kufunga msimu wakati wakicheza dhidi ya Malindi alidaiwa kumpiga kiwiko mwamuzi wa kati, Mbaraka Haule aliyekuwa akichezesha mchezo huo kwa madai ya kutotendewa haki.

Hussein alisema adhabu ya mchezaji huyo imetolewa chini ya Kifungu cha 31 cha Kanuni ya kuendeshea mashindano na ligi ambacho kinazungumzia masuala ya nidhamu.

Aidha, alifafanua kwamba mchezaji huyo ataanza kutumikia adhabu yake hiyo mara tu baada ya kuanza kwa msimu ujao.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 36 | 26 | 5 | 5 | 55 | 25 | 83 |
| 2. Simba | 33 | 26 | 4 | 3 | 69 | 14 | 82 |
| 3. Azam | 36 | 19 | 12 | 5 | 50 | 21 | 69 |
| 4. Kinondoni MC | 36 | 11 | 16 | 9 | 36 | 25 | 49 |
| 5. Mtibwa Sugar | 35 | 14 | 7 | 14 | 36 | 29 | 49 |
| 6. Lipuli | 36 | 12 | 12 | 12 | 30 | 36 | 48 |
| 7.Singida United | 35 | 11 | 11 | 13 | 28 | 35 | 44 |
| 8. Ndanda | 34 | 11 | 11 | 12 | 22 | 31 | 44 |
| 9. Coastal Union | 35 | 10 | 14 | 11 | 31 | 41 | 44 |
| 10. Tanzania Prisons | 36 | 10 | 13 | 13 | 27 | 29 | 43 |
| 11. Kagera Sugar | 35 | 10 | 13 | 12 | 31 | 37 | 43 |
| 12. Mbao | 35 | 11 | 10 | 14 | 23 | 35 | 43 |
| 13. Ruvu Shooting | 36 | 10 | 12 | 14 | 33 | 41 | 42 |
| 14. Alliance | 35 | 10 | 11 | 14 | 28 | 38 | 41 |
| 15. Stand United | 35 | 11 | 8 | 16 | 33 | 44 | 41 |
| 16. Mbeya City | 34 | 12 | 7 | 15 | 35 | 36 | 43 |
| 17. Biashara United | 34 | 10 | 10 | 14 | 26 | 31 | 40 |
| 18. JKT Tanzania | 35 | 9 | 13 | 13 | 22 | 32 | 40 |
| 19. Mwadui | 35 | 10 | 7 | 18 | 38 | 48 | 37 |
| 20. African Lyon | 34 | 4 | 10 | 20 | 21 | 46 | 22 |

# AZAM FC WAPATA KAULI SARE SIMBA

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya timu yake kuambulia pointi moja kutoka kwa Simba msimu huu, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddi Cheche, amesema mvua iliyonyesha juzi jijini Dar es Salaam imemharibia mipango yake ya kuibuka na ushindi katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliowakutanisha kwenye Uwanja wa Uhuru.

**Katika mechi ya mzunguko wa kwanza Azam FC ikiwa chini ya Mholanzi Hans van der Pluijm ilichapwa mabao 3-1.**

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo juzi, Cheche alisema amehuzunishwa na kitendo cha kugawana pointi na Simba, kwa sababu timu yake ilikuwa bora na ilistahili kupata ushindi katika mchezo huo.

Cheche alisema aliwaandaa vema wachezaji wake kuwabana nyota wa Simba na mara zote anapokabidhiwa kikosi hicho hupata matokeo mazuri.

"Mvua iliharibu mchezo, wachezaji wameshindwa kufanyia vema yale tuliyotarajia kwa sababu hali ya maji uwanjani ilisumbua, napenda niseme nimepoteza pointi mbili, haikuwa matarajio yangu," alisema kocha huyo kiraka ambaye ni maalum kwa kuandaa wachezaji wa U-20 wa matajiri hao wa Chamazi.

Naye beki kisiki na nahodha wa Azam FC, Aggrey Moris aliliambia gazeti ili kuwa mechi ilikuwa ngumu kwa kila timu na hiyo ilitokana na kila upande kuundwa na wachezaji wenye uzoefu na wakakamavu.

Alisema walijipanga kulipiza kisasi na hiyo iliwasaidia kutoruhusu bao lolote kufungwa na wapinzani wao.

Azam yenye pointi 69 imebakiza mechi mbili ili kumaliza msimu huu, lakini ikiwa inasubiri kuwavaa Lipuli FC katika mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA itakayochezwa Juni Mosi kwenye Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi.



Nahodha wa Simba, Mohamed Hussein, akijaribu kumtoka beki wa kulia wa Azam FC, Nicholas Wadada, kwenye mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Uhuru juzi, huku mpira ukishindwa 'kutembea' kutokana na maji yaliyosabishwa na mvua kubwa iliyonyesha kabla ya mechi. **PICHA: MTANDAO**



# Timu 13 zashuka daraja Zanzibar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KATIBU wa Kamati ya Kusimamia Mashindano na Ligi ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Alawi Haidar Foum (pichani), amesema jumla ya timu 13 zilizokuwa zikishiriki ligi tofauti zinazosimamiwa na ZFF, zimeshuka daraja msimu huu wa 2018/19.

Miongoni wa timu hizo, nne zinatoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja na tisa zikitoka Daraja la Pili Taifa.

Kwa mujibu wa katibu huyo, timu za Daraja la Kwanza Kanda zilizoshuka. msimu ujao zitacheza Ligi Daraja la Pili Taifa na zile za Daraja la Pili Taifa zitacheza shiriki ligi za wilayani kwao zilikotoka awali.

Akizungumza na mwandishi wetu juzi, Foum alizitaja timu zilizoshuka kutoka Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja kuwa ni African Coast, Zantex, Mahonda Kids na Charawe.

Kwa upande wa timu za Daraja la Pili Taifa alizitaja kuwa ni Sharp Boy's, Shangani, Negro Fc, Kijanja, Mchangani, Mpapa, White Bird, Sebuleni na Supertiger.

Michezo
Jumatano Mei 15, 2019
Nipashe



Guardiola: Sijafikiria kuondoka Man City HABARI UK.28



Beki wa Azam FC, Aggrey Moris, akimdhibiti mshambuliaji wa Simba, Emmanuel Okwi katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Uhuru juzi na kumalizika kwa sare tasa. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Aussems: Hesabu sasa kwa Mtibwa

**Na Somoe Ng'itu**

TUTAZINDUKA! Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, amesema alijiua mapema kabla ya mchezo dhidi ya Azam FC kama atapoteza pointi kutokana na aina ya mfumo ambao wapinzani hao walikuwa wakicheza katika mechi hiyo ya Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ilimalizika kwa sare ya bila kufungana.

Hata hivyo, Aussems alisema anaamini timu yake itarejea katika kasi yake ya ushindi katika mechi zinazofuata ambazo ni dhidi ya Mtibwa Sugar ya Turiani, Morogoro itakayochezwa kesho na Ndanda FC kutoka Mtwara ambayo watavaana ifikapo Mei 19, mwaka huu, zote kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Aussems alisema wachezaji wake walifanya kila linalowezekana kuhakikisha wanafunga bao katika mechi hiyo dhidi ya Azam, lakini hali ilikuwa ngumu kwa sababu mabingwa hao wa Kombe la Kagame waliingia kwa dhamira moja ya kujilinda.

"Tulijaribu kutumia krosi, kucheza pasi za chini, kupiga mipira mirefu, lakini hatukufanikiwa, pia tulijaribu kucheza kupitia upande wa kulia, kushoto na katikati, lakini pia tulishindwa kufanikiwa, na unapogundua huwezi kupata ushindi, unajitahidi usipoteze pointi," alisema Aussems.

Mbelgiji huyo alisema anawapongeza wachezaji wake kwa kutokata tamaa ya kusaka ushindi kwa sababu wanajua bado malengo yao ya kutetea taji hilo hayajatimia.

"Tutajipanga vizuri katika mechi nyingine zinazofuata, Alhamisi tutacheza dhidi ya Mtibwa Sugar, halafu Ndanda, ingawa tunajiandaa kukutana na ushindani pia," aliongeza kocha huyo anayesaidiwa na Dennis Kitambi.

Mechi nyingine za Simba zilizosalia msimu huu ni dhidi ya Singida United (ugenini), Biashara United (Uhuru) halafu itasafiri kuwafuata Mtibwa Sugar katika mchezo wa marudiano ambao utafunga pazia la msimu wakati huu ikiwa na pointi 82, na ikihitaji pointi tisa ili iweze kutetea ubingwa.

# Yanga yarudi ilipodumu

### ●●● Tshishimbi aishusha Simba kileleni Ruvu Shooting ikiikimbiza mchakamchaka huku...

**Na Adam Fungamwango**

KWA mara nyingine tena Yanga imerejea kileleni mwa Ligi Kuu Bara ilipodumu kwa muda mrefu kabla ya wiki moja iliyopita mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba kukalia kiti hicho kwa muda mfupi.

**Simba ilishindwa kuendelea kumiliki uongozi wa ligi hiyo baada ya juzi kulazimishwa sare tasa na Azam FC, hivyo kuondoka na alama moja iliyowawezesha kufikisha pointi 82 baada ya michezo 33.**

Hata hivyo, Yanga jana iliibuka na ushindi katika mechi yao ya 36 msimu huu baada ya kuichapa Ruvu Shooting bao 1-0, shukrani sikimwendea mfungaji Papy Tshishimbi aliyeziona nyavu dakika ya 15.

Matokeo hayo yanaifanya Yanga kurejea kileleni mwa ligi hiyo kufuatia kufikisha alama 83 moja mbele ya Simba huku wanyonge wao katika mchezo huo, Ruvu Shooting wakibaki nafasi ya 13 na pointi zao 42.

Yanga sasa imebakiza mechi mbili dhidi ya Azam FC na Mbeya City kabla ya ligi hiyo kumalizika, wakati Simba ambayo kesho itashuka Uwanja wa Uhuru kuikaribisha Mtibwa Sugar, ina jumla ya mechi tano mkononi na ikihitaji kushinda michezo mitatu tu ili kutetea ubingwa wao.

Katika mechi hiyo ya jana, Tshishimbi aliyetumia udhaifu wa mabeki wa Ruvu Shooting dakika ambao walikuwa wamesimama kuweka mtego wa kuotea, akautegua na kuuwahi kabla ya kufumua shuti kali lililomshida kipa Abdallah Rashid na kujaa wavuni.

Dakika ya tano tu ya mchezo, Ruvu Shooting ilikosa bao la wazi, baada ya Full Maganga kuwatoka mabeki wa Yanga na kupiga mpira uliomshinda kipa Klaus Kindoki, lakini kabla haujavuka mstari wa goli, Kelvin Yondani aliuwahi na kuuokoa.

Haikuwa siku nzuri kwa Heritier Makambo aliyeikosesha Yanga mabao manne ya wazi ambapo kama angekuwa makini angeiwezesha timu yake kuibuka na ushindi mnono.

Dakika ya 30 akiwa yeye na kipa, akipiga shuti lililogonga mwamba na kurejea uwanjani, huku mengine akikosa dakika ya 37 na 40. Kipindi cha pili pia Makambo alikosa bao la wazi, huku Tshishimbi naye akikosa mawili.

Ruvu Shooting, ikicheza bila straika wake tegemeo Said Dilunga, iliwaendesha mchakamchaka Yanga hasa kipindi cha pili, lakini ilishindwa jinsi ya kuutumbukiza mpira wavuni.

Mastraika wao Emmanuel Martin anayechezea kwa mkopo akitokea Yanga na Maganga walikosa umakini jinsi ya kumtungua Kindoki ambaye alikuwa akitema sana mashuti yao.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >